# UCHANGANUZI LINGANISHI WA SINTAKSIA YA SENTENSI SHARTI YA KISWAHILI SANIFU NA EKEGUSII

**NA**

**FRANCIS ONYONKA NYANDAGO**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI WA SANAA KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**NOVEMBA 2013.**

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo kikuu chochote kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji ya shahada yoyote.

………………………………  ..................................

Sahihi  Tarehe

**FRANCIS ONYONKA NYANDAGO**

**C50/60796/2011**

(Mtahiniwa).

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika chuo kikuu.

…………………………………  ………………………………...

Sahihi  Tarehe

**DKT. PRISCA JERONO**

Mhadhiri, Idara ya Isimu na Lugha,
Chuo kikuu cha Nairobi.

…………………………………  …………………………………

Sahihi  Tarehe

**DKT. NYACHAE MICHIRA**
Mhadhiri, Idara ya Isimu na Lugha,
Chuo kikuu cha Nairobi.

## TABARUKU

Tasnifu hii ninawatabarukia mke wangu mpenzi Esther Nyamoita Onyonka, watoto wangu Allan Bisonga na Brevard Nyakundi.

**SHUKRANI**

Ningependa kuwashukuru wafuatao ambao walinifaa kwa njia moja au nyingine mpaka nikafika kiwango hiki. Sitaweza kuwataja wote ila kuwataja baadhi yao. Ningependa kuwaomba wale ambao sitawataja wawe na uelewa kuwa msaada wao ulikuwa wa manufaa makubwa kwangu. Ninawashukuru.

Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt. Priscah Jerono na Dkt. Nyachae Michira. Wawili hawa wamenipa muongozo na ushauri ambao umefanikisha tasnifu hii. Maoni na mawaidha yao yalikuwa tegemeo kubwa katika kazi hii. Ningependa kukiri hapa kuwa, kama kuna dosari yoyote iliyojitokeza katika tasnifu hii, lawama zote ni zangu wala si za wasimamizi hawa wawili.

Shukrani zangu ziwaendee wafuatao walionikuza kitaaluma hadi nikafikia kiwango hiki. Hao ni pamoja na Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Ayub Mukhwana, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Amir Swaleh, Dkt. Jefwa Mweri na Dkt. Kineene wa Mutiso. Wengine ni Bw. Gichobi Mungania, Dkt. Mwenda Mbatiah, Prof. John Habwe, Dkt. Rayah Timammy na Prof. Kyalo Wamitila. Mchango wa wataalam hawa wote hauna kifani.

Ninawashukuru wazazi wangu Wilson Nyandago Onyonka na Josephine Nyaboke Nyandago waliohakikisha wamenilea na kunipa uwezo mpana wa kushiriki na kutangamana na jamii pana ya ulimwengu. Ninamshukuru mama mkwe wangu Sabina Nyaboke kwa upendo wake dhidi ya familia yangu kwa ujumla. Aidha ninawashukuru ndugu zangu, dada zangu na mashemeji zangu wote kwa kuwa karibu nami na kunipa motisha wa kukamilisha yote yaliyohusiana na masomo yangu ya shahada ya uzamili.

Ninawashukuru wanadarasa wenzangu kwa ushirikiano wao wa kufana na ulionifaidi kitaaluma. Miongoni mwao ni George Ogutu, Ledemi Makange, Merolyne Otiende, Ombongi Motuka, Kennedy Owallah, Lily Koech, Ibrahim keter, Lydia Moraa na Caleb Chacha. Wengine ni George Muniu, Mary Nguti, Joshua Muriithi, Ruth Katutu, Juliet Okeyo na Justus Ndumbu. Wote hawa wakiwemo Florence Vutagwa, Rose Obiero na Chepngetich Rono walinifaa kwa mijadala mbali mbali tulioshiriki pamoja.

Shukrani maalum ni kwa mke wangu mpenzi, Esther Nyamoita Onyonka kwa mapenzi na ushirika mwema alionifaidi wakati wa panda shuka zote nilizozipitia nikiandaa tasnifu hii. Aidha ninawashukuru watoto wangu Allan Bisonga na Brevard Nyakundi ambao kwa njia moja au nyingine wananipa motisha wa kutekeleza yote yale niyaazimiayo.

Shukrani zangu ziwaendee walimu wenzangu Bw. Macharia Mugwe, Bi. Keziah Nderi na Bw. Obed Mwangi walionielewa wakati wa harakati za kuandaa tasnifu hii. Walinishika nami nikashikamana hadi tamati mwa maandalizi ya tasnifu hii.

Ninamshukuru Johnson Kamau Muthee aliyejisatiti kupiga chapa tasnifu hii licha ya changamoto alizokumbana nazo akivichora vielelezo tungo.

Ninashukuru chuo kikuu cha Nairobi kwa kunipa fursa ya kuendeleza masomo yangu ya shahada ya uzamili, yaani Master of Arts (M.A).

Mwisho ninamshukuru Mungu kwa kuwezesha kila jambo linalohusiana na masomo na maisha yangu kwa ujumla. Asante Mungu kwa yote ambayo sitaweza kuyataja hapa.

Kwenu nyote ninasema shukrani na Mungu awe nanyi daima.

# YALIYOMO


UNGAMO ........ ii

TABARUKU ........ iii

SHUKRANI ........ iv

ORODHA YA VIFUPISHO NA ISHARA ........ ix

ORODHA YA MICHORO ........ x

MUHTASARI ........ x

SURA YA KWANZA ........ 1

1.0.0 Utangulizi ........ 1

1.1.1 LUGHA YA KISWAHILI ........ 1

1.1.2 LUGHA YA EKEGUSII ........ 2

1.2.0 TATIZO LA UTAFITI ........ 3

1.3.0 SABABU ZA KUCHAGUA SOMO ........ 4

1.4.0 MADHUMUNI YA UTAFITI ........ 4

1.5.0 NADHARIA TETE ........ 5

1.6.0 UPEO NA MIPAKA ........ 6

1.7.0 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA ........ 7

1.8.0 MSINGI WA NADHARIA ........ 12

1.9.0 MBINU ZA UTAFITI ........ 19

SURA YA PILI ........ 21

2.0.0 UMBO, MAANA NA MATUMIZI YA SENTENSI SHARTI YA KISWAHILI ........ 21

Utangulizi ........ 21

2.1.1 FASILI YA SENTENSI SHARTI YA KISWAHILI ........ 22

2.1.2 UTEGEMEZI KATIKA SENTENSI SHARTI YA KISWAHILI ........ 24

2.1.3 KISHAZI SHARTI CHA KISWAHILI ........ 24

2.2.0 KITAMBULISHI CHA KISHAZI SHARTI CHA KISWAHILI ........ 27

2.2.1 KITAMBULISHI SHARTI ‘KAMA’ ........ 28

2.2.2 KITAMBULISHI SHARTI ‘IKIWA’ ........ 29

2.2.3 KITAMBULISHI SHARTI ‘ENDAPO’ ........ 30

2.2.4 KITAMBULISHI SHARTI ‘IWAPO’ ........ 31

2.2.5 KITAMBULISHI SHARTI ‘KI’ ........ 32

2.2.6 KITAMBULISHI SHARTI ‘NGA NA NGALI’ .......... 34
2.2.7 KITAMBULISHI SHARTI ‘NGE NA NGELI’ .......... 36
2.3.0 MUUNDO WA SENTENSI SHARTI YA KISWAHILI .......... 37
2.3.1 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘KAMA’ .......... 39
2.3.2 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘IKIWA’ .......... 43
2.3.3 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘ENDAPO’ .......... 47
2.3.4 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘IWAPO’ .......... 53
3.2.5 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘KI’ .......... 59
2.3.6 MUUNDO WA SENTESI YENYE ‘NGA NA NGALI’ .......... 63
2.3.7 MUUNDO WA SENTENSI YENYE ‘NGE NA NGELI’ .......... 70
2.4.0 HITIMISHO .......... 78
SURA YA TATU .......... 79
3.0.0 UMBO, MAANA NA MATUMIZI YA SENTENSI SHARTI YA EKEGUSII. .......... 79
Utangulizi .......... 79
3.1.0 SENTENSI SHARTI YA EKEGUSII. .......... 79
3.1.1 KISHAZI SHARTI CHA EKEGUSII .......... 80
3.2.0 KITAMBULISHI SHARTI CHA EKEGUSII .......... 83
3.2.1 KITAMBULISHI SHARTI ‘ONYE’ CHA EKEGUSII .......... 84
3.2.2 KITAMBULISHI SHARTI ‘-ISE’ CHA EKEGUSII .......... 85
3.2.3 KITAMBULISHI SHARTI ‘K-’ CHA EKEGUSII .......... 86
3.2.4 KITAMBULISHI SHARTI ‘-ARE’ CHA EKEGUSII .......... 87
3.2.5 KITAMBULISHI SHARTI ‘EBE’ CHA EKEGUSII .......... 89
3.3.0 MUUNDO WA SENTENSI SHARTI YA EKEGUSII .......... 90
3.3.1 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘ONYE’ .......... 92
3.3.2 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘-ISE’ .......... 97
3.3.3 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘K-’ .......... 102
3.3.4 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘-ARE’ .......... 109
3.3.5 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘EBE’ .......... 115
3.4.0 HITIMISHO .......... 120
SURA YA NNE .......... 123
4.0.0 ULINGANISHI WA SENTENSI SHARTI YA KISWAHILI NA EKEGUSII .......... 123
4.1.0 KAIDA YA NADHARIA YA UPANUZI WA SARUFI SAWAZISHI .......... 123

4.2.0 UAINISHAJI WA SENTENSI SHARTI YA KISWAHILI NA EKEGUSII .................................. 125
4.3.0 ULINGANISHI WA KISHAZI SHARTI CHA KISWAHILI NA EKEGUSII ................................ 127
4.4.0 ULINGANISHI WA VITAMBULISHI SHARTI VYA KISWAHILI NA ..................................... 131
EKEGUSII ........................................................................................................ 131
4.4.1 MAUMBO YA VITAMBULISHI SHARTI ........................................................................ 134
4.4.2 VITAMBULISHI SHARTI HURU ................................................................................ 134
4.4.3 VITAMBULISHI SHARTI FUNGE ............................................................................... 136
4.5.0 ULINGANISHI WA MUUNDO WA SENTENSI SHARTI YA KISWAHILI ........................... 139
NA EKEGUSII .................................................................................................. 139
4.5.1 SENTENSI ZENYE KITAMBULISHI KATIKA KISHAZI SHARTI NA ................................... 139
SHURUTIWA ................................................................................................... 140
4.5.2 MUUNDO WA SENTENSI ZENYE VITAMBULISHI KATIKA VISHAZI ............................... 145
SHARTI PEKEE ....................................................................................................... 145
SURA YA TANO ..................................................................................................... 153
5.0.0 HITIMISHO ....................................................................................................... 153
5.1.0 MAPENDEKEZO ................................................................................................. 156
MAREJELEO ........................................................................................................... 157

## ORODHA YA VIFUPISHO NA ISHARA

E – Kielezi

EK – Ekegusii

H – Kihusishi

KE - Kikundi kielezi

khj – Kama hapo juu

KIJ - Kijalizo

Kip – Kiambishi kipatanishi

KN – Kirai Nomino

KS – Kiswahili Sanifu

KIS – Kisaidizi

KT – Kirai Tenzi

N – Nomino

NJ – Njeo

n.k – na kadhalika

SB – Sarufi bia

S – Sentensi

SZGM – Sarufi Zalishi Geuza Maumbo

T – Kitenzi

Ts – Kitenzi kisaidizi

U – Kiunganishi

UF – Umbo kifonetiki

UM – Umbo Mantiki

Ø – Mofu kapa

* - Si sawa kisarufi

$\overline{S}$ - Kishazi kinachotangulizwa kwa kijalizo

**ORODHA YA MICHORO**

Kielelezo cha nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi…………………………..18

**MUHTASARI**

Lengo la tasnifu hii ni kufanya uchunguzi linganishi wa sentensi sharti ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii kwa kutumia nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi. Tumeigawa kazi hii katika sura tano. Katika sura ya kwanza, tumetoa maelezo ya kimsingi yanayohusu somo la utafiti, madhumuni ya utafiti na upeo wa tasnifu. Masuala mengine ambayo yameshughulikiwa ni pamoja na sababu za kulichagua somo, nadharia tete, yaliyoandikwa kuhusu somo hili, msingi wa nadharia na mbinu za utafiti.

Sura ya pili inalenga kushughulikia sintaksia ya sentensi sharti ya Kiswahili Sanifu. Sura imeanza kwa kutoa fasili ya sentensi sharti ya Kiswahili na ufafanuzi wa viambajengo vyake. Viambajengo hivi ni pamoja na kishazi sharti, kishazi shurutiwa, vitambulishi sharti na viunganishi viambatishi. Vipashio vinavyotumiwa kutolea masharti vimetambuliwa na kufafanuliwa. Vipashio hivi ni pamoja na 'kama, ikiwa, endapo, iwapo, ki, nga, ngali, nge na ngeli'. Suala lingine lililoshughulikiwa katika sura hili ni muundo wa sentensi sharti ya Kiswahili na ugeuzi unaojitokeza katika kuigeuza sentensi sharti kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo geuzi. Imebainishwa kuwa sentensi sharti ya Kiswahili ikiwa katika kiwango cha muundo msingi huwa na kishazi shurutiwa mwanzoni kikifuatwa na kishazi sharti. Vishazi hivi huunganishwa kwa mujibu wa kitambulishi sharti kinachokitegemeza kishazi sharti kwa kishazi shurutiwa. Sentensi hiyo inapogeuzwa hadi kiwango cha muundo geuzi, kanuni ya ugeuzi hukitanguliza kishazi sharti kikifuatwa na kishazi shurutiwa. Wakati wa ugeuzi huo, kiunganishi kiambatishi kisicho cha lazima hutokea na kukitegemeza kishazi sharti kwa kishazi shurutiwa.

Sura ya tatu inashughulikia fasili ya sentensi sharti ya Ekegusii na ufafanuzi wa viambajengo vyake. Viambajengo hivi ni pamoja na kishazi sharti, kishazi shurutiwa, vitambulishi sharti na viunganishi viambatishi. Imebainika kuwa sentensi sharti ya Ekegusii huundwa kwa kishazi sharti na kishazi shurutiwa. Vitambulishi sharti katika lugha ya Ekegusii ni pamoja na 'onye, -ise, -are, k- na ebe'. Kuna kiunganishi kiambatishi kitumiwacho ambacho si cha lazima kinachotumiwa kukiunganisha kishazi sharti na kishazi shurutiwa. Kiunganishi hiki ni 'rirorio' ambacho hudhihirika katika kiwango cha muundo geuzi pekee. Mengine yaliyoshughulikiwa katika sura hii ni

muundo wa sentensi sharti ya Ekegusii na ugeuzi unaojitokeza katika kuigeuza sentensi sharti kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo geuzi. Uchunguzi umepata kuwa sentensi sharti ya Ekegusii ikiwa katika kiwango cha muundo msingi huwa na kishazi shurutiwa kikitangulia mwanzoni mwa sentensi kikifuatwa na kishazi shurutiwa. Kishazi sharti hutegemezwa kwa kishazi shurutiwa kwa matumizi ya kitambulishi sharti kinachotekeleza pia jukumu la kutambulisha sharti. Sentensi sharti hugeuzwa kutoka kiwango cha muundo msingi hadi muundo geuzi kutokana na ugeuzi unaokitanguliza kishazi sharti kikifuatwa na kishazi shurutiwa. Ugeuzi huo husababisha kutokea kwa kiunganishi kiambatishi 'rirorio' kisicho cha lazima na kinachoviunganisha vishazi husika kwa kukitegemeza kishazi sharti kwa kishazi shurutiwa.

Katika sura ya nne, ulinganishi wa vipengele mbali mbali vinavyohusiana na sintaksia ya sentensi sharti ya Kiswahili sanifu na Ekegusii umefanywa. Kumeshughulikiwa uainishaji wa sentensi sharti ya Kiswahili na Ekegusii, kufanana na kutofautiana kwa kishazi sharti cha Kiswahili na cha Ekegusii, kufanana na kutofautiana kwa miundo ya sentensi sharti ya Kiswahili na Ekegusii na ulinganishi wa michakato ya ugeuzi inayogeuza sentensi sharti kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo geuzi.

Sura ya tano inatoa mahitimisho ya kijumla ya tasnifu hii. Inaanganzia masuala muhimu yaliyoshughulikiwa na mahitimisho yao katika kila sura ya tasnifu hii na kisha kutoa mapendekezo kulingana na maoni ya mtafiti.

# SURA YA KWANZA

## 1.0.0 Utangulizi

Tasnifu hii inangazia ufafanuzi linganishi wa sintaksia ya sentensi sharti ya Kiswahili sanifu na Ekegusii. Uchunguzi huu umetumia msingi wa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi. Katika sura hii ya kwanza, tumeanza kwa kutoa maelezo ya kijumla kuhusu lugha ya Kiswahili Sanifu na lugha ya Ekegusii ambazo ndizo lugha tulizozishungulikia.

Tumetoa maelezo kuhusu tatizo letu la utafiti, malengo, na upeo na mipaka ambayo ilituongoza katika shughuli nzima ya uchunguzi huu. Tumeelezea madhumuni ya utafiti wetu, nadharia tete na sababu za kuchagua somo hili. Tumefanya udurusu wa maandishi yanayohusiana na utafiti na kuonyesha jinsi udurusu huo ulivyonufaisha utafiti huu. Jambo lingine tulilolishughulikia katika sura hii ni msingi wa Nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi na kufaa kwake katika uchunguzi huu.

Hatimaye katika sura hii tumezibainisha mbinu za utafiti tulizozitumia kufanikisha utafiti huu. Kimsingi tumeshughulikia ulinganishi kisintaksia wa sentensi sharti ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii.

## 1.1.1 LUGHA YA KISWAHILI

Lugha ya Kiswahili ni lugha ya kibantu ambayo inazungumzwa katika maeneo mengi barani Afrika. Matumizi makubwa ya lugha hii yameshuhudiwa katika nchi za Afrika ya Mashariki na za Afrika ya Kati.

Guthrie (1948) aliiainisha lugha ya Kiswahili katika kundi kubwa la lugha za Kibantu. Aliiweka lugha hii katika ukanda wa G kundi la 40 na lugha ya 2. Kwa hivyo nambari ya Kiswahili ni G42.

Whiteley (1969) na Myachina (1981) wanaeleza kuwa Kiswahili ni neno linalotumika kurejelea zaidi ya lahaja kumi na nane zenye asili na chimbuko moja. Mojawapo ya lahaja hizi ni Kiunguja. Lahaja hii ndiyo ilisanifishwa na kutambuliwa kama lahaja sanifu ya Kiswahili.

Kwa hivi sasa, lugha ya Kisawhili imepatiwa majukumu mbali mbali kimatumizi katika mataifa kadhaa. Ni lugha ya kimataifa inayotumiwa na mashirika ya utangazaji ya nchi kadhaa kama vile Uingereza, Ujerumani, nchi za Kongo, Kenya Tanzania na nyinginezo. Nchini Kenya, lugha hii imetwikwa jukumu la kuwa lugha ya Kitaifa mbali na kuwa lugha rasmi. Kiswahili Sanifu ni lugha inayofunzwa kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu.

### 1.1.2 LUGHA YA EKEGUSII

Lugha ya Ekegusii ni mojawapo ya lugha za Kibantu inayozungumzwa magharibi mwa Kenya. Kiasili wazawa watumizi lugha hii wanaitwa Abagusii (Wakisii). Abagusii ni Wabantu ambao kiasilia wanaishi katika jimbo la Kisii na la Nyamira. Wabantu wengine wanaopatikana magharibi mwa Kenya ni Abaluhyia, Abakuria na Abasuba. Kijiografia Abagusii wanapakana na wazungumzaji wa lugha za Kinailoti ambao ni Wakipsigis, Wajaluo na Wamaasai.

Guthrie (1971), aliweza kuziainisha lugha za Kibantu katika makundi mbali mbali ikiwemo lugha ya Ekegusii. Aliiweka lugha ya Ekegusii katika ukanda wa E, kundi la 40, lugha ya 2. Hivyo nambari ya lugha ya Ekegusii ni E 42. Lugha hii inakaribiana na lugha ya Kimaragoli E41 na ile ya Kikuria E43.

Bosire (1993) anaeleza kuwa lugha ya Ekegusii ina lahaja mbili; lahaja ya Rogoro na lahaja ya Maate. Lahaja ya Rogoro ndiyo tumeitumia katika uchunguzi wetu. Hii ni kwa kuwa muda tuliokuwa nao haungeturuhusu kuzishughulikia lahaja zote mbili kwa wakati mmoja. Hata hivyo tungependa kudokeza kuwa lahaja ya Rogoro ina matumizi mapana kimaeneo ikilinganishwa na lahaja ya Maate. Aidha mawasiliano rasmi katika lugha ya Ekegusii hufanywa kwa kutumia lahaja ya Rogoro.

### 1.2.0 TATIZO LA UTAFITI

Chunguzi nyingi zimewahi kufanywa kuhusu lugha ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii kwa kutumia nadharia mbali mbali ikiwemo nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi. Aidha lugha hizi mbili zimewahi kufanyiwa tafiti nyingi za kiulinganishi katika viwango mbali mbali. Licha ya tafiti hizo zote, hakuna uchunguzi linganishi wa kisintaksia uliowahi kufanyiwa sentensi sharti ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii kwa msingi wa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi. Hii ilimaanisha kuwa kulikuwa na habari kuhusu lugha hizi mbili ambayo haikuwa imewekwa wazi na ambayo ilistahili kushughulikiwa kiisimu ili kufumbuliwa. Ni katika upungufu huo wa kiusomi tuliamua kushughulikia sintaksia ya sentensi zenye vishazi sharti zinazopatikana katika Kiswahili Sanifu na Ekegusii, kwa msingi wa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi. Utafiti wetu umezingatia ulinganishi wa sentensi zenye vishazi sharti katika lugha hizi mbili.

Tumeelezea miundo ya vishazi sharti na vipashio vya masharti vitumiwavyo katika lugha hizi mbili. Tumechunguza kufanana na kutofautiana kwa miundo ya vishazi hivyo na vile vile kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya masharti katika lugha hizi.

Mageuzi yanayotokana na ugeuzi katika sentensi zenye vishazi sharti katika lugha hizi ni jambo lingine ambalo tumelishughulikia. Tumeyachunguza na kuyafafanua mageuzi hayo na kuelezea kutofautiana na kufanana kunaojitokeza.

## 1.3.0 SABABU ZA KUCHAGUA SOMO

Uchunguzi huu utakuwa umeendeleza utafiti wa isimu linganishi na kwa hivyo utakuwa mchango mkubwa kwa sarufi bia.

Kutokana na udadisi wetu, na kadri tunavyofahamu, hakuna uchunguzi linganishi wa sintaksia ya sentensi sharti ya Kiswahili sanifu na Ekegusii uliowahi kutekelezwa kwa kutumia nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi. Kwa hivyo kumekuwa na pengo la kiusomi lililostahili kujazwa kupitia kwa uchunguzi ambao tumeufanya.

Kazi hii itakuwa mchango wetu katika uchambuzi wa sintaksia katika lugha ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii. Matarajio yetu ni kuwa kazi ambayo tumeishughulikia itawafaa wanafunzi na wasomi wote wa isimu kwa ujumla, hasa wale watakaoshughulikia lugha za Kibantu.

## 1.4.0 MADHUMUNI YA UTAFITI

Tumedhamiria kuchunguza sintaksia ya sentensi zenye vishazi sharti zilizopo kwenye Kiswahili Sanifu na Ekegusii kwa kuzingatia;

1. Miundo ya sentensi sharti katika lugha ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii kwa mujibu wa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi.
2. Vipashio vya masharti vitumiwavyo katika lugha ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii.
3. Ugeuzi unaojitokeza katika sentensi zenye vishazi sharti katika lugha ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii kwa mujibu wa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi.
4. Ulinganishi wa miundo ya sentensi, vipashio vya masharti na ugeuzi unaojitokeza baina ya sentensi sharti ya Kiswahili Sanifu na ya Ekegusii kwa mujibu wa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi.

## 1.5.0 NADHARIA TETE

Utafiti wetu umetekelezwa katika misingi ya nadharia tete zifuatazo;

1. Miundo mingi ya sentensi zenye vishazi sharti katika Kiswahili Sanifu na Ekegusii inafanana kwa mujibu wa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi.
2. Vipashio vya masharti katika lugha ya Kiswahili Sanifu ni vya aina nyingi kuliko vile vya lugha ya Ekegusii.
3. Kanuni nyingi za ugeuzi zinazosababisha mageuzi katika sentensi zenye vishazi sharti katika Kiswahili Sanifu na Ekegusii zinafanana kufuatana na nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi.

4. Sentensi sharti ya Kiswahili Sanifu na ya Ekegusii zinalingana kwa mujibu wa muundo wa sentensi, vipashio vya masharti na kanuni za ugeuzi kufuatana na nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi.

## 1.6.0 UPEO NA MIPAKA

Tulivyodokezea katika tatizo la utafiti ni kuwa tunashughulika na ulinganishi wa sintaksia ya sentensi sharti ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii kwa msingi wa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi.

Tunafahamu kuwa lugha ya Ekegusii ina lahaja mbili; lahaja ya Rogoro na lahaja ya Maate. Katika uchunguzi huu tumejishughulisha na lahaja ya Rogoro ambayo hutumiwa katika maandishi rasmi na mashirika ya utangazaji nchini Kenya yanayotangaza kwa lugha ya Ekegusii. Lahaja ya Rogoro inatofautiana na ya Maate kwa kiwango kidogo sana. Hivyo basi kazi hii itakuwa wakilishi ya lahaja zote mbili na matokeo yake yanatarajiwa kusaidia kuelewa lahaja hizi mbili za Ekegusii.

Kwa upande wa lugha ya Kiswahili, tumetumia Kiswahili Sanifu na kutoshughulika na lahaja zingine za Kiswahili. Ni matarajio yetu kuwa matokeo na mahitimisho ya uchunguzi huu yatasaidia kuelewa sintaksia ya sentensi sharti ya lugha ya Kiswahili.

Uchunguzi wetu utaendelezwa katika msingi wa Nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi. Hivyo basi tutahitaji hasa Kitengo Msingi na kitengo cha ugeuza maumbo vya nadharia hii. Nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi inadhamiriwa kutoa ufafanuzi wa kiisimu katika viwango vyote vya lugha. Hii ni pamoja na tawi la mofofonolojia, tawi la sintaksia na  lile la semantiki. Katika utafiti huu, tumeshughulikia tawi la sintaksia na

kutojishughulisha na matawi hayo mengine. Hata hivyo, ilipobidi tumeweza kuyataja matawi hayo katika uchunguzi huu pale imehitajika. Lengo letu kuu ni vipashio vya masharti, miundo ya sentensi sharti ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii, na jinsi ugeuza maumbo unavyovipanga viambajengo vyake katika lugha hizi mbili.

## 1.7.0 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Kuna kazi nyingi kuhusu lugha hizi mbili ambazo zimeshughulikiwa na wataalamu mbalimbali na ambazo zimekuwa za manufaa makubwa katika uchunguzi wetu.

Guthrie (1948), aliweza kushughulikia lugha za Kibantu kwa ujumla. Aliweza kutumia mbinu za kisayansi kuziainisha lugha za Kibantu. Kazi ya Guthrie imetuwezesha kutambua makundi ya lugha hizi yaani Kiswahili sanifu na Ekegusii ili kutambua lugha zilizokaribiana nazo ili kuweza kuzitambua na kusoma kazi zingine za utafiti kuzihusu lugha hizi.

Gesare (1992), alishughulikia Mofolojia ya Lugha ya Ekegusii. Ametumia nadharia ya Umiundo kuafikia malengo ya kazi yake. Ingawa kazi yake ilikuwa ya Kimofolojia huku na sisi tukishughulikia kitengo cha sintaksia, kuna vipengee kadhaa kama vile toni katika lugha ya Ekegusii na uainishaji wa nomino za ngeli, ambavyo tumevirejelea katika kazi yake ikikumbukwa kuwa kitengo cha mofolojia na sintaksia vinaingiliana.

Mayaka (2000), alishughulikia sentensi sahili, sentensi ambatani na sentensi changamano katika lugha ya Ekegusii. Kazi hii imekuwa ya manufaa kwetu kwani sentensi sharti ambayo tumeishughulikia ni aina mojawapo ya sentensi changamano. Ufafanuzi kuhusu

sifa za vishazi vinavyoiunda sentensi changamano ya Ekegusii umechangia kuifafanua sentensi sharti ya Ekegusii.

Polome (1967), ameshughulikia lugha ya Kiswahili katika vitengo mbali mbali. Katika kazi hii, kumeshughulikiwa miundo ya sentensi za Kiswahili Sanifu. Tumekuwa tukiirejelea kazi hii ili kupata elimu pana kuhusu miundo ya sentensi za Kiswahili Sanifu, hasa sentensi changamano.

Maw (1969), alichunguza uhusiano wa ndani wa viambajengo katika sentensi za Kiswahili. Aliweza kushughulikia muundo wa sentensi, kishazi na kategoria za makundi. Aliweza kugusia sentensi sharti na vishazi vyake. Hivi ni vipengee vinavyohusiana na uchunguzi wetu. Kazi hii imekuwa ya manufaa kwetu kutokana na maoni tuliyoyakopa hasa kuhusu muundo wa sentensi, na vishazi kama vijenzi vya sentensi ya Kiswahili.

Myachina (1981), naye alishughulikia lugha ya Kiswahili kwa upana ambapo sarufi ya Kiswahili Sanifu imeshughulikiwa. Uchunguzi wetu utanufaika kwa kuirejelea kazi hii ili kupata uelewa zaidi wa sintaksia ya Kiswahili Sanifu.

Mgullu (1990), amezifafanua sentensi sahili, ambatano na changamano katika Kiswahili sanifu kwa kutumia nadharia ya Sarufi Sawazishi. Ingawa alitumia nadharia iliyo tofauti na yetu, kazi hii imekuwa muhimu kwetu hasa sehemu inayochanganua sentensi ambatano. Ni katika sehemu hii ambapo ametoa maelezo kwa ufupi kuhusu sentensi sharti ya Kiswahili. Mgullu amevitambua vitambulishi sharti vitano katika lugha ya Kiswahili. Tutakavyoona baadaye katika kazi hii, ni kuwa lugha ya Kiswahili ina vitambulishi sharti takriban tisa na wala si vitano. Tumezama katika kuchanganua kwa kutoa maelezo ya kina kuhusu sentensi sharti tukijikita katika ugeuzi maumbo kwa

msingi wa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi. Hili ni jambo ambalo halijawahi kushughulikiwa katika kazi yoyote ile.

Omusula (1990), amelinganisha mifanyiko ya Kimofolojia baina ya mnyambuliko wa kitenzi cha Kiswahili na cha Kikabarasi. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa kuwa inashughulika na isimu linganishi sawa na uchunguzi tunaodhamiria kuufanya. Vile vile lugha ya Kikabarasi ni lugha ya Kibantu ilivyo lugha ya Ekegusii zote zikiwa zinalinganishwa na lugha ya Kiswahili ambayo pia ni lugha ya Kibantu.

Mgullu (1999), ameelezea dhana ya mofu ambapo ametubainishia aina za mofu. Maelezo yake yametufaa kubainisha maumbo ya vitambulishi sharti vya Kiswahili Sanifu na vya Ekegusii. Kuna vishazi sharti vilivyo na umbo la mofu huru na vile vilivyo na umbo la mofu funge katika lugha hizi mbili.

Gicheru (1999), amelinganisha Kikundi Nomino cha Kiswahili Sanifu na cha Kikikuyu cha Kabete. Kazi hii imetupa mwanga katika kupata mwelekeo wa jinsi ya kushughulikia kazi za ulinganishi na kwa kuwa lugha zote husika ni za Kibantu.

Jerono (2003), ameshughulikia Kishazi huru cha Kiswahili Sanifu akitumia nadharia ya X-bar. Uchunguzi huu una mahitimisho ambayo yatahusiana na uchunguzi tutakaoufanya. Hii ni kwa kuwa Kishazi huru ni kiambajengo cha lazima cha sentensi sharti ambayo tumeichunguza.

Oichoe (2005), amelinganisha Kirai Tenzi cha Kiswahili Sanifu na Ekegusii Kimofosintaksia. Aliweza kutumia mtazamo wa Uminimalisti katika kufanikisha uchunguzi wake. Kazi hii ni muhimu kwani lugha hizo mbili alizozishughulikia ndizo

tumezishughulikia katika uchunguzi wetu. Ingawa alitumia nadharia tofauti na yetu ni matumaini yetu kuwa mahitimisho yaliyopatikana katika uchunguzi wake yamechangia pakubwa katika kutekeleza uchunguzi wetu.

Obuchi na Mukhwana (2010), wameelezea viambishi katika vitenzi ambapo wametoa maelezo kwa ufupi kuhusu baadhi ya vitambulishi sharti vya Kiswahili ambavyo ni 'nga, ngali, nge, ngeli, ki, ikiwa, na iwapo'. Maelezo kuhusu maumbo haya yamekuwa muhimu kwa kutupa mwongozo wa matumizi sahihi hasa maumbo hayo yanapotumiwa katika muktadha wa sentensi sharti. Aidha ufafanuzi wao kuhusu sentensi changamano umetufaa sana kuuelewa muundo wa sentensi sharti. Hili linatokana na ukweli kuwa sentensi sharti ina muundo wa sentensi changamano. Wanatueleza kuwa sentensi changamano huundwa na kishazi kikuu kimoja, na kishazi tegemezi kimoja au zaidi. Hii ni sifa inayopatikana katika sentensi sharti.

Chomsky (1957), amewasilisha mtazamo wa Sintaksia unaotambuliwa kama Sarufi Geuza Maumbo Zalishi. Kazi hii ndiyo ilikuwa chanzo cha, na asili ya sarufi zalishi. Katika kazi hiyo, Chomsky alikusudia kukuza fafanuzi mwafaka za hali ya sintaksia ya lugha mbalimbali,yaani jinsi lugha mahususi zinavyounganisha maneno kuunda sentensi. Vile vile kazi hiyo ilidhamiria kukuza nadharia ya kijumla ya sintaksia inayobainisha ni mambo yapi ya kijumla yanayopatikana katika lugha mbali mbali na jinsi gani masuala hayo yanavyotofautiana katika uwanja huu wa sintaksia. Hii ndiyo kwa kawaida inaitwa nadharia ya Sarufi bia. Kazi hii imekuwa muhimu kwetu kwani ufafanuzi wake umetufahamisha kwa undani msingi na asili ya Sarufi Zalishi. Huu ndio msingi wa nadharia ambayo tumeitumia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi. Ni mojawapo ya nadharia za mtazamo wa sarufi zalishi.

Chomsky (1965), alishughulikia ufafanuzi wa masuala mengi yanayohusiana na sarufi. Miongoni mwa masuala hayo yanawiana na uchunguzi wetu na kwa hivyo tumekuwa tukiirejerea kazi hiyo. Tumenufaika kwa kupata ufafanuzi na maelezo kuhusu kitengo msingi, sheria za kitengo msingi, muundo ndani na ugeuza maumbo wa sarufi. Aidha kazi hii imetupa mwanga mpana katika kuelewa nadharia ya Sarufi Geuza Maumbo Zalishi kwa ujumla.

Jacobsen (1977), ameelezea historia na maendeleo ya nadharia ya Sarufi Geuza Maumbo Zalishi. Ametoa ufafanuzi wa nadharia hiyo katika vipindi mbalimbali ambavyo ni,

a) Kipindi kabla ya mwaka wa 1965. Hapa anaelezea kuasisiwa kwa nadharia hii katika kazi ya Chomsky (1957), Syntactic Structures. Katika mwaka wa 1963, Katz na Fodor walichapisha 'The Structure of a Semantic Theory' ambayo iliweza kutambua kitengo cha semantiki kuwa kigezo muhimu katika ufafanuzi wa lugha.

b) Kipindi cha mwaka wa 1965, ambapo nadharia ya Sarufi Sawazishi iliweza kukuzwa.

c) Kipindi baada ya mwaka wa 1965 ambapo nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi iliweza kubuniwa kutokana na marekebisho yaliyofanyiwa nadharia ya Sarufi Sawazishi.

Kazi hii ya Jacobsen imekuwa muhimu kwetu katika kupata ufafanuzi na uelewa wa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi ambayo uchunguzi wetu umejikita kwayo.

## 1.8.0 MSINGI WA NADHARIA

Msingi wa uchuguzi wetu umo katika nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi ya Chomsky. Nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi ilitokana na mpango mrefu wa maendeleo katika Sarufi Geuza Maumbo Zalishi. Asili ya maendeleo haya katika nadharia hiyo ni katika kazi ya Chomsky ya mwaka 1957 iliyoitwa Syntactic Structures. Sarufi hiyo ilifanyiwa mabadiliko mwaka wa 1965 wakati Chomsky alipotokea na kazi yenye ufafanuzi wa kina zaidi iliyoitwa 'Aspects of the Theory of Syntax'. Kazi hii ilikuwa na kielelezo cha nadharia ya Sarufi Geuza Maumbo kilichokuwa na kitengo cha sintaksia, fonolojia na semantiki. Kitengo cha semantiki ndicho kilichoongezwa na hivyo kuwa kipengele kilichotofautisha kielelezo hiki kutoka kile cha awali. Kazi hii ya mwaka wa 1965 ndiyo inafahamika kama Sarufi Sawazishi.

Kazi hiyo ndiyo iligundua kuwa kulikuwa na umilisi wa kiisimu aliokuwa nao mzawa wa lugha fulani ambao unaweza kuelezewa na kufafanuliwa tu kwa kutumia nadharia ya kisemantiki. Kulingana na Katz na Fodor (1964), ujuzi huu wa kiisimu wa mzawa wa lugha ni pamoja na ule unaomwezesha kutambua makosa ya kisemantiki, kutambua utata na kutambua usemi fasili.

Kwa hivyo kitengo cha semantiki kilikuwa kitengo muhimu sana. Hata hivyo Chomsky hakuweza kukikuza kitengo hicho. Alichofanya ni kukijumuisha kama mojawapo ya vitengo vya sarufi katika hatua hii ya maendeleo ya nadharia hiyo.

Nadhara ya Sarufi ndiyo kwa kawaida inajulikana kama Nadharia ya Sarufi Sawazishi ya Sarufi Geuzi Maumbo. Kulingana na nadharia Sarufi Sawazishi, kila sentensi ina

viwango viwili vya miundo ya kisintaksia ambavyo vinaweza kutambulika. Viwango hivyo ni:

- **i.** Muundo ndani
- **ii.** Muundo nje

Muundo ndani huwa na vielelezo tungo ambavyo huzalishwa na sheria za sehemu msingi. Vielelezo tungo hivyo hubadilishwa kuwa muundo nje kwa kutekelezwa kwa kundi la sheria za ugeuza maumbo zilizo na mpangilio maalum.

Grinder (1973:150) anaeleza kuwa Nadharia ya Sarufi Sawazishi ndiyo ilikuwa ya kwanza kuwasilisha kielelezo kilichokamilika cha ugeuza maumbo kilichotumiwa kufafanunulia lugha asilia. Nadharia hii ilileta mapinduzi makubwa katika historia ya Nadharia ya Ugeuza Maumbo. Hata hivyo kulitokea maendeleo mengine mengi baada ya kuasisiwa kwa nadharia ya sarufi. Wanaisimu waliibuka na mawazo mengi. Miongoni mwa wanaisimu hawa ni Katz na Fodor walioibua wazo la Semantiki Zalishi. Hii ilikuwa Nadharia ya semantiki.

Uchunguzi uliofanywa na Katz na Fodor pamoja na ule wa wanaisimu wengine wakati wa kipindi hiki uligundua mambo mengi ambayo athari yake ilikuwa ni kupinga baadhi ya vipengee hata vile vya kimsingi kuhusu nadharia ya Sarufi Sawazishi. Baadhi ya madai ya nadharia hii yaliishia kufutiliwa mbali na wanaisimu akiwemo Chomsky mwenyewe. Baadhi ya madai yaliyokataliwa ni pamoja na yale yaliyosema kuwa:

**(i)** Ugeuza maumbo ni wa kuhifadhi maana, na kuwa maana yote inapatikana katika muundo ndani, na kuwa hakuna maana yoyote inayoweza kupatikana katika muundo nje.

**(ii)** Sarufi geuza maumbo iwe ni ya kuhifadhi miundo bila kuibadili. Wazo hili lilikuwa limependekezwa na Katz na Postal (1963).

Madai haya kuhusu hali ya ugeuza maumbo yalizua matatizo katika nyanja kama vile ugeuza maumbo ubwete au ukanushi unapohusika katika usogezi wa viarifu mantiki (mfano vielezi vya kiasi kama vile –chache, -ingi na ukanushi). Ilitambuliwa kuwa wakati nafasi ya viarifu mantiki inageuzwa kuimarishwa hadi viwango vya juu vya sentensi kulikuwa na kubadilika kwa maana. Kwa sababu hii, sio mageuzi yote yalihifadhi maana. Misimamo kama hii katika nadharia Sarufi Sawazishi haikuwa na budi kubadilishwa. Hii ilipelekea kurekebishwa kwa nadharia ya Sarufi Sawazishi na kuzaliwa kwa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi ili kutoa suluhisho kwa matatizo kama hayo na mengine.

Chomsky (1972) na wanaisimu wengine wa kipindi hiki wanaipendekeza nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi iliyopanua mipaka ya sheria za kiufasiri au kiufafanuzi ili kujumuisha miundo nje. Nadharia hii inasisitiza kuwa si maana yote hutokea katika kiwango cha muundo ndani. Inaamini kuwa baadhi ya maana hutokeza katika kiwango cha muundo nje. Kwa mfano, nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi ina sheria za ufasiri wa kisemantiki zinazoshughulika na miundo nje. Kutokana na jambo hili, maana kisemantiki inapatikana kutokana na sheria za kiufasiri zinazotekelezwa katika kiwango cha muundo nje.

Chomsky na wenzake katika kuibua nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi, walikuwa wanalenga kutokea na mfumo wa kanuni uliojulikana kama sarufi bia. Walikuwa wakichunguza sarufi mahususi (kwa mfano sarufi ya lugha kama vile Kiswahili) wakiwa na lengo la kutambua sifa za kijumla za lugha kutoka sarufi za lugha hizo mahususi. Radford (1981) anaelezea jinsi waasisi hao wa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi walivyoelezea sarufi ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi. Sarufi hii ina viwango vitatu vya muundo katika sintaksia. Viwango hivyo ni;

**i.** Muundo ndani

**ii.** Muundo nje

**iii.** Umbo fonetiki na umbo mantiki.

Muundo ndani ndio wasilisho la kisintaksia la kipengee fulani cha kisarufi. Muundo nje wa sentensi ndicho kiwango cha mwisho katika uwakilishi wa kisintaksia wa sentensi. Muundo nje ndio chanzo cha kitengo fonolojia cha sarufi. Umbo fonetiki na umbo mantiki ni viwango vilivyo na kanuni ambazo hufanya kazi kwa wakati mmoja ili kutoa uwasilishi wa kifonetiki (sauti) na uwasilishi wa kisemantiki (maana).

Muundo ndani unazalishwa na kanuni za kitengo msingi. Kitengo Msingi hujumuisha:

**i.** Kanuni Miundo Virai (zilizo hasa za aina ya x-bar)

**ii.** Msamiati (vidahizo, sheria za uundaji wa maneno, sheria za upangaji/uundaji upya n.k)

**iii.** Sheria za uingizaji wa leksimu.

Muundo nje unazaliwa kutoka kwa muundo ndani kutokana na kanuni za kitengo cha Ugeuza Maumbo. Kitengo hiki kina mageuzi maumbo kama vile ugeuza maumbo swali, uhamishaji wa vipashio, uchopekaji, udondoshaji na mageuzi mengine ambayo yaweza kutajwa kama usogezi alfa. Kitengo cha ugeuza maumbo vile vile kina masharti ambayo kwayo ugeuza maumbo hutekelezwa. Masharti haya ni kama vile: masharti ya kuhifadhi maumbo, masharti ya kifundo tupu, masharti ya unakili na mengine. Sarufi hufanya kazi kwa jinsi inavyoelezwa hapa.

Sehemu msingi ya kitengo cha sintaksia huwa na mfumo wa kanuni muundo virai zilizo za aina ya x-bar. Katika muktadha huu, x inaweza kuwakilisha kitenzi, nomino, kiwakilishi au kielezi. Haya ndiyo maneno makuu. Maneno makuu huchukua vijalizo vya vibainishi. Hii inamaanisha kuwa chochote kilicho upande wa kulia wa x ni kijalizo na chochote kilicho upande wa kushoto ni kibainishi. Mpangilio huu hutekelezeka katika leksikoni (msamiati) iliyo katika sehemu msingi.


Leksikoni huwa na mkusanyiko wa maneno yasiyo na mpangilio wowote. Maneno haya huwa hayamo katika muktadha wowote ule. Katika sehemu msingi ndiko kunakuwa na vijalizo na vibainishi na ambapo vinateuliwa na maneno makuu. Chomsky (1965) anaeleza kuwa kanuni za sehemu msingi huzalisha seti iliyofinywa ya mikufu msingi. Mikufu hii ina jukumu la ufafanuzi wa kimuundo unaoitwa kielelezo tungo msingi. Ufafanuzi huu wa kimuundo ndio unazalisha muundo ndani. Hivyo kielelezo tungo msingi huzalisha umbo ndani la sentensi. Huu muundo ndani huelekea kwa kitengo geuza maumbo.

Kitengo geuza maumbo hutekeleza mageuzi kama vile kudondoa au kuondoa, kuchopeka, ugeuza maswali, usogezi au uhamishaji wa vipashio na kadhalika. Kitengo geuza maumbo kina aina kadhaa ya vikwazo vinavyoathiri mageuzi. Mfano wa vikwazo hivi ni lile sharti la ukaribu. Radford (1981) anaeleza kuwa sharti la ukaribu linadai kuwa hakuna kiambajengo kinaweza kuhamishwa zaidi ya kifundo funge kimoja katika utekelezaji wa kanuni yoyote.

Kutoka kwa kitengo geuza maumbo kunazaliwa miundo nje. Hii miundo nje huwa ni maumbo ya kidhahania kwa kuwa miundo hiyo huwa na kategoria tupu kama vile PRO (pronomino dhahania ambayo haijitokezi katika muundo nje, ambayo ina urejereaji wa kidhahania au urejelewa wake unaweza kubainishwa na kirai nomino katika kishazi kilicho karibu nayo). Kategoria tupu inayopatikana katika muundo nje ni nyayo. Hizi ni nyayo zinazoachwa nyuma kutokana na usogezi wa kiambajengo fulani. Hatimaye miundo nje inaelekezwa kwa vijitengo vingine kama vile kijitengo fonolojia, mantiki, nadharia ya uhusika na nadharia ya masharti. Kila kijitengo hutekeleza jukumu lake na kuchangia kwa ufasiri wa kisemantiki wa muundo wa kisarufi.

Ingawa kuna vitengo vingi vya sarufi ambavyo vimewasilishwa katika Upanuzi wa Sarufi Sawazishi, upeo wa uchunguzi wetu utajumuisha tu kitengo msingi na kitengo geuza maumbo na kutoshughulika na umbo fonetiki na umbo mantiki.

Kifuatacho nikielelezo cha nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi.




(Jacobsen 1977:95)

Sheria za umbo kifonetiki ambazo hupatikana katika kitengo cha kifonolojia, na zile za kimantiki ambazo zinapatikana katika kitengo cha kisemantiki ziliendelezwa katika nadharia ya Umilikifu na Masharti. Nadharia hii ilizaliwa kutokana na marekebisho yaliyofanyiwa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi. Miongoni mwa sheria za Umilikifu na Masharti zinazojumuishwa katika umbo la kifonetiki ni sheria za udondoshaji, sheria za kifonetiki na sheria za mtindo. Katika umbo la kisemantiki (mantiki), kunatambuliwa sheria za kiufasiri kama vile za kuelewa maana, sheria za anaphora (mrejeosabiki), na sheria za idadi na kanuni funge.

Nadharia ya Umilikifu na Masharti ni nadharia iliyo na mpangilio wa vijinadharia kadhaa zinazofafanua sarufi ya lugha. Nadharia hii ina vijinadharia vinavyoingiliana na vilivyo na malengo ya kuieleza lugha. Baadhi ya nadharia zinazopatikana chini ya mwavuli wa nadharia ya Umilikifu na Masharti ni pamoja na nadharia ya x-bar, nadharia funge, nadharia ya thita, nadharia ya uhusika na nadharia ya masharti. Nadharia hizo zilizoorodheshwa hapo juu na vijinadharia vingine ambavyo havikuorodheshwa hapa, kwa pamoja huunda nadharia ya Umilikifu na Masharti.

## 1.9.0 MBINU ZA UTAFITI

Katika uchunguzi wetu kuna sehemu mbili muhimu za uchanganuzi wa kisintaksia ambazo tumezishughulikia. Kwanza tumefafanua muundo viambajengo wa sentensi sharti ya Kiswahili sanifu na Ekegusii kwa kutumia sheria za kitengo msingi kwa mujibu wa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi.

Pili, tumechanganua maenezi/ usambazaji wa viambajengo vya sentensi sharti na kuelezea mabadiliko ya mpangilio wa viambajengo kutokana na ugeuza maumbo wa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi.

Ili kufikia ufafanuzi kama huo, tulihitaji data tuliyoichanganua na elimu ya kina kuihusu nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi. Kwa hivyo tumefanya utafiti maktabani ili kupata habari kuhusu madai na kanuni za nadharia hiyo. Utafiti huu maktabani umehusu kazi zinazofafanua msingi wa nadharia ambayo inahusika na uchunguzi wetu. Pia utafiti huu maktabani umehusisha kazi mahususi ambazo zinahusika na uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili Sanifu na zile za Ekegusii.

Mtafiti anayo tajriba ya kina kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili Sanifu kutokana na mafunzo ambayo amepokea katika taasisi mbalimbali zinazoshughulika na mafunzo ya lugha hii. Hivyo mtafiti ana ujuzi ulio karibu sawa na mzawa mtumizi lugha. Ametumia ujuzi huo ili kutekeleza uchanganuzi kuhusu masuala yote yaliyowezesha kufanikishwa kwa utafiti huu. Aidha tumetumia machapisho ya Kiswahili Sanifu ili kupata data ya kuchanganuliwa.

Kwa kuwa mtafiti ni mzawa wa lugha ya Ekegusii, ametumia tajriba yake katika lugha hii ili kuvichambua vipengele vyote vilivyochunguzwa kuihusu lugha hii. Kutokana na umilisi alio nao kuhusu lugha hizi husika, amekuwa katika nafasi nzuri kuweza kuzichanganua kiulinganishi kwa mujibu wa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi.

# SURA YA PILI

## 2.0.0 UMBO, MAANA NA MATUMIZI YA SENTENSI SHARTI YA KISWAHILI

### Utangulizi

Sura hii inatoa utangulizi wa sentensi sharti ya Kiswahili kwa njia ya kueleza fasili yake, maelezo kwa ufupi kuhusu majukumu kisemantiki ya vishazi na vipashio vingine vinavyoijenga sentensi sharti. Tunalenga kutoa maelezo kuhusu kishazi sharti ambacho ni kiambajengo cha lazima katika sentensi sharti. Tumeeleza ni vipashio vipi vinavyokiunda kishazi sharti na ni jinsi gani vishazi tofauti vinaunganishwa ili kuunda sentensi sharti.


Katika sura hii tumechunguza muundo msingi wa sentensi sharti ya Kiswahili. Tumefanya udadisi kuhusu jinsi viambajengo vya sentensi sharti vinavyojitokeza katika kiwango cha muundo msingi. Aidha tumechunguza mchakato wa ugeuzi unaopelekea sentensi sharti kugeuzwa kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo geuzi. Tumezitambua kaida zinazoongoza ugeuzi huo kwa misingi ya nadharia tunayoitumia. Mwisho kabisa tumetoa mahitimisho kuhusu masuala muhimu yaliyoshughulikiwa katika sura hii.

### 2.1.1 FASILI YA SENTENSI SHARTI YA KISWAHILI

Sentensi sharti ya Kiswahili ni aina ya sentensi inayojumuisha vishazi viwili au zaidi vinavyowasilisha hali za mambo hivi kwamba kutokea kwa hali ya jambo moja kunaweka sharti dhidi ya kutokea hali ya jambo lingine. Hii inamaanisha kuwa hali inayoelezewa na mojawapo wa vishazi, huweka masharti dhidi ya kutokea kwa hali nyingine inayoelezewa na kishazi kile kingine. Kishazi kile kinachoelezea sharti lililowekwa dhidi ya hali fulani ndicho kinaitwa kishazi sharti. Kishazi kile kinachoelezea hali iliyowekewa sharti ndicho kishazi shurutiwa.

Hartman (1972), anaeleza kuwa kishazi sharti ni kishazi kinachowasilisha sharti kwa kawaida kwa kutumia neno ‘kama’. Platt (1985), naye anaeleza kuwa kishazi sharti ni mojawapo wa kishazi elezi kinachoanza kwa neno ‘kama’ au viunganishi vingine vilivyo na maana sawa na ‘kama’, ambapo hali fulani katika kishazi kimoja inategemea kitu fulani ambacho kinatajwa katika kishazi kingine.

Kutokana na fasili hizi, tungependa kueleza kuwa sentensi sharti ya Kiswahili huwa na vishazi viwili au zaidi. Vishazi vya lazima ni kishazi sharti na kishazi shurutiwa. Kwa mfano tukichukulia sentensi sharti $S_1$ na vishazi vyake vijenzi vikawa $S_2$ na $S_{3,}$ tunaweza kusema kuwa $S_1$ imeundwa kwa muungano wa $S_2$ na $S_3$ kama inavyoonyeshwa katika mchoro ufuatao.



Katika kielelezo cha hapo juu, $S_2$ inaweza kuwa kishazi sharti na $S_3$ ikiwa ni kishazi kilichoshurutiwa. Hii inamaanisha kuwa $S_1$ inajumuisha $S_2$ na $S_3$ hivi kwamba $S_2$ na $S_3$ zinafafanua hali mbili za matukio ambapo kutokea kwa tukio linalowakilishwa na $S_2$ huweka sharti kwa tukio ambalo ni hali inayowakilishwa na $S_3$. Mfano wa $S_1$ unaweza kuonekana katika sentensi ifuatayo.

1. Kama dereva atafika leo basi abiria watasafiri kesho.

Katika sentensi ya hapo juu, 'abiria watasafiri kesho' ni kishazi kilichoshurutishwa na kishazi kilichokitangulia. Tukio linalowakilishwa na kishazi hiki, linategemea kutimika kwa tukio linaloelezewa na kishazi kilichokitangulia yaani 'kama dereva atafika leo' ambacho ni kishazi sharti. Sentensi ya (1) inatoa maana kuwa ikitokea kuwa dereva hatafika, basi abiria hawatasafiri. Kusafiri kwa abiria kunategemea kufika kwa dereva.

Kutokana na maelezo haya, sentensi sharti ya Kiswahili inaundwa kwa muungano wa vishazi visivyopungua viwili. Kishazi kimoja ni kile kinachoeleza sharti huku kingine kikiwa ni kile kinachowekewa sharti. Hali hii inatupatia muundo wa sentensi changamano. Hivyo sentensi sharti ya Kiswahili Sanifu ina muundo wa sentensi changamano. Obuchi na Mukhwana (2010), wanaeleza kuwa sentensi changamano ni aina ya sentensi yenye kishazi tegemezi kimoja au zaidi, mbali na kuwa na kishazi huru kimoja au zaidi. Kwa kuwa sentensi sharti ni sentensi changamano, ni lazima kishazi kimoja chake kiwe kishazi tegemezi. Tungependa kufafanua kwa ufupi maana ya utegemezi ili tuweze kuelewa uhusiano unaopatikana baina ya vishazi husika.

### 2.1.2 UTEGEMEZI KATIKA SENTENSI SHARTI YA KISWAHILI

Kishazi tegemezi kinafafanuliwa kuwa ni kishazi bebwa, yaani sentensi iliyobebwa katika muundo wa sentensi nyingine. Sentensi hiyo iliyokibeba kishazi tegemezi ndani yake inaitwa kishazi jumuishi. Kwa mujibu wa nadharia ya sarufi, sentensi jumuishi huundwa kwa sentensi kuu pamoja na sentensi tegemezi. Kutokana na mawazo haya, tunasema kuwa sentensi sharti ya Kiswahili huwa na kishazi kikuu (kishazi shurutiwa), na kishazi tegemezi (kishazi kinachotoa sharti). Mawazo hayo yanaweza kuonekana katika sentensi inayofuata.

2. $[_{S_1}$ Mkulima atapanda $[_{\bar{S}}$ kama $[_{S_2}$ mvua itanyesha.$]]]$

Sentensi nzima ya hapo juu ni kishazi jumuishi. Kishazi hicho kina sentensi kuu $s_1$ na kishazi tegemezi $s_2$. Sentensi jumuishi hapo juu inaweza kurejelewa kama kishazi kikuu kwa kuwa haijategemezwa kwa kishazi kingine.

### 2.1.3 KISHAZI SHARTI CHA KISWAHILI

Kishazi sharti hupatikana katika kategoria ya kielezi katika sentensi. Ni kishazi chenye uamilifu wa kielezi katika muundo wa sentensi. Kishazi hiki hutumika kama kipashio kielezi kinachofafanua kishazi kikuu kwa kutaja sharti linalotawala tukio linaloelezewa na kishazi kikuu.Vielezi huainishwa katika makundi madogo madogo kutegemea ni nini vinavyotumiwa kufafanua. Kuna vielezi vinavyofafanua sehemu ya kishazi kama vile

kitenzi, kivumishi au kielezi kingine. Aidha kuna miundo ya vielezi ambavyo hufafanua kishazi kizima. Hivi huwa ni vishazi vinavyovifafanua vishazi vingine kwa kutekeleza majukumu miongoni mwao yakiwa yale ya kuelezea ukweli, hali au namna, kutoa mapendekezo yaliyo kinyume na kile kinachotarajiwa kutokana na ukweli wa hali ya mambo, na kutoa masharti ambayo kwayo matukio fulani hutekelezwa. Kishazi elezi kilicho na uamilifu wa kutoa sharti ndicho tunachoshughulika nacho katika uchunguzi huu.

Kishazi sharti cha Kiswahili ni kishazi elezi ambacho hutaja sharti ambalo hubainisha kutukia kwa jambo fulani. Kishazi hiki hutaja hali ambayo lazima iwepo ili jambo fulani liweze kutekelezeka. Mfano wa muundo wa sentensi inayofuata utatusaidia kuelewa wazo la kishazi elezi cha sharti.

3. (a) Kama utakiuka sheria basi utahukumiwa.

Katika sentensi ya (3a) kuna vishazi viwili (au mapendekezo mawili) ambavyo ni (3b) na (3c) inavyoonyesha hapa chini.

3. (b) Kama utakiuka sheria.

(c) Basi utahukumiwa.

Baina ya vishazi hivi viwili (3c) ndicho kishazi cha pendekezo kuu. Kinaelezea wazo kuu la sentensi (3a). Kishazi (3b) ni kishazi elezi cha sharti. Ili tukio linaloelezewa na (3c) kufanyika, ni lazima sharti linalotajwa na (3b) litimizwe kwanza. Katika mfano huu, kitendo cha kukiuka sheria lazima kifanywe kwanza ndipo kile cha kuhukumiwa kiweze kufanyika. Tumeona katika mfano wa (3a) kuwa kishazi sharti ni aina ya kiambajengo

elezi ambacho upeo wake wa ufafanuzi unajumuisha kishazi shurutiwa kizima ambapo hicho kishazi sharti kimetegemezwa. Kiunganishi tegemezi ‘kama’ ambacho hutanguliza kishazi sharti cha Kiswahili mara tu kinapoingizwa katika kishazi, huhitaji kuwa kishazi hicho kiunganishwe na kishazi kingine, yaani pendekezo kuu, ili kuifanya taarifa iwe kamilifu na sahihi.

Kishazi sharti cha Kiswahili kinaweza kutokea upande wa kulia au kushoto mwa kishazi kikuu kwa mujibu wa mpangilio wa viambajengo katika sentensi. Wakati kishazi elezi cha sharti kinapowekwa kushoto mwa kishazi kikuu katika sentensi, kinaunganishwa na kishazi kikuu kwa mujibu wa kiunganishi tegemezi ambacho ni kipashio ‘basi’. Kiunganishi tegemezi ‘basi’ si cha lazima katika hali hii. Hii ni kwa sababu alama ya uakifishi ya koma (,) inaweza kupachikwa baina ya kishazi elezi cha sharti na kishazi kikuu. Alama hii huwakilisha mpumuo katika maongezi. Hali hizi mbili zinadhihirishwa hapa chini.

4. (a) Kama utakiuka sheria basi utahukumiwa.

(b) Kama utakiuka sheria, utahukumiwa.

Wakati kishazi sharti kinapowekwa kulia mwa kishazi shurutiwa, kitangulizi cha sharti hutumiwa kuviunganisha vishazi hivi. Mfano ni kama sentensi inayofuata.

4. (c) Utahukumiwa kama utakiuka sheria.

Sentenzi (4c) inaweza kugawa katika vishazi viwili pamoja na kitangulizi cha sentensi sharti kwa mfano ‘kama’.

5. (a) Utahukumiwa.

   (b) Utakiuka sheria.

Halafu kitangulizi cha sharti ‘kama’ kinachopekwa katika (5b) ili kukibainisha kama kishazi kielezi cha sharti inavyoonyeshwa katika (5c) hapa chini;

5. (c) Kama utakiuka sheria.

Jukumu la kisemantiki la kishazi sharti (5c) ni kutaja sharti ambalo chini yake tukio linalowasilishwa na (5a), ambacho ni kishazi shurutiwa cha (4a), linaweza kutekelezwa.

## 2.2.0 KITAMBULISHI CHA KISHAZI SHARTI CHA KISWAHILI

Tumekwisha kuonyesha jinsi kishazi sharti cha Kiswahili kinavyoweza kutambuliwa. Kishazi elezi cha sharti cha Kiswahili kinaweza kutambuliwa kwa kipashio kibainishi ambacho ni ‘kama’ au vitambulishi vingine vya sharti. Tungependa basi kuchunguza na kuvitambua vipashio vingine ambavyo vinaweza kutumiwa badala ya ‘kama’ katika kutambulisha kishazi sharti cha Kiswahili.

Katika lugha ya Kiswahili Sanifu, vipashio vifuatavyo hutumiwa kama vitambulishi vya kishazi sharti. Vitambulishi hivyo ni kama vinavyoorodheshwa hapa chini.

i. kama
ii. ikiwa
iii. endapo
iv. iwapo
v. ki
vi. nga na ngali
vii. nge na ngeli

### 2.2.1 KITAMBULISHI SHARTI 'KAMA'

Kijalizo 'kama' ndicho hutumiwa sana katika kutambulisha sentensi sharti za Kiswahili. Kijalizo hiki kinaweza kutumiwa katika njeo zote yaani wakati uliopita, wakati uliopo na wakati ujao. Aidha kitambulishi hiki kinaweza kutumiwa ama kabla ya au baada ya kishazi kikuu.

6 (a) Kama unahisi njaa basi agiza chakula ule.

(b) Kama mkulima alipata miche basi aliipanda.

Sentensi (6a) imeandikwa katika njeo ya wakati uliopo. Nayo sentensi (6b) imeandikwa katika njeo ya wakati uliopita. Sentensi hizo zinaweza kuandikwa zikawa na mpangilio mwingine wa vishazi bila kubadilisha maana inavyoonyeshwa katika (7).

7 (a) Agiza chakula ule kama unahisi njaa.

(b) Mkulima aliipanda miche kama aliipata.

Sentensi ifuatayo nayo ni sentensi sharti iliyo na kitambulishi cha kishazi ‘kama’ na imeandikwa katika njeo ya wakati ujao.

8. Kama wanariadha watajiandaa kiholela basi wataukosa ushindi.

Sentensi (8) imeandikwa kwa kukitanguliza kitambulishi cha kishazi sharti, yaani ‘kama’. Sentensi hiyo inaweza kuandikwa vishazi viambajengo vyake vikibadilishana nafasi huku kitambulishi kishazi sharti kikijitokeza baina ya vishazi hivyo. Hapa kishazi sharti kinachukua sehemu ya pili ya sentensi kikiwa kimetambulishwa na ‘kama’.

9. Wanariadha wataukosa ushindi kama watajiandaa kiholela.

### 2.2.2 KITAMBULISHI SHARTI ‘IKIWA’

Kipashio ‘ikiwa’ ni kitambulishi cha kishazi sharti katika Kiswahili. Kitambulishi hiki hutumiwa kutolea masharti inavyoonyeshwa katika tungo zifuatazo.

10. (a) Ikiwa askari atafanya uhalifu basi ataadhibiwa.

(b) Ikiwa askari alifanya uhalifu basi aliadhibiwa.

Vishazi sharti katika sentensi za hapo juu vimetambuliwa kwa matumizi ya 'ikiwa'. Vishazi hivyo vimetokea kabla ya kishazi shurutiwa. Vishazi sharti vya hapo juu huweza kutokea baada ya kishazi shurutiwa inavyoonyeshwa katika sentensi zifuatazo.

11. (a) Askari ataadhibiwa ikiwa atafanya uhalifu.

(b) Askari aliadhibiwa ikiwa alifanya uhalifu.

### 2.2.3 KITAMBULISHI SHARTI 'ENDAPO'

Kitambulishi kishazi sharti 'endapo' kina matumizi sawa na kitambulishi kishazi sharti 'ikiwa na kama'. Kijalizo hiki huweza kukitambulisha kishazi sharti kinachotokea kabla au baada ya kishazi kikuu. Sentensi (12) inaonyesha matumizi mwafaka wa 'endapo' kama kitambulishi cha kishazi sharti.

12. (a) Endapo unataka kusafiri basi kwanza lipa nauli.

(b) Endapo utataka kusafiri basi kwanza utalipa nauli.

Vishazi sharti katika sentensi za hapo juu vimetambuliwa kwa matumizi ya 'endapo'. Vishazi hivyo vimetokea kabla ya kishazi shurutiwa. Vishazi sharti vya hapo juu huweza kutokea baada ya kishazi shurutiwa inavyoonyeshwa katika sentensi zifuatazo.

13. (a) Kwanza lipa nauli endapo unataka kusafiri.

(b) Kwanza utalipa nauli endapo utataka kusafiri.

### 2.2.4 KITAMBULISHI SHARTI 'IWAPO'

Kipashio 'iwapo' ni kitambulishi cha kishazi sharti katika Kiswahili. Kitambulishi hiki hutumika katika kishazi elezi cha sharti ili kuonyesha kuwa kishazi chenyewe ni maelezo ya masharti yanayotolewa dhidi ya tendo fulani. Kitambulishi cha kishazi sharti hiki hutumiwa katika njeo tofauti tofauti.

14. Iwapo alisoma kwa bidii alipita mtihani.

Sentensi hii ina vishazi viwili. Vishazi hivyo ni;

(i) Iwapo alisoma kwa bidii.

(ii) Alipita mtihani.

Kishazi elezi cha sharti katika sentensi hii ni 'Iwapo alisoma kwa bidii'. Kishazi kikuu ni 'alipita mtihani'. Sentensi yenyewe imeandikwa katika njeo ya wakati uliopita. sentensi ina maana kuwa anayerejelewa alistahili kusoma kwa bidii ili aweze kupita mtihani. Kama hakusoma kwa bidii, basi inamaanisha kuwa hakupita mtihani. Kitendo cha kuupita mtihani kilitegemea sharti linalotolewa katika kishazi elezi cha sharti. Sharti hilo ni kusoma kwa bidii. Kipashio 'iwapo' kimetumiwa kutambulisha sharti hilo. Kipashio

‘iwapo’ kinaweza kutumiwa kutambulisha kishazi sharti kikitokea kabla ya kishazi kikuu au baada ya kishazi kikuu katika sentensi. Katika sentensi ya (14) hapo juu, kitambulishi hiki cha kishazi sharti kimetumiwa kutambulisha kishazi sharti kilicho mbele ya kishazi shurutiwa. Kinaweza pia kutumiwa kutambulisha kishazi sharti kinachotokea baada ya kishazi kikuu kama inavyoonyeshwa katika sentensi ifuatayo.

15. Alipita mtihani iwapo alisoma kwa bidii.

Katika sentensi hii, ‘Alipita mtihani’ ni kishazi kikuu kilichoshurutiwa. Kishazi sharti ni ‘iwapo alisoma kwa bidii.’ Kishazi hiki kimetokea baada ya kishazi kikuu kikiwa kimetambulishwa na ‘iwapo’.

### 2.2.5 KITAMBULISHI SHARTI ‘KI’

Kitambulishi kishazi sharti ‘ki’ hutumiwa katika njeo ya wakati ujao na hali ya mazoea pekee.

Obuchi na Mukhwana (2010), wanaeleza kuwa mofu ‘ki’ huonyesha masharti yanayowezekana. Wanaendelea kueleza kuwa kitendo fulani huenda kisiwezekane leo lakini kikawezekana baadaye iwapo masharti fulani yatatimia. Mfano ni katika sentensi inayofuata.

16. Wachezaji wakicheza vizuri watashinda.

Sentensi ya hapo juu imeandikwa katika njeo ya wakati ujao. Sentensi hii ina vishazi viwili. Vishazi hivyo ni;

(i) Wachezaji wakicheza vizuri.

(ii) Wachezaji watashinda.

‘Wachezaji wakicheza vizuri,’ ni kishazi sharti ilhali ‘Wachezaji watashinda’ ni kishazi kikuu. Mofu ‘ki’ katika kikundi tenzi ‘wakicheza’ imetumika kuonyesha sharti ambalo limehimiliwa katika kishazi ‘wakicheza vizuri’. Maana ya sentensi yenyewe ni kuwa kushinda kwa wachezaji kunategemea kucheza vizuri. Hivyo kama hawatacheza vizuri basi hawatashinda.

Mofu ‘ki’ hutumika kutoa masharti katika hali ya mazoea. Kiambishi hiki hutumiwa na kiambishi cha hali ya mazoea yaani ‘hu’ kuonyesha matukio ambayo hutarajiwa kimazoea kutendeka kutokana na sharti fulani. Mfano ni kama inavyoonyeshwa katika sentensi inayofuata.

17. Wanafunzi wakifunzwa vizuri hupita mtihani.

Sentensi hii inadhirisha kutumiwa kwa ‘ki’ katika kishazi sharti katika sentensi ya hali ya mazoea. ‘Wanafunzi wakifunzwa vizuri’ ni kishazi sharti ilhali ‘wanafunzi hupita mtihani’ ni kishazi kikuu (kishazi shurutiwa) tunamopata mofu ‘hu’. Mofu ‘hu’ imetumika kusawiri hali ya mazoea. Hali ya mazoea ina maana kuwa kitendo fulani hutokea kila wakati kwa jinsi ile ile bila ya matarajio ya kitendo hicho kutokea kwa jinsi nyingine tofauti na ilivyozoelewa. Sentensi (17) hapo juu ina maana kuwa ni kawaida kwa wanafunzi kupita mtihani ikiwa sharti la wanafunzi hao kufunzwa vizuri limetekelezwa.

Kishazi sharti kinachotambulishwa na ‘ki’ huweza kutokea kabla ya kishazi kikuu au baada ya kishazi kikuu. Hali hii inadhihirishwa katika sentensi ifuatayo.

18. Wanafunzi hupita mtihani wakifunzwa vizuri.

Ingawa kishazi sharti katika sentensi ya hapo juu kimetokea baada ya kishazi shurutiwa, hali hii haileti maana tofauti na ile ya sentensi ambayo kishazi sharti kimekitangulia kishazi shurutiwa. Maana inabaki kuwa ile ile.

### 2.2.6 KITAMBULISHI SHARTI 'NGA NA NGALI'

Umbo 'nga' na 'ngali' hutumiwa kutolea masharti katika njeo ya wakati uliopita. 'Nga' na 'ngali' haziwezi kutumiwa kutoa masharti katika njeo ya wakati uliopo wala wakati ujao. Obuchi na Mukhwana (2010) wanaeleza kuwa 'nga' na 'ngali' hutumiwa kueleza kuwa kitendo cha sharti ambacho kilipaswa kutimizwa kimepitwa na wakati na kwa hivyo kitendo shurutiwa hakitatimizwa. 'Nga' na 'ngali' hutumiwa kibadilifu. Maumbo haya hutumiwa kimpishano huru ambapo umbo moja huweza kutumiwa badala ya hilo lingine pasina kubadili maana.

'Nga' na 'ngali' hutumiwa kutambulisha kishazi sharti kama inavyoonyeshwa katika sentensi zifuatazo.

19. (a) Juma angalikuwa na pesa angalijenga nyumba.

(b) Juma angakuwa na pesa angajenga nyumba.

Kila moja ya sentensi za hapo juu ina vishazi viwili. Katika sentensi ya (19a) 'ngali' inajitokeza katika kila kishazi. vile vile katika sentensi ya (19b), 'nga' inajitokeza katika kila kishazi.

Uamuzi wa kutambua ni kipi kishazi shurutiwa na ni kipi kishazi sharti unafanywa kisemantiki. Sentensi (19a na b) zina maana sawa kwani ‘nga’ na ‘ngali’ hutumiwa kimpishano huru bila kubadili maana. Sentensi zote zinatoa maana kuwa kitendo cha Juma kujenga nyumba kinategemea uwezo wa Juma kuwa na pesa. Sentensi zinaarifu kuwa Juma hakuwa na pesa na kwa hivyo hakujenga nyumba. Kujenga nyumba hakungetokea pasina kuwa na pesa. Katika hali hii inabainika kuwa kishazi ‘Juma angalikuwa na pesa’, na ‘Juma angakuwa na pesa’, ndivyo vishazi sharti.

Obuchi na Mukhwana (Khj) wanaeleza kuwa ‘nga’ na ‘ngali’ huweza kutumiwa pamoja na neno ‘kama’ katika tungo moja. Kwa kurejelea matumizi ya neno ‘kama’ tunaweza kung’amua ni kipi kishazi sharti na ni kipi kishazi shurutiwa katika sentensi sharti. Tuangalie mifano ifuatayo.

20 (a) Juma angalijenga nyumba kama (Juma) angalikuwa na pesa.

(b) Juma angajenga nyumba kama (Juma) angakuwa na pesa.

Kutokana na mifano ya hapo juu, kishazi sharti cha (20a) ni ‘Kama (Juma) angalikuwa na pesa’. Sentensi ya (20b) nayo ina kishazi sharti ‘Kama (Juma) angakuwa na pesa’.

Mgullu (1990) anaeleza kuwa katika sentensi sharti, kishazi kile kilicho na neno ‘kama’ huwa ndicho kishazi sharti. Kishazi kile kisicho na neno ‘kama’ huwa ndicho kishazi kikuu. Katika misingi hii, sentensi (20a) ina kishazi kikuu ‘Juma angalijenga nyumba’, na kishazi sharti ‘kama (Juma) angalikuwa na pesa’.

### 2.2.7 KITAMBULISHI SHARTI ‘NGE NA NGELI’

Maumbo ‘nge’ na ‘ngeli’ hutumiwa kutoa masharti katika njeo ya wakati uliopita. Maumbo haya mawili hayatumiwi kutoa masharti katika njeo ya wakati uliopo wala wakati ujao. ‘Nge’ na ‘ngeli’ hutumiwa kuibua maana kuwa sharti ambalo lilipaswa kutekelezwa limepitwa na wakati na kwa hivyo kitendo hakikutimizwa. ‘Nge’ na ‘ngeli hutumiwa kibadilifu kutoa masharti katika sentensi. Maumbo haya hutumiwa kimpishano huru ambapo umbo moja laweza kutumiwa badala ya lingine bila kubadili maana. ‘Nge’ na ngeli hutumiwa kutambulisha kishazi sharti kama inavyoonyeshwa katika sentensi zifwatazo.

21 (a) Mkora angelishikwa umati ungelimuua.

(b) Mkora angeshikwa umati ungemuua.

Katika sentsi (21a), ‘ngeli’ imetokeza katika kishazi cha kwanza na vile vile cha pili. Sentensi (21b) nayo, ‘nge’ imetokeza katika kishazi cha kwanza na cha pili. Katika hali hii, shughuli ya kukitambua kishazi sharti na kishazi shurutiwa inafanywa kwa misingi ya maana inayopatikana katika tungo husika. Sentensi (21a na b) za hapo juu zina maana sawa kwa kuwa, ‘nge’ na ‘ngeli’ hutumiwa kimpishano huru pasina kubadili maana. Sentensi hizi mbili zinatoa maana kuwa kitendo cha kuuawa kwa mkora kinategemea kitendo cha kushikwa kwa mkora huyo. Sharti hapa ni kuwa kitendo cha kumshika mkora kingetimizwa kwanza, ndiposa kile cha kumuua mwizi huyo kiweze kutekelezwa. Katika muktadha wa sentensi hizi mbili, mkora hakushikwa na kwa hivyo umati hukuweza kumua. Kishazi kinachosetiri sharti katika sentensi (21a) ni, ‘mkora angelishikwa’ ilhali

katika sentensii ya (21b) ni, ‘mkora angeshikwa’. ‘Umati ungelimuua’ na ‘umati ungemuua’ ni vishazi shurutiwa katika sentensi (21a na b) mtawalia.

Neno ‘kama’ huweza kutumiwa pamoja na ‘nge’ au ‘ngeli’ katika sentensi sharti ya Kiswahili. Katika hali hii, Mgullu (1990), anaeleza kuwa kishazi kile kilicho na neno ‘kama’ katika sentensi sharti yenye ‘ngeli’ au ‘nge’, huwa ndicho kinachotambuliwa kama kishazi sharti. Kile kisicho na neno ‘ kama’ huwa ndicho kishazi kikuu (kishazi shurutiwa). Hivyo basi tunaweza kutambua kishazi sharti kwa misingi ya matumizi ya neno ‘kama’ inavyoonyeshwa katika sentensi zifuatazo.

22. (a) Kama mkora angelishikwa umati ungelimuua.

(b) Kama mkora angeshikwa umati ungemuua.

Kishazi ‘kama mkora angeshikwa’ katika sentensi ya (22a), ndicho kishazi sharti. Katika sentensi (22b), ‘kama mkora angeshikwa’ ndicho kishazi sharti. Katika vishazi hivi viwili kuna matumizi ya neno ‘kama’ ambalo linaelekeza kutambuliwa kwa vishazi hivyo kama vishazi sharti.

## 2.3.0 MUUNDO WA SENTENSI SHARTI YA KISWAHILI

Katika sehemu hii tunataka kuchunguza jinsi mageuzi katika sentensi sharti ya Kiswahili yanavyotekelezwa kutokana na kanuni za kitengo geuza maumbo cha sarufi. Tumejaribu kutoa ufafanuzi wa muundo wa sentensi sharti ya Kiswahili kwa kutumia kanuni muundo virai za kitengo msingi cha sarufi.

Aidha katika sehemu hii tumevitambua baadhi ya viambajengo ambavyo vinaweza kugeuzwa au kusogezwa kwa kuzingatia kanuni za ugeuza maumbo. Nadharia ya upanuzi wa sarufi sawazishi ina msimamo kuwa sentensi zina muundo wa kiviwango au kitabaka ambao huunda seti za kategoria za viambajengo. Kategoria hizo huwa zimetambuliwa kwa maneno fulani. Muundoviambajengo wa sentensi unaweza kuwasilishwa kwa matumizi ya kielelezo tungo msingi au kwa matumizi ya sentensi za mabano. Kielelezo tungo ni mchoro unaowasilisha seti ya kanuni zinazounda sentensi ambazo hujumuisha kanuni muundo virai za aina ya x-bar.

Tumekwishafafanua kuwa kishazi sharti ni kishazi elezi. Hata hivyo, katika uchunguzi huu, hatutakichanganua kishazi hicho kama kishazi kielezi, badala yake tutakichanganua kama $\mathbf{\overline{S}}$, yaani kishazi kinachotangulizwa kwa kijalizo. Hii ni kwa kuwa kishazi sharti cha Kiswahili ni kishazi bebwa kilichotegemezwa kwa kishazi shurutiwa.

Vipashio vyote vinavyotumika kutanguliza kishazi sharti katika Kiswahili ambavyo ni ‘kama, ikiwa, endapo, iwapo, ki, nga, ngali, nge na ngeli’, tutavichanganua kama vijalizo. Hii ni kwa sababu kila kimojawapo kinabainisha hicho kishazi sharti na tena kinatokea katika nafasi ya kijalizo katika sentensi. Tuki (1990) inaeleza kuwa kijalizo ni kipashio kinachokikamilisha kipashio kingine katika tungo. Uchanganuzi huu tumeukopa kutoka kwa Chomsky (1981) ambako kuna madai kuwa kuna kanuni ya muundo virai katika Kingereza (na katika kila lugha iliyo na vijalizo) inayokubali aina ya vijalizo kubainishwa katika muundo msingi. Kanuni hii katika Kiingereza ni kama:

$\overline{S} \rightarrow$ KIJ – S

Ambapo alama KIJ inawakilisha kifundo cha muundo msingi ambacho kinatawala kijalizo, Bresnan (1970:300). Uchanganuzi huu unachukulia kuwa sentensi inajumuisha kiambajengo Kijalizo na sehemu pendekezo (wazo kuu) S. Tungependa kutaja hapa kuwa tunaenda kutumia $\bar{S}$ kama kifundo kinachotawala kishazi elezi cha sharti.

### 2.3.1 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘KAMA’

Tulivyoeleza awali ni kuwa kishazi sharti ‘kama’ ndicho kilicho na matumizi mengi katika kutambulisha Kizashi sharti katika Kiswahili. Kitambulishi hiki huweza kutumiwa kutambulisha sentensi sharti katika njeo zote. Hebu tutazame jinsi kinavyotumiwa kuwasilisha kishazi sharti katika kiwango cha muundo msingi kutokana na mifano inayofuata.

23. (a) Kama mvua itanyesha basi mimea itanawiri.

(b) $[_{S_1}$ Mimea$_{KN}$ $[$ itanawiri$_{KT}$ $[_{\bar{S}}$ kama $[_{S_2}$ mvua itanyesha $]]]]$

(c) Kama mvua ilinyesha basi mimea ilinawiri

(d) $[_{S_1}$ Mimea$_{KN}$ $[$ ilinawiri$_{KT}$ $[_{\bar{S}}$ kama $[_{S_2}$ mvua ilinyesha $]]]]$

(e) Kama mvua haikunyesha basi mimea haikunawiri.

(f) $[_{S_1}$ Mimea$_{KN}$ $[$haikunawiri$_{KT}$ $[_{\bar{S}}$ kama $[_{S_2}$ mvua haikunyesha $]]]]$

Sentensi (23a na c) ni sentensi ambazo zinafanana lakini zimeandikwa katika njeo tofauti. Sentensi (23a) imeandikwa katika wakati ujao, ilhali ya (23c) imeandikwa katika wakati uliopita. Sentensi (23e) ni aina ya sentensi kanushi. Imekanusha katika wakati uliopita. Sentensi (23a, c na e) ziko katika kiwango cha muundo geuzi. Sentensi (23b, d na f) ni miundo ndani ya (23a, c na e) mtawalia.


Tukiuchukulia mfano wa (23a na b), tunaona kuwa sentensi (23a) inafanana na (23b). Tofauti iliyo baina ya sentensi hizi ni kuwa katika (23a), kishazi sharti kiko mwanzoni mwa sentensi ilhali katika (23b), kishazi sharti kiko mwishoni mwa sentensi. Sentensi (23b) ni muundo msingi wa sentensi (23a) kwa madai kuwa, sentensi inayoanza kwa kishazi kikuu huchukuliwa kuwa ndiyo ya kimsingi huku zile zinazoanza kwa vishazi vya mapendekezo zikichukuliwa kuwa miundo geuzwa inayotokana na miundo msingi. (Mgullu 1990).

Tukichukulia mfano wa (23b), tunaona kuwa sentensi hiyo ambayo ni muundo msingi wa (23a), ina vishazi viwili. Vishazi hivyo ni $S_1$ na $S_2$. Kishazi $S_2$ kimebebwa katika kishazi $S_1$ kwa matumizi ya kiunganishi tegemezi ‘kama’ ambacho kina jukumu muhimu la kutambulisha kishazi sharti.

23. (g) Kama mvua itanyesha.

Muundo msingi wa (23a), unaweza kuwasilishwa kwa matumizi ya kielelezo tungo (24).

24.





Mimea itanawiri kama mvua itanyesha.

Kielelezo tungo (24) ni wasilisho linalodhihirisha vipengee ambavyo tulivitaja katika sura ya pili. Kielelezo tungo kinadhihirisha kuwa sentensi sharti inaundwa kwa vishazi visivyopungua viwili. Vishazi hivyo ni $S_1$ na $\overline{S}$ kwa mfano katika (24). Katika kielelezo tungo (hicho) kishazi kikuu ni kile kinachotawaliwa na $S_1$ ambacho kina viambajengo vyake KN na KT vya juu. Kishazi bebwa ni kile kinachotawaliwa na $\overline{S}$ ambacho kina viambajengo KIJ na $S_2$. Hapa $S_2$ inavitawala viambajengo ambavyo ni KN na KT vya

chini katika kielelezo tungo. Kiambajengo $\bar{S}$ ambacho ni kiambajengo cha chini cha $S_1$ kina uhuru wa kusogezwa. Kinaweza kuwekwa sehemu iliyo kushoto mwa kishazi kikuu katika muundo ambao utaonekana inavyodhihirishwa katika (25).

25.




Kama mvua itanyesha (basi) mimea itanawiri.

Kielelezo tungo (25) kinawasilisha sentensi iliyo katika kiwango cha muundo geuzi. Kielelezo tungo hicho kinatokana na kanuni ya usogezi ambayo inakisogeza kishazi elezi cha sharti hadi nafasi iliyo kabla ya kishazi kikuu, na kisha kuchochea kuchipuka na kuchopekwa kwa ‘basi’, ambayo inakitegemeza kishazi shurutishwa, ambacho sasa kimetangulizwa mwanzoni.

Hata hivyo ‘basi’ ni kipashio ambacho si cha lazima. Kinatumiwa kwa hiari. Ni kipashio ambacho huchochewa tu kwa kutangulizwa kwa kishazi elezi cha sharti. Kipashio ‘basi’ kinajitokeza tu katika muundo geuzi wakati kishazi sharti kinatangulizwa au kuwekwa mbele ya kishazi kikuu (kishazi shurutiwa) kama vile katika (25). Wakati kishazi sharti kinatokea baada ya kishazi shurutishwa kama vile katika (26) hapa chini, itapelekea kipashio ‘basi’ kutohitajika.

26. $[_{S_1}$ Mimea itanawiri $[_{\bar{S}}$ kama $[_{S_2}$ mvua itanyesha $]]]$

Kutokana na sentensi (26) tunaona kuwa ‘basi’ hahitajiki na kwa hivyo haipo katika mpangilio huo. Hii ni kwa kuwa kipashio ‘kama’ kinatekeleza jukumu la kuunganisha hivyo vishazi viwili na vile vile kukitambulisha kishazi sharti.

### 2.3.2 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘IKIWA’

Tumekwisha taja kuwa kitambulishi sharti ‘ikiwa’ kinatumiwa kutambulisha kishazi sharti cha Kiswahili. Mfano ni katika sentensi inayofuata.

27. Ikiwa mwanafunzi atahitimu basi mwalimu atatuzwa.

Hebu sasa tuzame katika kuchunguza muundo msingi wa sentensi sharti inayotambulishwa na ‘ikiwa.’ Sentensi (27) hapo juu ni sentensi iliyo katika kiwango cha

muundo geuzi. Sentensi hiyo inaweza kuwasilishwa katika kiwango cha muundo msingi kama inavyotolewa katika (28).


28. [ Mwalimu KN ]$_{S_1}$ [ atatuzwa KT ] [ ikiwa ]$_{\overline{S}}$ [ mwanafunzi atahitimu ]$_{S_2}$ ] ] ] ]

Sentensi (28) ni muundo msingi wa (27). Sentensi hii ina vishazi viwili ambavyo ni $S_1$ and $S_2$. Vishazi hivi viwili vimeunganishwa pamoja kwa matumizi ya kiunganishi tegemezi ‘ikiwa.’ Licha ya kutekeleza jukumu la kuunganisha vishazi hivyo, ‘ikiwa’ ni kipashio kilicho na jukumu lingine maalum la kutambulisha kishazi sharti. Kitambulishi sharti ‘Ikiwa’ kinatambuliwa chini ya kijalizo ili kishazi elezi cha sharti (29) kiweze kutambuliwa kama $\overline{S}$, (kwa sababu ni sentensi bebwa).

29. Ikiwa mwanafunzi atahitimu

Tulivyosema ni kuwa (28) ni muundo msingi wa (27) ambao ni muundo geuzi. Sentensi (28) yaani muundo msingi wa (27) inaweza kuwasilishwa kwa matumizi ya kielelezo tungo (30).

30.





Mwalimu atatuzwa ikiwa mwanafunzi atahitimu.

Kutokana na kielelezo tungo cha (30), tunaona kuwa kuna vishazi viwili ambavyo ni $S_1$ na $\overline{S}$. $S_1$ ndicho kishazi kikuu ambacho kinatawala KN na KT vya juu kama viambajengo vyake. Kishazi bebwa ni $\overline{S}$ ambacho kinatawala viambajengo KIJ na $S_2$. Hii $S_2$ nayo inatawala viambajengo KN na KT vya chini.

Kishazi $\overline{S}$ kinaweza kusogezwa na kuwekwa nafasi iliyo kushoto mwa kishazi kikuu. Hali hii inadhihirishwa katika kielelezo tungo (31).

31.




Ikiwa mwanafunzi atahitimu (basi) mwalimu atatuzwa.

Kielelezo tungo cha (31) ni wasilisho la muundo geuzi wa (30). Muundo geuzi huu unazaliwa kutokana na kanuni ya usogezi inayoleta mbele kishazi elezi cha sharti hadi nafasi iliyokuwa ya kishazi kikuu na kisha kuchochea kuibuka na kuchopekwa kwa kiunganishi tegemezi 'basi.' Kiunganishi hiki huweza kukitegemeza kishazi shurutishwa ambacho sasa kiko katika nafasi ya mwanzoni mwa sentensi.

Hata hivyo, 'basi' ni kiunganishi kiambatishi cha kitambulishi sharti ambacho si cha lazima. Hata katika muktadha wa 'ikiwa', kutokana na uchochezi unaotokana na usogezi wa kishazi sharti, kiambatishi hiki si cha lazima. 'Basi' inaambatanishwa na 'ikiwa' kutokana na uchochezi unaotokana na kutangulizwa mbele kwa kishazi elezi cha sharti. Kiunganishi hiki 'basi' kinajitokeza tu katika muundo geuzi wakati kishazi sharti

kinatangulizwa mbele ya kishazi shurutishwa kama katika (31). Wakati kishazi sharti kinatokea baada ya kishazi shurutiwa, kama (32) hapa chini, hapo utapata kuwa ‘basi’ haitahitajika.

32. $[_{S_1}$ Mwalimu atatuzwa $[_{\bar{S}}$ ikiwa $[_{S_2}$ mwanafunzi atahitimu $]]]$

‘Basi’ haipo katika (32) kwa sababu ‘ikiwa’ inatekeleza jukumu la kuunganisha vishazi viwili husika na vile vile kutambulisha kishazi sharti.

### 2.3.3 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘ENDAPO’

‘Endapo’ ni umbo lingine linalotumiwa katika sentensi sharti ya Kiswahili ili kuelezea masharti. Hutumiwa kutaja maelezo ya sharti linalohitajika kutimizwa kabla ya kitendo fulani kutekelezwa. Kitendo hicho hutokea kutegemea kutimizwa kwa sharti lililotajwa. Sentensi ifutayo ni mfano wa matumizi ya ‘endapo’ katika kutambulisha sharti.

33. Endapo wanyamapori wataangamizwa, utalii utapungua nchini.

Sentensi (33), ni sentensi sharti inayotambuliwa kwa mujibu wa kitambulishi sharti ‘endapo.’ Sentensi hii ina vishazi viwili ambavyo ni;

i. Endapo wanyamapori wataangamizwa.
ii. Utalii utapungua nchini.

'Endapo wanyamapori wataangamizwa' ndicho kishazi elezi cha sharti. Nacho kishazi 'Utalii utapungua nchini' ni kishazi shurutiwa. Kishazi hiki ndicho kishazi kikuu. Vishazi hivi kwa pamoja vinaiunda sentensi (33) ambayo tunaweza kuirejelea kama kishazi jumuishi.

Maana tunayoipata kutoka sentensi (33) ni kuwa utalii utapungua nchini kwa sharti kuwa wanyamapori wataangamizwa. Kupungua kwa utalii kunategemea kutimizwa kwa kitendo cha kuangamizwa kwa wanyamapori. Hivyo ikiwa wanyamapori hawataangamizwa, basi na utalii hautapungua nchini.

Sentensi (33) imewasilishwa katika kiwango cha muundo geuzi. Katika muundo huu, kishazi sharti kinachotambulishwa na 'endapo' kimetokea kabla ya kishazi shurutiwa. hivyo kishazi shurutiwa kimetokea baada ya kishazi sharti. Sentensi (33) inaweza kuwasilishwa katika kiwango cha msingi kama inavyoonyeshwa katika kielelezo (34) kinachotumia mabano.

34. [ Utalii [ utapungua nchini [ endapo [ wanyamapori [ wataangamizwa. ] ] ] ] ]

KN KT $\overline{S}$ KN KT

$S_1$ $S_2$

Sentensi (33) na (34) zina maana sawa. Sentensi zote zinatoa masharti. Tofauti baina ya sentensi hizi inajitokeza katika kiwango cha muundo wao. Katika sentensi (33), kishazi sharti kimetokea kabla ya kishazi shurutiwa.


Kishazi sharti katika sentensi (34) kimetokea baada ya kishazi shurutiwa. Sentensi (33) ipo katika kiwango cha muundo geuzi ilhali (34) ni uwasilishi wa muundo msingi wa sentensi (33). Hali hii inatokana na sababu tuliyoitaja hapo awali kuwa sentensi sharti ambayo kishazi shurutiwa chake hutokea mwanzoni ndiyo uwasilishi wa muundo msingi.

Sentensi (34) ambayo tumeitambua kama muundo msingi wa (33) ina vishazi viwili. Vishazi hivyo ni $S_1$ na $S_2$. Kishazi $S_2$ ambacho ni kishazi sharti kimetegemezwa kwa kishazi $S_1$ ambacho ni kishazi shurutiwa kwa mujibu wa kiunganishi kitegemezi ‘endapo’. Hali hii inabainisha kuwa umbo ‘endapo’ linatekeleza majukumu mawili katika muktadha wa sentensi sharti ya Kiswahili. Kinakitambulisha kishazi sharti na vile vile kukitegemeza kishazi hicho kwa kishazi shurutiwa.

Kama vitambulishi vingine vya sharti katika Kiswahili, ‘endapo’ inazalishwa chini ya kifundo kijalizo. Hali hii inasababisha kishazi sharti ambacho ni kishazi tegemezi kuwasilishwa kama $\overline{S}$ jinsi tulivyodokeza awali.

Sentensi (34) ambayo ni muundo msingi wa sentensi sharti (33), inaweza kuwasilishwa kwa matumizi ya kielelezo tungo kinachofuata.

35.




Utalii utapungua nchini endapo wanyamapori wataangamizwa.


Kielelezo tungo (35) ni wasilisho la sentensi sharti iliyo katika kiwango cha muundo msingi. Katika kiwango hiki, kishazi shurutiwa kinatokea kabla ya kishazi sharti. Hivyo kishazi elezi cha sharti kinatokea baada ya kishazi shurutiwa.

Katika kielelezo tungo (35), kishazi shurutiwa ni kile kinachotawaliwa na $S_1$ ambacho kina viambajengo KN na KT. Hiki ndicho kishazi kikuu. Kishazi sharti ni kile kinachotawaliwa na $\overline{S}$, na ambacho kina viambajengo KIJ na $S_2$. Kishazi hiki ndicho

kishazi tegemezi. Kwa pamoja vishazi hivi vinawasilisha sentensi sharti iliyo na muundo wa sentensi changamano.

Kishazi sharti katika kielelzo tungo (35) kinaweza kusogezwa kwa ujumla wake kutoka sehemu kilipo na kuhamishwa hadi sehemu iliyo kushoto mwa kishazi shurutiwa. Usogezi huo unapotekelezwa na kukamilika, muundo ufuatao wa sentensi sharti unajitokeza. Sentensi hiyo inajitokeza katika kiwango cha muundo geuzi. Tutazame kielelezo tungo (36).

36.




Endapo wanyamapori wataangamizwa (basi) utalii utapungua nchini.

Kielelezo tungo (36) kimezalishwa kutokana na kanuni ya usogezi inayokihamisha kishazi elezi cha sharti kutoka sehemu iliyo baada ya kishazi shurutiwa, na kukipeleka hadi sehemu iliyo kabla ya kishazi shurutiwa. Wakati wa usogezi huu, kiunganishi kitegemezi 'basi' huchochewa na kuchipuka. Kiunganishi hiki kinaishia kuchopekwa baina ya kishazi sharti na kishazi shurutiwa. Kiunganishi hiki hutokea tu kwa hiari na kwa hivyo si cha lazima katika sentensi sharti tunayoishughulikia. Umbo hili 'basi' hutokea tu katika kiwango cha muundo msingi. Umbo hilo linapotokea katika muundo geuzi, hutekeleza jukumu la kukitegemeza kishazi sharti kwa kishazi shurutiwa.

Usogezi ambao umetekelezwa na kuzalisha kielelezo tungo (36) unaweza kufafanuliwa kwa matumizi ya sentensi za mabano kama inavyotekelezwa kwa kutumia vielelezo vifuatavyo.


**37.** [ ___ utalii utapungua nchini [ endapo [ wanyamapori wataangamizwa. ]]]

Usogezi na kuchipuka kwa 'basi'

Kielelezo cha hapo juu kinafafanua mahali kishazi elezi cha sharti kilipo na ambapo kitatolewa na kusogezwa hadi sehemu kabla ya kishazi shurutiwa.

Kielelezo hiki kinawasilisha sentensi hiyo iliyo katika kiwango cha muundo msingi. Baada ya usogezi unaoashiriwa katika kielelezo hicho kukamilika, muundo ufuatao unatokea.

38




Kutokana na usogezi unaoashiriwa kwa mishale, kishazi elezi cha sharti kimehamishwa kutoka sehemu iliyo baada ya kishazi shurutiwa na kutiwa katika sehemu iliyo kabla ya kishazi shurutiwa. Huku kutangulizwa kwa kishazi sharti kunachochea kuchipuka kwa kiunganishi kitegemezi ‘basi’ kinachochopekwa baina ya vishazi hivi viwili. Kiunganishi ‘basi’ kinakitegemeza kishazi sharti kwa kishazi kikuu katika upande wa kushoto mwa kishazi kikuu. Hata hivyo tumekwisha taja kuwa umbo ‘basi’ si la lazima katika muktadha wa sentensi sharti. Kielelezo (38) kinawasilisha sentensi hiyo katika kiwango cha muundo geuzi. Mchakato huu wote wa usogezi unadhihirisha kuwa kishazi elezi cha sharti kinachotambuliwa na ‘endapo’ kina uhuru wa kusogezwa na hivyo kutokea kabla au baada ya kishazi shurutiwa.

### 2.3.4 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘IWAPO’

Umbo ‘iwapo’ hutumiwa kutoa masharti katika lugha ya Kiswahili. ‘Iwapo’ hutumiwa katika njeo na hali mbalimbali kuwasilisha sentensi sharti. Iwapo ina matumizi sawa na vitambulishi sharti vya Kiswahili ‘ikiwa, endapo, na kama. Mfano ufuatao unatuonyesha jinsi ‘iwapo’ inavyotumiwa kuwasilisha masharti.

39. Iwapo mbunge atajiuzulu, uchaguzi utaandaliwa tena.

Sentensi (39) ni sentensi sharti. Sentensi hii ina vishazi viwili. Kuna kishazi sharti na kishazi shurutiwa. Kishazi sharti ni kile ambacho kimetangulizwa na ‘iwapo.’ Kishazi hiki ni ‘Iwapo mbunge atajiuzulu.’ Nacho kishazi shurutiwa hapa ni ‘uchaguzi utaandaliwa tena’. Vishazi hivi viwili ndivyo viambajengo vikuu vinavyoiunda sentensi sharti ya hapo juu.

Katika sentensi (39) kuna vitenzi viwili vikuu. Kitendo cha kwanza ni kujiuzulu kwa mbunge na cha pili ni kuandaliwa kwa uchaguzi. Sharti linalopatikana katika sentensi hii ni kuwa lazima kitendo cha mbunge kujiuzulu kitimizwe kwanza ndipo kile cha kuandaliwa kwa uchaguzi kiweze kutekelezwa. Kwa hivyo ikiwa mbunge hatajiuzulu, basi uchaguzi hautaandaliwa tena. Kishazi kinacholisetiri sharti hili kimetangulizwa na ‘iwapo.’

Kishazi sharti ambacho kinatambulishwa na ‘iwapo’ kimejitokeza mwanzoni mwa sentensi. Sentensi yenyewe iko katika kiwango cha muundo geuzi. Sentensi hiyo inaweza kuwasilishwa katika kiwango cha muundo msingi inavyodhihirishwa katika sentensi ifuatayo.

40 [[Uchaguzi [utaandaliwa tena [iwapo [mbunge atajiuzulu.]]]]]

KN KT $\overline{S}$ KN KT

$S_1$ $S_2$

Sentensi (40) inasetiri maana sawa na sentensi (39). Tofauti inayojitokeza baina ya sentensi hizi mbili ni kuwa katika sentensi (39), kishazi sharti kimetokea kabla ya kishazi


shurutiwa. Katika sentensi (40), kishazi sharti kimetokea baada ya kishazi shurutiwa. Sentensi (40) ni muundo msingi wa sentensi (39). Ubainishi huu unatokana na ukweli kuwa sentensi sharti inayoanza na kishazi shurutiwa huwa ndio uwasilishi wa muundo msingi.

Sentensi (40) ina vishazi viwili. Vishazi hivyo ni $S_1$ na $S_2$. Kishazi $S_2$ kimebebwa katika kishazi $S_1$. Kitambulishi sharti 'iwapo' kimetekeleza jukumu la kutambulisha kishazi sharti na pia kuviunganisha vishazi hivyo viwili kwa mujibu wa kukitegemeza kishazi sharti kwa kishazi shurutiwa.

Kitambulishi sharti 'iwapo' huzalishwa chini ya kifundo kijalizo. Hali hii husababisha kishazi sharti kinachotambulishwa na 'iwapo' ambacho ni kishazi tegemezi kuwasilishwa kama $\overline{S}$.

Sentensi (40) ambayo ni muundo msingi wa (39) inaweza kuwasilishwa kwa matumizi ya kielelezo tungo kinachofuata.

41.





Uchaguzi utaandaliwa tena iwapo mbunge atajiuzulu.

Kielelezo tungo (41) kinadhihirisha vishazi viwili vilivyoshirikishwa kuunda sentensi sharti yenye kitambulishi sharti ‘iwapo.’ Vishazi hivyo ni kishazi shurutiwa na kishazi sharti. Katika kielelezo tungo (41), kishazi shurutiwa ni kile kinachotawaliwa na $S_1$ ambacho kina viambajengo KN na KT. Hiki ndicho kishazi kikuu. Kishazi sharti ni kile kinachotawaliwa na $\overline{S}$ , ambacho kina viambajengo KIJ na $S_2$. Hiki ndicho kishazi tegemezi.

Kishazi sharti katika kielelezo tungo cha hapo juu kinaweza kusogezwa kutoka sehemu kilipo na kutiwa sehemu iliyo kushoto mwa kishazi shurutiwa. Usogezi huo unapokamilika, muundo ufuatao wa sentensi sharti unadhihirishwa.

42.




Iwapo mbunge atajiuzulu (basi) uchaguzi utaandaliwa tena.

Kielelezo tungo (42) ni matokeo ya usogezi uliofanyiwa kielelezo tungo (41). Kielelezo tungo hicho kimezaliwa kutokana na kanuni ya usogezi inayokisogeza kishazi elezi cha sharti na kukitua katika nafasi iliyo kabla ya kishazi kikuu.

Wakati wa mchakato huo, kiunganishi tegemezi 'basi' kinachochewa kuchipuka. Kiunganishi hiki kinachopekwa baina ya kishazi sharti na kishazi shurutiwa. Kiunganishi hiki si cha lazima. Kinajitokeza tu kihiari wakati wa kutanguliza kishazi sharti. Hata hivyo kinapochopekwa baina ya vishazi hivyo viwili, huweza kutekeleza jukumu la kukitegemeza kishazi sharti kwa kishazi shurutiwa. Kiunganishi 'basi' hujitokeza tu katika kiwango cha muundo geuzi. Huwa hakipatikani katika muundo msingi katika muktadha wa sentensi sharti tunayoishughulikia.

Uhamisho uliotekelezwa katika kielelezo tungo (42) unaweza kuelezewa kwa matumizi ya sentensi za mabano inavyoonyeshwa katika vielelzo vifuatavyo.

43. [$_{S_1}$ ___ uchaguzi utaandaliwa tena [iwapo [$_{S_2}$ Mbunge atajiuzulu. ]]]

Usogezi na kuchipuka kwa 'basi'

Kielelezo cha hapo juu kinaonyesha mahali kishazi sharti kilipo na ambapo kitatolewa na kusogezwa hadi sehemu kabla ya kishazi shurutiwa. Baada ya usogezi kutekelezwa na kukamilika, muundo ufuatao unapatikana.

44. [Iwapo [mbunge atajiuzulu] basi [uchaguzi utaandaliwa tena ___ ]]

Kishazi sharti kinasogezwa kama inavyoashiriwa na mishale na kutua sehemu kabla ya kishazi shurutiwa. Hali hii inachochea kuchipuka kwa kiunganishi tegemezi 'basi' ambacho kinakitegemeza kishazi sharti katika upande wa kushoto mwa kishazi kikuu. Hali hii inadhihirisha usogevu wa kishazi elezi cha sharti kinachoweza kutokea kabla au baada ya kishazi shurutiwa.

### 3.2.5 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘KI’

Mofu ‘ki’ hutumiwa kutoa masharti katika njeo ya wakati ujao, na vile vile katika hali ya mazoea. Ifuatayo ni mifano ya matumizi ya mofu ‘ki’ katika sentensi sharti ya Kiswahili.

45. Mgeni akitaka kula, mama atapika.

46. Mgeni akitaka kula, mama hupika.

Sentesni (46) ya hapo juu imeandikwa katika njeo ya wakati uliopita. Sentensi (46) imeandikwa katika hali ya mazoea. Sentensi (45) ina vishazi viwili ambavyo ni;

(i) Mgeni akitaka kula.

(ii) Mama atapika.

Maana inayoibuka kutokana na sentensi (45) ni kuwa kitendo cha mama kupika kitatekelezwa baada ya kile cha mgeni kufika, mama hatapika kutokana na hali hii inabainika kuwa ‘mama atapika’ ni kishazi shurutiwa ilhali ‘mgeni akitaka kula’ ni kishazi sharti. Sentensi (46) nayo ina vishazi viwilli. Vishazi hivyo ni;

(i) Mgeni akitaka kula.

(ii) Mama hupika.

Maana inayopatikana katika sentensi hii ni kuwa kitendo cha mgeni kutaka kula ni lazima hutimizwa kwanza ndipo kile cha mama kupika kutokea. Sentensi hii imeandikwa katika hali ya mazoea. Mofu ‘hu’ katika kishazi “mama hupika” ndiyo imetumiwa kuonyesha hali ya kitendo kuzoelewa kutendeka kwa jinsi ile ile kila wakati. Sentensi ina maana kuwa kila wakati mgeni anapotaka kula, ni kawaida mama kupika kutokana na kutaka

kula huko kwa mgeni. Katika muktadhaa wa sentensi hii, ikiwa mgeni hataki kula, basi mama huwa hapiki.


Tukirejelea sentensi ya (45) inabainikia kuwa sentensi hiyo imeandikwa katika kiwango cha muundo geuzi. Katika kiwango cha muundo msingi, sentensi hiyo inawasilishwa inavyoonyeshwa katika kielelezo (47).

47. [Mama atapika [mgeni akitaka kula.]]

S S

Sentensi (47) ina maana sawa na sentensi (45). Tofauti iliyo baina ya sentensi hizi mbili ni kuwa katika (45), kishazi sharti kinatangulia kishazi shurutiwa ilhali katika (47), kishazi sharti kinatokezea baada ya kishazi shurutiwa. Sentensi (47) inaweza kuwasilishwa kwa matumizi ya kielezo tungo kifuatacho.

48.





Mama atapika mgeni akitaka kula.

Kielelezo tungo (48) kinaonyesha kuwa kuna vishazi viwili vilivyotumiwa kuunda sentensi moja. Vishazi hivyo ni $S_1$ na $\bar{S}$ . Katika kielezo tungo hiki, kishazi kikuu ni kile ambacho kinatawaliwa na $S_1$. Hiki ndicho kishazi shurutiwa. Kishazi $\bar{S}$ na ambacho kina kimbajengo KIJ na $S_2$ ndicho kishazi bebwa. Hiki kishazi bebwa ndicho pia kishazi sharti.

Kishazi $\bar{S}$ ambacho ni kishazi sharti kina uhuru wa kusogezwa. Kutoka mahali kilipo na kuhamishwa hadi sehemu iliyo kushoto mwa kishazi kikuu inavyoonyeshwa katika muundo ufuatao.

49.




Mgeni akitaka kula (basi) mama atapika.

Kielelezo tungo (49) kinawasilisha muundo geuzi wa sentensi (48). Muundo huu umezaliwa kutokana na kanuni ya usogezi ambayo inakihamisha kishazi elezi cha sharti hadi nafasi iliyo kabla ya kishazi shurutiwa. Hali hii inasababisha geuzi la kuchipuka kwa kiunganishi tegemezi ‘basi’. Kiunganishi hiki si cha lazima. Huchipuka na kuchopekwa kwa hiari. Kiunganishi kitegemezi ‘basi’ kinatekeleza jukumu la kukitegemeza kishazi sharti kwa kishazi kikuu. Hivi sasa mageuzi yamekamilika na kishazi sharti kimetangulizwa na kutokea kabla ya kishazi shurutiwa.

Tumetaja hapa kuwa umbo ‘basi’ si la lazima katika mpangilio wa viambajengo vya sentensi sharti. Huwa hakipo katika muundo msingi wa sentensi sharti. Kiunganishi hiki hujitokeza tu katika muundo geuzi kutokana na kule kuhamishwa kwa kishazi sharti kutoka sehemu iliyo baada ya kishazi kikuu hadi sehemu iliyo kabla ya kishazi kikuu. Ikiwa ugeuzi utafanywa na kishazi sharti kitokee baada ya kishazi kikuu, hali hii itapelekea kipashio ‘basi’ kutohitajika na hivyo kudondoshwa kutoka kwa mpangilio wa viambajengo inavyoonyeshwa katika (50).

**50**. [ Mama atapika [ mgeni akitaka kula. ] ]

Sentensi ya (50) inayoonyesha kuwa kiunganishi ‘basi’ hakihitajiki na kwa hivyo hakipo katika mpangilio wa sentensi hiyo. Jukumu lake (ambalo si la lazima) la kuunganisha vishazi hiyvo viwili linatekelezwa na mofu ‘ki’. Kwa hivyo ‘ki’ inatekeleza majukumu mawili. Inatumika kutambulisha sharti na vile vile kukitegemeza kishazi sharti kwa kishazi kikuu.

### 2.3.6 MUUNDO WA SENTENSI YENYE 'NGA NA NGALI'

'Nga' na 'ngali' ni maumbo yanayotumiwa kutoa masharti katika lugha ya Kiswahili. Maumbo haya hutumiwa kutolea masharti hayo katika njeo ya wakati uliopita pekee. Katika muktadha wa sentensi ya sharti, 'nga' na 'ngali' hazitumiwi kutolea masharti katika wakati uliopo wala wakati ujao. Mgullu (1990) anaeleza kuwa umbo 'nga' na 'ngali' hutumiwa kibadilifu bila kubadili maana. Maoni haya ni sawa na ya Obuchi na Mukwana (2010) wanaosema kuwa, 'nga' na 'ngali' hutumiwa kimpishano huru. Hii inatupa maana kuwa 'nga' inaweza kutumiwa badala ya 'ngali' bila kubadilisha maana katika tungo. Kwa kutumia mifano ifuatayo, tungependa kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu 'nga' na 'ngali'.

51. Maria angalikuwa na jiko angalipika chakula.
52. Maria angakuwa na jiko angapika chakula.

Sentensi (51) na (52) ni sentensi sahihi zinazotoa masharti katika njeo ya wakati uliopita. Sentensi hizi zina maana sawa. Kila moja ya sentensi hizi ina vishazi viwili. Katika sentensi ya (51), kitambulishi sharti 'ngali' kinatokezea katika vishazi vyote viwili. Vile vile katika sentensi (52) kitambulishi sharti 'nga' kinatokezea katika vishazi vyote viwili. Sentensi (a) ina vishazi vifuatavyo.

(i) Maria angalikuwa na jiko.
(ii) Maria angalipika chakula.

Sentensi (52) nayo ina vishazi vifuatavyo

(i) Maria angakuwa na jiko.

(ii) Maria angapika chakula.

Kutokana na ukweli kuwa ‘nga’ inajitokeza katika vishazi vyote, na ngali ikitokea vivyo hivyo, kuna haja ya kufanya uamuzi kukitambua kishazi kikuu na kishazi sharti. Kwa kutumia misingi ya kisemantiki, tunaweza kung’amua ni kishazi kipi kinachosetiri sharti na ni kipi kishazi kikuu. Kwa kuwa sentensi zote zina maana sawa, inabainika kuwa kitendo cha Maria kupika chakula kilitegemea kitendo cha kuwa na jiko. Sharti la kuwa na jiko lilitumainiwa kutimizwa kwanza ndipo kile kitendo cha kupika chakula kitekelezwe. Kwa kuwa Maria hakuwa na jiko, hakuweza kupika chakula. Kutokana na maelezo haya inatudhihiririkia kuwa kishazi ‘Maria angalikuwa na jiko’ na kile ‘Maria angakuwa na jiko’ ndivyo vishazi sharti. ‘Angalipika chakula’ na ‘Angapika chakula’ ni vishazi shurutiwa.

Obuchi na Mukhwana (khj) wanaeleza kuwa neno ‘kama’ linaweza kutumiwa pamoja na ‘nga’ au ‘ngali’ katika sentensi sharti. Kutokana na hali hii, Mgullu (1990) anaeleza kuwa kishazi kile kilicho na neno ‘kama’ ndani yake, ndicho kinachotambuliwa kama kishazi sharti. Kile kisicho na neno ‘kama’ ndani yake, ndicho kinatambuliwa kama kishazi kikuu. Mifano ifuatayo itatusaidia kulifafanua wazo hili.

53. Kama Maria angalikuwa na jiko angalipika chakula

54. Kama Maria angakuwa na jiko angapika chakula.

Kishazi ‘Kama Maria angalikuwa na jiko’ na kile ‘Kama Maria angakuwa na jiko’ ndivyo vishazi sharti. Hii ni kwa kuwa katika vishazi hivi kuna matumizi ya neno ‘kama’ ambalo hutumiwa kama kitambulishi sharti. Kishazi ‘(Maria) angalipika chakula’ na kile

‘(Maria) angapika chakula’ ni vishazi shurutiwa. Ndani yao hamna matumizi ya neno ‘kama’.

Kufikia hapa tumeweza kukitambua kishazi sharti na kishazi shurutiwa katika sentensi sharti iliyo na kitambulishi sharti ‘nga’ na ‘ngali’. Tungependa basi kuchunguza ni hali gani inayosababisha kuwepo kwa ‘nga’ na ‘ngali’ kama vitambulishi sharti katika lugha ya Kiswahili.

Mifano ya sentensi (53) na (54) hapo juu inathibitisha mawazo ya Mgullu (khj) anayeeleza kuwa kuna uwezekano wa kutumia ‘nga’ pekee bila kuiunganisha na ‘li’. Katika muktadha huu wa sentensi sharti, ‘nga’ ni kitambulishi sharti ilhali ‘li’ ni kiambishi kipatanishi cha njeo ya wakati uliopita. Wakati mwingine kiambishi kipatanishi cha njeo ‘li’ hudondoshwa ikiwa kuna kijalizo cha sharti ‘nga’ katika kikundi tenzi kimoja. Kipashio hicho ‘li’ kinapodondoshwa maana ya sentensi huwa haibadiliki kamwe, na sentensi husalia kuwa sahihi.

Wesana-chomi (1986) anafafanua kuwa katika muktadha wa sentensi sharti, ‘nga’ ni kijalizo kinachotumiwa katika sentensi sharti ilhali ‘li’ ni kitambulishi cha njeo ya wakati uliopita. Kutokana na maelezo haya inabainika kuwa si lazima ‘li’ itumiwe pamoja na ‘nga’. ‘Li’ inatumiwa kihiari na inaweza kujitokeza katika muundo geuzi au idondoshwe katika mchakato wa kuigeuza sentensi kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo geuzi. Hali hii inadhihirisha kuwa ‘nga’ na ‘li’ ni mofu tofauti. Kila moja ya mofu hizi ina jukumu tofauti la kisintaksia. ‘Nga’ ina jukumu la kutambulisha sharti katika kishazi sharti ilhali ‘li’ ina jukumu la kutambulisha njeo ya wakati uliopita. Matumizi ya ‘nga’ katika sentensi sharti ya Kiswahili yamebanwa katika wakati uliopita

peke yake. Ni kutokana na ukweli huu kwamba ‘nga’ inatumiwa katika njeo ya wakati uliopita, ambapo kutokea kwake na ‘li’ katika kikundi tenzi kimoja, inahisiwa kuwa maumbo haya yanajitokeza sawia na kujirudia kutekeleza jukumu la kutambulisha njeo. Katika muktadha kama huu, njeo ya wakati uliopita huweza kutambulishwa kwa kutumia ‘nga’. Kutokana na hali kama hii, wakati mwingine inapelekea ‘li’ kudondoshwa. Ni kwa misingi hii tunakuwa na kitambulishi sharti ‘nga’ au ‘ngali’ katika kishazi cha sentensi sharti ya Kiswahili. Hata hivyo inastahili kueleweka kuwa ‘nga’ na ‘ngali’ hazitumiwi kwa pamoja katika sentensi moja. Kila moja hutumiwa kivyake bila kuzichanganya. Mfano wa sentensi inayofuata ina matumizi ya ‘nga’ na ‘ngali’ ambayo si sahihi.

55. * Mkulima angapanda mapema angalipata mazao mengi.

Sentensi hii si sahihi na haikubaliki kwa sababu ‘nga’ na ‘ngali’ zimetumiwa kwa kuchanganywa pamoja katika sentensi moja isivyostahili. Matumizi sahihi huhitaji kila moja ya maumbo haya litumiwe peke yake katika sentensi sharti bila kulitumia hilo lingine katika sentensi hiyo hiyo. Matumizi sahihi ni kama inavyodokezwa katika tungo zifuatazo.

56. Mkulima angapanda mapema angapata mazao mengi.

au

57. Mkulima angalipanda mapema angalipata mazao mengi.


Kufikia hapa tumeeleza misingi ya kutokea na kutumiwa kwa kitambulishi sharti ‘nga’ na ‘ngali’ katika sentensi sharti ya Kiswahili. Tungependa kuwasilisha sentensi sharti yenye kitambulishi ‘nga’ na ‘ngali’ katika kiwango cha muundo msingi na kudhihirisha ugeuzi

unaojitokeza wakati aina hii ya sentensi inapogeuzwa hadi kiwango cha muundo geuzi. Sentensi ‘Maria angalikuwa na jiko angalipika chakula’ imewasilishwa katika kiwango cha muundo geuzi. Sentensi hii inaweza kuwasilishwa katika kiwango cha muundo msingi kama ifuatavyo.

58. [Maria angalipika chakula [kama (Maria) angalikuwa na jiko]]

Kishazi ‘Maria angalipika chakula’ ndicho kishazi shurutiwa. Kishazi kilicho na neno ‘kama’ huwa ndicho kishazi sharti. Kwa hivyo kishazi sharti hapa ni ‘kama (Maria) angalikuwa na jiko’. Sentensi ‘Maria angalipika chakula kama (Maria) angalikuwa na jiko’, ambayo ni muundo msingi wa sentensi ‘Maria angalikuwa na jiko angalipika chakula’, inaweza kuwasilishwa kwa matumizi ya kielelezo tungo kinachofuata.

59.





Maria angalipika chakula kama (Maria) angalikuwa na jiko.

Kielelezo tungo cha hapo juu kinatuonyesha kuwa kitambulishi cha sharti ‘nga’ kinazalishwa chini ya kifundo cha kikundi tenzi katika kishazi shurutiwa. Vitambulishi sharti ‘kama’ na ‘nga’ vinazaliwa chini ya kifundo cha kijalizo katika kishazi sharti. Kanuni ya uhamishaji hukihamisha kitambulishi sharti ‘nga’ kutoka kifundo cha kijalizo hadi sehemu ya kifundo cha kikundi tenzi katika kishazi sharti. Kitambulishi sharti ‘nga’ huchopekwa baina ya kiambishi kipatanishi ngeli na kiambishi kitambulishi cha njeo ya wakati uliopita-(li).

Sentensi (58) ya hapo juu huweza kugeuzwa kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo geuzi. Katika ugeuzi huo kishazi sharti husogezwa na kuwekwa katika nafasi iliyo kushoto mwa kishazi kikuu. Kishazi sharti kinatangulizwa huku kishazi kikuu kikitokea baada ya kishazi sharti. Hali hii inadhihirishwa na kielelezo tungo kifuatacho.

60.




Kama Maria anga(li)kuwa na jiko (Maria) anga(li)pika chakula

Kielelezo tungo cha hapo juu, kinadhihirisha kuwa kishazi sharti kinachotambulishwa na ‘nga’ au ‘ngali’ kina uhuru wa kuhama na kutokeza katika sehemu kabla ya kishazi kikuu au kutokeza baada ya kishazi kikuu. Uhamisho huo tunaweza kuuita utangulizaji wa kishazi sharti. Tunatambua kuwa wakati wa mchakato wa kuigeuza sentensi ya hapo juu kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo geuzi, kitambulishi cha njeo ya wakati uliopita (li) huweza kutokea katika muundo geuzi au kutotokea. Hali hii hufanyika kihiari. Kitambulishi hicho cha njeo kinapotokea katika muundo geuzi, huungwa pamoja na mofu ‘nga’ na kuunda umbo ‘ngali’, ambalo hutumika kutolea

masharti. Ikiwa kitambulishi njeo ‘li’ hakitokei katika muundo geuzi, basi kunakuwa na umbo ‘nga’ pekee lisiloambatanishwa na kitambulishi (li) cha njeo ya wakati uliopita. Hali hii hutokea kwa sababu katika muktadha wa sentensi sharti, ‘nga’ hutumiwa katika njeo ya wakati uliopita peke yake. Kiambishi kitambulishi cha njeo ya wakati uliopita (li) huweza kudondoshwa na kuacha jukumu la kutambulisha njeo kutekelezwa na ‘nga’. Hali hii hupelekea ‘nga’ kutekeleza jukumu la kutambulisha sharti hali kadhalika lile la kutambulisha njeo ya wakati uliopita.

### 2.3.7 MUUNDO WA SENTENSI YENYE ‘NGE NA NGELI’

‘Nge’ na ‘ngeli’ ni maumbo yanayotumiwa kutoa masharti katika lugha ya Kiswahili. Maumbo haya sawa na ‘nga’ na ‘ngali’, hutumiwa kutolea masharti hayo katika njeo ya wakati uliopita pekee. Katika muktadha wa sentensi sharti, ‘nge’ na ‘ngeli’ hazitumiwi kutolea masharti katika wakati uliopo wala wakati ujao. Mgullu (1990) anaeleza kuwa umbo ‘nge’ na ‘ngeli’ hutumiwa kibadilifu bila kubadili maana. Maoni haya ni sawa na ya Obuchi na Mukwana (2010) wanaosema kuwa, ‘nge’ na ‘ngeli’ hutumiwa kimpishano huru. Hii inatupa maana kuwa ‘nge’ inaweza kutumiwa badala ya ‘ngeli’ bila kubadilisha maana katika tungo. Kwa kutumia mifano ifuatayo, tungependa kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu ‘nge’ na ‘ngeli’.

61. Shule ingelijengwa watoto wangelisoma.

62. Shule ingejengwa watoto wangesoma.

Sentensi (61) na (62) ni sentensi sahihi zinazotoa masharti katika njeo ya wakati uliopita. Sentensi hizi zina maana sawa. Kila moja ya sentensi hizi ina vishazi viwili. Katika sentensi ya (61), kitambulishi sharti ‘ngeli’ kinatokezea katika vishazi vyote viwili. Vile vile katika sentensi (62) kitambulishi sharti ‘nge’ kinatokezea katika vishazi vyote viwili. Sentensi (a) ina vishazi vifuatavyo.

i. Shule ingelijengwa.
ii. Watoto wangelisoma.

Sentensi (62) nayo ina vishazi vifuatavyo.

i. Shule ingejengwa.
ii. Watoto wangesoma.

Kutokana na ukweli kuwa ‘nge’ inajitokeza katika vishazi vyote, na ngeli ikitokea vivyo hivyo, kuna haja ya kufanya uamuzi kukitambua kishazi kikuu na kishazi sharti. Kwa kutumia misingi ya kisemantiki, tunaweza kung’amua ni kishazi kipi kinachosetiri sharti na ni kipi kishazi kikuu. Kwa kuwa sentensi zote zina maana sawa, inatubainikia kuwa kitendo cha watoto kusoma kilitegemea kitendo cha shule kujengwa. Sharti la kujengwa shule lilitumainiwa kutimizwa kwanza ndipo kile kitendo cha watoto kusoma kitekelezwe. Kwa kuwa shule haikujengwa, watoto hawakusoma. Kutokana na maelezo haya inadhihirika kuwa kishazi ‘Shule ingelijengwa’ na kile ‘Shule ingejengwa’ ndivyo vishazi sharti. ‘Watoto wangelisoma’ na ‘watoto wangesoma’ ni vishazi shurutiwa.

Obuchi na Mukhwana (khj) wanaeleza kuwa neno ‘kama’ linaweza kutumiwa pamoja na ‘nge’ au ‘ngeli’ katika sentensi sharti. Kutokana na hali hii, Mgullu (1990) anaeleza kuwa

kishazi kile kilicho na neno ‘kama’ ndani yake, ndicho kinachotambuliwa kama kishazi sharti. Kile kisicho na neno ‘kama’ ndani yake, ndicho kinatambuliwa kama kishazi kikuu. Mifano ifuatayo itatusaidia kulifafanua wazo hili:

63. Kama Shule ingelijengwa watoto wangelisoma

64. Kama Shule ingejengwa watoto wangesoma.

Kishazi ‘Kama shule ingelijengwa’ na kile ‘Kama shule ingejengwa’ ndivyo vishazi sharti. Hii ni kwa kuwa katika vishazi hivi kuna matumizi ya neno ‘kama’ ambalo hutumiwa kama kitambulishi sharti. Kishazi ‘watoto wangelisoma’ na kile ‘watoto wangesoma’ ni vishazi shurutiwa. Ndani yao hamna matumizi ya neno ‘kama’.

Kufikia hapa tumeweza kukitambua kishazi sharti na kishazi shurutiwa katika sentensi sharti iliyo na kitambulishi sharti ‘nge’ na ‘ngeli’. Tungependa basi kuchunguza ni hali gani inayosababisha kuwepo kwa ‘nge’ na ‘ngeli’ kama vitambulishi sharti katika lugha ya Kiswahili.

Mifano ya sentensi (63) na (64) hapo juu inathibitisha mawazo ya Mgullu (khj) anayeeleza kuwa kuna uwezekano wa kutumia ‘nge’ pekee bila kuiunganisha na ‘li’. Katika muktadha huu wa sentensi sharti, ‘nge’ ni kitambulishi sharti ilhali ‘li’ ni kiambishi kipatanishi cha njeo ya wakati uliopita. Wakati mwingine kiambishi kipatanishi cha njeo ‘li’ hudondoshwa ikiwa kuna kijalizo cha sharti ‘nge’ katika kikundi tenzi kimoja. Kipashio hicho ‘li’ kinapodondoshwa maana ya sentensi huwa haibadiliki kamwe, na sentensi husalia kuwa sahihi.

Wesana-chomi (1986) anafafanua kuwa katika muktadha wa sentensi sharti, ‘nge’ ni kijalizo kinachotumiwa katika sentensi sharti ilhali ‘li’ ni kitambulishi cha njeo ya wakati uliopita. Kutokana na maelezo haya inabainika kuwa si lazima ‘li’ itumiwe pamoja na ‘nge’. ‘Li’ inatumiwa kihiari na inaweza kujitokeza katika muundo geuzi au idondoshwe katika mchakato wa kuigeuza sentensi kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo geuzi. Hali hii inadhihirisha kuwa ‘nge’ na ‘li’ ni mofu tofauti. Kila moja ya mofu hizi ina jukumu tofauti la kisintaksia. ‘Nge’ ina jukumu la kutambulisha sharti katika kishazi sharti ilhali ‘li’ ina jukumu la kutambulisha njeo ya wakati uliopita. Matumizi ya ‘nge’ kama yale ya ‘nga’ katika sentensi sharti ya Kiswahili, yamebanwa katika wakati uliopita peke yake. Ni kutokana na ukweli huu kwamba ‘nge’ inatumiwa katika njeo ya wakati uliopita, ambapo kutokea kwake  na ‘li’ katika kikundi tenzi kimoja, inahisiwa kuwa maumbo haya yanajitokeza sawia na kujirudia kutekeleza jukumu la kutambulisha njeo. Katika muktadha kama huu, njeo ya wakati uliopita huweza kutambulishwa kwa kutumia ‘nge’ jinsi ‘nga’ inavyotumiwa. Kutokana na hali kama hii, inapelekea ‘li’ kudondoshwa wakati mwingine. Ni kwa misingi hii tunakuwa na kitambulishi sharti ‘nge’ au ‘ngeli’ katika kishazi cha sentensi sharti ya Kiswahili. Hata hivyo inastahili kueleweka kuwa ‘nge’ na ‘ngeli’ hazitumiwi kwa pamoja katika sentensi moja. Kila moja hutumiwa kivyake bila kuzichanganya. Mfano wa sentensi inayofuata ina matumizi ya ‘nge’ na ‘ngeli’ ambayo si sahihi.

65. * Nyumba ingepakwa rangi ingelipendeza.

Sentensi hii si sahihi na haikubaliki kwa sababu ‘nge’ na ‘ngeli’ zimetumiwa kwa kuchanganywa katika sentensi moja isivyostahili. Matumizi sahihi huhitaji kila moja la

umbo hili litumiwe peke yake katika sentensi sharti bila kulitumia hilo lingine katika sentensi hiyo hiyo. Matumizi sahihi ni kama inavyodokezwa katika tungo zifuatazo.

66. Nyumba ingepakwa rangi ingependeza.

au


67. Nyumba ingelipakwa rangi ingelipendeza.

Kufikia hapa tumeeleza misingi ya kutokea na kutumiwa kwa kitambulishi sharti ‘nge’ na ‘ngeli’ katika sentensi sharti ya Kiswahili. Tungependa kuwasilisha sentensi sharti yenye kitambulishi nge na ‘ngeli’ katika kiwango cha muundo msingi na kudhihirisha ugeuzi unaojitokeza wakati aina hii ya sentensi inapogeuzwa hadi kiwango cha muundo geuzi. Sentensi ‘Shule ingelijengwa watoto wangelisoma’ imewasilishwa katika kiwango cha muundo geuzi. Sentensi hii inaweza kuwasilishwa katika kiwango cha muundo msingi kama ifuatavyo.

68. [Watoto wangelisoma [kama shule ingelijengwa]]

Kishazi ‘Watoto wangelisoma’ ndicho kishazi shurutiwa. Kishazi kilicho na neno ‘kama’ huwa ndicho kishazi sharti. Kwa hivyo kishazi sharti hapa ni ‘kama shule ingelijengwa’. Sentensi ‘Watoto wangelisoma kama shule ingelijengwa’, ambayo ni muundo msingi wa sentensi ‘Shule ingelijengwa watoto wangelisoma’, inaweza kuwasilishwa kwa matumizi ya kielelezo tungo kinachofuata.

69





Watoto wangelisoma kama shule ingelijengwa.

Kielelezo tungo (69) kinaonyesha kuwa kitambulishi cha sharti ‘nge’ kinazalishwa chini ya kifundo cha kikundi tenzi katika kishazi shurutiwa. Vitambulishi sharti ‘kama’ na ‘nge’ vinazaliwa chini ya kifundo cha kijalizo katika kishazi sharti. Kanuni ya uhamishaji hukihamisha kitambulishi sharti ‘nge’ kutoka kifundo cha kijalizo hadi sehemu ya kifundo cha kikundi tenzi katika kishazi sharti. Kitambulishi sharti ‘Nge’ huchopekwa baina ya kiambishi kipatanishi ngeli na kiambishi kitambulishi cha njeo ya wakati uliopita ‘li’.

Sentensi (69) ya hapo juu huweza kugeuzwa kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo geuzi. Katika ugeuzi huo kishazi sharti husogezwa na kuwekwa katika nafasi iliyo kushoto mwa kishazi kikuu. Kishazi sharti kinatangulizwa huku kishazi kikuu kikitokea baada ya kishazi sharti. Hali hii inadhihirishwa na kielelezo tungo kifuatacho.

70




(Kama) shule inge(li)jengwa watoto wange(li)soma.

Kielelezo tungo (70), kinadhihirisha kuwa kishazi sharti kinachotambulishwa na ‘nge’ au ‘ngeli’ kina uhuru wa kuhama na kutokeza katika sehemu kabla ya kishazi kikuu au kutokeza baada ya kishazi kikuu. Uhamisho huo tunaweza kuuita utangulizaji wa kishazi sharti. Tunatambua kuwa wakati wa mchakato wa kuigeuza sentensi ya hapo juu kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo geuzi, kitambulishi cha njeo ya wakati uliopita (li) huweza kutokea katika muundo geuzi au kutotokea. Hali hii hufanyika kihiari. Kitambulishi hicho cha njeo kinapotokea katika muundo geuzi, huungwa pamoja

na mofu ‘nge’ na kuunda umbo ‘ngeli’, ambalo hutumika kutolea masharti. Ikiwa kitambulishi njeo ‘li’ hakitokei katika muundo geuzi, basi kunakuwa na umbo ‘nge’ pekee lisiloambatanishwa na kitambulishi (li) cha njeo ya wakati uliopita. Hali hii hutokea kwa sababu katika muktadha wa sentensi sharti, ‘nge’ hutumiwa katika njeo ya wakati uliopita peke yake. Kiambishi kitambulishi cha njeo ya wakati uliopita (li) huweza kudondoshwa na kuacha jukumu la kutambulisha njeo kutekelezwa na ‘nge’. Hali hii hupelekea ‘nge’ kutekeleza jukumu la kutambulisha sharti hali kadhalika lile la kutambulisha njeo ya wakati uliopita.

## 2.4.0 HITIMISHO

Katika sura hii ya pili tumetoa fasili ya sentensi sharti ya Kiswahili. Tumeeleza umbo la sentensi sharti ya Kiswahili kwa mujibu wa mpangilio wa viambajengo vikuu vinavyotumika kuiumba aina hii ya sentensi. Tumevitambua viambajengo vikuu vya sentensi sharti ya Kiswahili ambavyo ni pamoja na kishazi shurutiwa, kishazi elezi cha sharti, kitambulishi cha kishazi sharti na kiunganishi kiambatishi cha kitambulishi cha kishazi sharti katika lugha ya Kiswahili. Tumefafanua jinsi ya kukitambua kishazi sharti kutegemea na aina ya kitambulishi sharti kilichotumiwa katika sentensi husika. Matumizi ya sentensi sharti ya Kiswahili yameelezewa katika sura hii. Vitambulishi sharti katika lugha ya Kiswahili vimetambuliwa na matumizi yao kuelezewa. Vitambulishi sharti hivyo ni pamoja na 'kama, ikiwa, endapo, iwapo, ki, nga, ngali, nge na ngeli. Tumeona kuwa vitambulishi sharti 'nga, ngali, nge na ngeli' hutumiwa kutolea masharti katika njeo ya wakati uliopita peke yake. Maumbo haya manne hutumiwa kimpishano huru bila kubadili maana. Kitambulishi sharti 'ki' hutumiwa kutolea masharti katika njeo ya wakati ujao pekee. Hivyo vingine ambavyo ni 'kama, ikiwa, endapo, na iwapo' hutumiwa katika njeo zote za nyakati kutolea masharti katika Kiswahili. Tumefafanua muundo wa sentensi sharti ya Kiswahili na mageuzi yanayotekelezwa wakati wa kuigeuza sentensi sharti kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo geuzi. Muundo msingi wa sentensi sharti ya Kiswahili huanza kwa kishazi shurutiwa kikifuatwa na kishazi sharti. Hii ni kinyume na muundo geuzi ambapo kishazi shurutiwa hukifuata kishazi sharti katika mpangilio wa viambajengo vya sentensi sharti. Muundo geuzi hutokea wakati kishazi sharti kinasogezwa na kutiwa sehemu kabla ya kishazi shurutiwa.

# SURA YA TATU

## 3.0.0 UMBO, MAANA NA MATUMIZI YA SENTENSI SHARTI YA EKEGUSII.

### Utangulizi

Sura hii inatoa utangulizi wa sentensi sharti ya Ekegusii kwa njia ya kueleza fasili yake, maelezo kwa ufupi kuhusu majukumu kisemantiki ya vishazi na vipashio vingine vinavyoijenga aina hii ya sentensi. Tunalenga kutoa maelezo kuhusu kishazi sharti ambacho ni kiambajengo cha lazima katika sentensi sharti . Tunaeleza ni vipashio vipi vinavyokiunda kishazi sharti na ni jinsi gani vishazi tofauti vinaunganishwa ili kuunda sentensi sharti ya Ekegusii.

## 3.1.0 SENTENSI SHARTI YA EKEGUSII.

Sentensi sharti ya Ekegusii ni aina ya sentensi inayojumuisha vishazi viwili au zaidi vinavyowasilisha hali za mambo hivi kwamba kutokea kwa hali ya jambo moja kunaweka sharti dhidi ya kutokea hali ya jambo lingine. Hii inamaanisha kuwa hali inayoelezewa na mojawapo wa vishazi, huweka masharti dhidi ya kutokea kwa hali nyingine inayoelezewa na kishazi kile kingine katika sentensi hiyo. Kishazi kile kinachoelezea sharti lililowekwa dhidi ya hali fulani ndicho kinaitwa kishazi sharti. Kishazi kile kinachoelezea hali iliyowekewa sharti ndicho kishazi shurutiwa. Tungependa basi kuchunguza vishazi husika kama viambajengo vya sentensi sharti ya Ekegusii.

### 3.1.1 KISHAZI SHARTI CHA EKEGUSII

Kishazi sharti cha Ekegusii hupatikana katika kategoria ya kielezi katika sentensi. Ni kishazi chenye uamilifu wa kielezi katika muundo wa sentensi. Kishazi hiki hutumika kama kipashio kielezi kinachofafanua kishazi shurutiwa kwa kutaja sharti linalotawala tukio linaloelezewa na kishazi shurutiwa. Vielezi huainishwa katika makundi madogo madogo kutegemea ni nini vinavyotumiwa kufafanua. Kuna vielezi vinavyofafanua sehemu ya kishazi kama vile kitenzi, kivumishi au kielezi kingine. Aidha kuna miundo ya vielezi ambavyo hufafanua kishazi kizima. Hivi huwa ni vishazi vinavyovifafanua vishazi vingine kwa kutekeleza majukumu miongoni mwao yakiwa yale ya kuelezea ukweli, hali au namna, kutoa mapendekezo yaliyo kinyume na kile kinachotarajiwa kutokana na ukweli wa hali ya mambo, au kutoa masharti ambayo kwayo matukio fulani hutekelezwa. Kishazi elezi kilicho na uamilifu wa kutoa sharti ndicho tunachoshughulika nacho katika uchunguzi huu.

Kishazi sharti cha Ekegusii hueleza sharti kwayo tukio fulani huweza kutekelezeka. Kishazi hicho hutaja hali fulani ambayo lazima iwepo ili jambo fulani liweze kufanyika. Udadisi wa muundo wa sentensi za hapa chini zilizo na kishazi sharti utatufaa kuelewa wazo hili.

1. EK: Onye gwakoorire emeremo yago rirorio timoka.

   KS: Kama umemaliza kazi yako basi pumzika.

2. EK: Omoremi naasimeke onye embura kegotwa.

KS: Mkulima atapanda kama mvua itanyesha.

3. EK: Onye omogeni kagoika rirorio embori nenyenywe.

KS: Kama mgeni atafika basi mbuzi atachinjwa.

Kwa kutumia mfano wa sentensi ya tatu, tungependa kutoa ufafanuzi kuhusu kishazi sharti cha Ekegusii. Katika muundo wa sentensi (3) kuna vishazi viwili ambavyo ni (4) na (5) inavyoonyeshwa hapa chini.

4. EK: Onye omogeni kagoika.

KS: Kama mgeni atafika.

5. EK: Rirorio embori nenyenywe.

KS: Basi mbuzi atachinjwa.

Baina ya vishazi hivi viwili, (4) ni kishazi sharti ilhali (5) ni kishazi cha pendekezo au wazo kuu (kishazi kikuu). Kutokana na vishazi hivi viwili tunaelewa kuwa ili tukio linaolezewa na (5) kutendeka ni lazima sharti ambalo linatajwa katika (4) litendeke ndiposa la (5). Kutokana na mfano wa (3), kishazi sharti cha Ekegusii ni aina ya kiambajengo elezi ambacho hutekeleza jukumu la kufafanua kishazi shurutiwa kizima kilichokibeba hicho kishazi sharti. Mara tu kiunganishi tegemezi ‘onye’ ambacho hutanguliza kishazi sharti cha Ekegusii kinapoingizwa katika kishazi, huhitaji kuwa

kishazi hicho kiunganishwe na kishazi kingine (kishazi shurutiwa) ili kuifanya taarifa iwe kamilifu na sahihi.

Kishazi elezi cha sharti cha Ekegusii kinaweza kuwa upande wa kulia au kushoto mwa kishazi kikuu tunapozingatia mfuatano wa viambajengo katika sentensi. Wakati kishazi elezi cha sharti kinawekwa upande wa kushoto mwa kishazi shurutiwa, vishazi hivi viwili huunganishwa pamoja kwa matumizi ya kiunganishi tegemezi ‘rirorio’. Hiki kiunganishi si cha lazima katika hali hii. Hii ni kwa sababu, badala yake alama ya uakifishi ya koma (,) inaweza kupachikwa baina ya vishazi hivi viwili ili kuviunganisha. Sentensi mbili zifuatazo zinabainisha hali hizo.

6. (a) EK: Onye omogeni kagoika rirorio embori nenyenywe.

KS: Kama mgeni atafika basi mbuzi atachinjwa.

(b) EK: Onye omogeni kagoika, embori nenyenywe.

KS: Kama mgeni atafika, mbuzi atachinjwa.

Kishazi elezi cha sharti kinapowekwa upande wa kulia wa kishazi kikuu, kitangulizi cha sharti ‘onye’ au vitangulizi vingine kama tutakavyovitambua baadaye, hutumika kuviunganisha vishazi hivi.

7. EK: Embori nenyenywe onye omogeni kagoika.

KS: Mbuzi atachinjwa kama mgeni atafika.

Sentensi (7) inaweza kugawa katika vishazi viwili pamoja na kitangulizi cha sentensi sharti ‘onye’.

8. (a) EK: Embori nenyenywe

KS: Mbuzi atachinjwa

(b) EK: Omogeni kagoika

KS: Mgeni akifika

Kitangulizi cha sharti ‘onye’ kinachopekwa katika kishazi (8b) ili kukibainisha kama kishazi kielezi cha sharti inavyodhihirisha katika (8c).

8. (c) EK: Onye omogeni kagoika.
KS: Kama mgeni atafika.

Jukumu la kisemantiki la kishazi sharti (8c) ni kutaja sharti ambalo chini yake tukio linalowasilishwa na kishazi (8a) ambacho ni kishazi kikuu cha (6a) linaweza kutekelezwa.

### 3.2.0 KITAMBULISHI SHARTI CHA EKEGUSII

Katika lugha ya Ekegusii, vipashio vifuatavyo hutumiwa kutambulisha kishazi sharti cha lugha hiyo.

(i) onye

(ii) -ise

(iii) k-

(iv) -are

(v) ebe

### 3.2.1 KITAMBULISHI SHARTI ‘ONYE’ CHA EKEGUSII

Kipashio ‘onye’ hutumiwa kutambulisha kishazi sharti. Kitambulishi hiki hutumiwa kama inavyoonyeshwa katika mifano ifuatayo.

9. (a) EK: Onye Omari onyorete chibesa, rirorio nagorete omogondo.

KS: Kama omari alipata pesa basi alinunua shamba.

(b) EK: Omari nagorete omogondo onye onyorete chibesa.

KS: Omari alinunua shamba kama alipata pesa.

(c) EK: Onye Omari gakonyora chibesa rirorio nagore omogondo.

KS: Kama Omari atapata pesa basi atanunua shamba.

(d) EK: Omari nagore omogondo onye gakonyora chibesa.

KS: Omari atanunua shamba kama atapata pesa.

Katika sentensi (9a), kishazi 'Onye Omari onyorete chibesa' ndicho kishazi sharti. Kipashio 'onye' kimetiwa mwanzoni mwa 'Omari onyorete chibesa' ili kukitambua kishazi hicho kuwa ni maelezo ya sharti. 'Nagorete omogondo' ni kishazi shurutiwa katika sentensi hii.

### 3.2.2 KITAMBULISHI SHARTI '-ISE' CHA EKEGUSII

Mofu '-ise' huunganishwa na visabiki vya viambishi ngeli na nafsi ili kukitambulisha kishazi sharti cha Ekegusii. Kitambulishi hiki cha kishazi sharti hutumiwa katika njeo ya wakati ujao pekee. Mifano ifuatayo inatuonyesha jinsi '-ise' inavyotumiwa kutambulisha kishazi sharti cha Ekegusii.

10. (a) EK: Aye noogore omogondo oise konyora chibesa.

KS: Wewe utanunua shamba endapo utapata pesa.

(b) EK: Omogeni aise goika rirorio embori nenyenywe.

KS: Mgeni endapo atafika basi mbuzi atachinjwa.

(c) EK: Embura eise gotwa rirorio omoremi nasimeke.

KS: Mvua ikiwa itanyesha basi mkulima atapanda.

### 3.2.3 KITAMBULISHI SHARTI ‘K-’ CHA EKEGUSII

Mofu ‘k-’ huweza kuunganishwa na irabu a, e, i na o kutegemea ngeli ya nomino au nafsi ili kuwasilisha sharti katika Ekegusii. Mofu hiyo huunganshwa na vokali hizo ili kurejelea nomino inayohusishwa na kitenzi fulani ili kutoa sharti katika kishazi. Tuitazame mifano ifuatayo.

11. (a) EK: <u>Ka</u>aranyore chibesa rirorio Omari nagore omogondo.

    KS: Kama atapata pesa basi Omari atanunua shamba.

    (b) EK: <u>Ke</u>enyomba eraagachwe rirorio mbanganye.

    KS: Kama nyumba itajengwa basi watahama.

    (c) EK: <u>Ki</u>torache rirorio ntomonyore.

    KS: Kama tutakuja basi tutampata.

    (d) EK: <u>Ko</u>oraruge rirorio noragere.

    KS: Kama utapika basi utakula.

Katika kila sentensi (11a hadi d), kishazi kilichotangulizwa ni kishazi sharti huku kile cha pili kikiwa kishazi shurutiwa. Mofu ‘k-’ imeunganishwa na vokali mbalimbali kutegemea vipatanishi vya ngeli na nafsi ili kutambulisha kishazi sharti. Kishazi sharti kinachotambulishwa na ‘k-’ kinaweza kuwa katika sehemu ya kwanza au ya pili ya

sentensi. Sentensi (11a hadi d) zina vishazi sharti vilivyo mwanzoni mwa sentensi. Tutazame hivi vilivyo katika sehemu ya pili ya sentensi.

12. a). EK: Omari nagore omogondo <u>ka</u>aranyore chibesa.

KS: Omari atanunua shamba kama atapata pesa.

b). EK: Imbang'anye enyomba <u>ke</u>raagachwe.

KS: Watahama kama nyumba itajengwa.

c). EK: Intomorore <u>ki</u>torache.

KS: Tutamuona kama tutakuja.

d). EK: Noragere <u>ko</u>oraruge.

KS: Utakula kama utapika.

### 3.2.4 KITAMBULISHI SHARTI '-ARE' CHA EKEGUSII

Mofu '-are' ya Ekegusii ni mzizi wa kitenzi ambacho tunaweza kukitafsiri hapa kama mzizi '–wa' katika Kiswahili. Mzizi '-are' huweza kuunganishwa na vipatanishi vya ngeli na nafsi katika nyakati za njeo ya wakati uliopita. Toni huweza kutumiwa kubainisha vitenzi vya wakati mrefu uliopita na wakati mfupi uliopita. Oichoe (2005), anaeleza kuwa, toni ya kupanda {'} ikiwekwa katika kiambishi ngeli kilichounganishwa

na '-are', huweza kubainisha wakati mrefu uliopita. Toni ya kushuka {̀} katika hali hiyo itabainisha wakati mfupi uliopita. Hebu tuchungunze mifano ifuatayo:

13. a). EK: Nkorika báaré.

KS: Walikuwa wakiandika.

b). EK: Nkorika bàaré.

KS: Walikuwa wakiandika.

Sentensi ya (13a) inatubainishia kuwa waliandika muda mrefu uliopita. Toni ya kupanda imetiwa katika irabu 'a' ya silabi 'ba' ambayo ni kisabiki cha nafsi ya tatu, katika wingi. Sentensi ya (13b) inatoa maana kuwa walikuwa wakiandika muda mfupi uliopita ukilinganishwa na ule muda wa (13a). Toni ya kushuka imetiwa katika irabu 'a' ya silabi 'ba' ili kubainisha hali hiyo. Kwa kutumia toni pamoja na mofu '-are', sharti huweza kuwasilishwa katika Ekegusii. Mofu hiyo '-are' pamoja na toni huweza kutambulisha sharti katika njeo ya wakati uliopita. Toni huweza kubainisha sentensi sharti iliyo katika njeo ya wakati mrefu uliopita na ile ya wakati mfupi uliopita. Mifano ifuatayo inafafanua hali hii.

14. (a). EK: Omari áaré konyora chibesa rirorio nkogora áaré omogondo.

KS: Omari angalipata pesa basi angalinunua shamba.

(b). EK: Omari àaré konyora chibesa rirorio nkogora àaré omogondo.

KS: Omari angalipata pesa basi angalinunua shamba.

Sentensi (14a) inadhihirisha sharti lililotolewa katika wakati uliopita, muda mrefu. Sentensi ya (14b) nayo inalitoa sharti hilo hilo lakini wakati muda mfupi uliopita ukilinganishwa na ule wa sentensi (14a). Katika sentensi (14a) kuna toni ya kupanda katika irabu ya silabi ya mwanzo ya kikundi tenzi ‘aare’. Hivyo sharti lipo katika muda mrefu uliopita. Sentensi ya (14b), toni ya kushuka imetiwa katika irabu ya silabi ya kwanza ya kikundi tenzi kicho hicho na kudhihirisha kuwa sharti limetolewa katika kitenzi kilicho katika muda mfupi uliopita. Tungependa kusema kuwa -are hutumiwa pamoja na toni kutoa sharti katika njeo za nyakati hizo mbili zilizotajwa. Kutokana na mifano tuliyoitoa, inaonyesha kuwa ‘-are’ hujitokeza katika vishazi viwili vya sentensi sharti ya Ekegusii. Inajitokeza katika kishazi sharti na vile vile katika kishazi shurutiwa.

### 3.2.5 KITAMBULISHI SHARTI ‘EBE’ CHA EKEGUSII

Umbo ‘ebe’ hutumiwa kutolea masharti katika lugha ya Ekegusii. Umbo hili hutumiwa katika njeo zote za nyakati kutolea masharti. Umbo ‘ebe’ hutumiwa kukitambulisha kishazi sharti katika Ekegusii kama inavyoonyeshwa katika sentensi zifuatazo.

15 EK: Ebe omokori emeremo nakorete emeremo buya, namentetwe chibesa. (wakati uliopita).

KS: Ikiwa mfanyikazi alifanya kazi vizuri, aliongezwa pesa.

16 EK: Ebe omokori emeremo nakore emeremo buya, namentwe chibesa. (wakati ujao)

KS: Endapo mfanyikazi atafanya kazi vizuri, ataongezwa pesa.

Kila moja ya sentensi za hapo juu ina vishazi viwili. Sentensi ya (15) ina vishazi vifuatavyo;

(i) Ebe omokori emeremo nakorete emeremo buya.

(ii) (Omokori emeremo) namententwe chibesa.

Kishazi 'Ebe omokori emeremo nakorete emeremo buya' ndicho kishazi sharti. Kishazi '(omokori emeremo) namentetwe chibesa' ndicho kishazi shurutiwa. Maana katika sentensi (15) ya hapo juu ni kuwa kitendo cha kuongezewa pesa kilitegemea kitendo cha kufanya kazi vizuri. Hivyo basi ikiwa mhusika alifanya kazi vizuri, basi aliongezewa pesa. Lakini ikiwa hakufanya kazi vizuri, basi hakuongezewa pesa. Sharti ni kuwa mfanyi kazi alitumainiwa kutimiza kitendo cha kufanya kazi vizuri ili kitendo cha kuongezewa pesa kiweze kutekelezwa.

Sentensi (15) hapo juu inaweza kuwasilishwa kwa kutumia njeo ya wakati uliopo kama inavyofuata.

EK: Ebe omokori emeremo kagokora emeremo buya, aakomentwa chibesa.

KS: Endapo mfanyikazi anafanya kazi vizuri, anaongezwa pesa.

### 3.3.0 MUUNDO WA SENTENSI SHARTI YA EKEGUSII

Katika sehemu hii tunachunguza jinsi mageuzi katika sentensi sharti ya Ekegusii unavyotekelezwa kutokana na kanuni za kitengo geuza maumbo cha sarufi. Tumejaribu kutoa ufafanuzi wa muundo wa sentensi sharti ya Ekegusii kwa kutumia kanuni muundo virai za kitengo msingi.

Aidha katika sehemu hii tunatambua baadhi ya viambajengo ambavyo vinaweza kugeuzwa au kusogezwa kwa kuzingatia kanuni za ugeuza maumbo. Nadharia ya upanuzi wa sarufi sawazishi ina msimamo kuwa sentensi zina muundo wa kiviwango au kitabaka ambao huunda seti za kategoria za viambajengo. Kategoria hizo huwa zimetambuliwa kwa maneno fulani. Muundoviambajengo wa sentensi sharti ya Ekegusii unaweza kuwasilishwa kwa matumizi ya kielelezo tungo au kwa matumizi ya sentensi za mabano. Kielelezo tungo ni mchoro unaowasilisha seti ya kanuni zinazounda sentensi ambazo hujumuisha kanuni muundo virai za aina ya x-bar.

Tumekwishafafanua kuwa kishazi sharti cha Ekegusii ni kishazi elezi. Hata hivyo, katika uchunguzi huu, hatutakichanganua kishazi hicho kama kielezi. Badala yake tumekichanganua kama $\overline{S}$,yaani kishazi kinachotangulizwa kwa kijalizo. Hii ni kwa kuwa kishazi sharti cha Ekegusii ni kishazi bebwa kinachotegemezwa kwa kishazi shurutiwa.

Vipashio vyote vinavyotumika kutanguliza kishazi sharti katika lugha ya Ekegusii ambavyo ni ‘onye, -ise,-are, k- na ebe’, tutavichanganua kama vijalizo. Hii ni kwa sababu kila kimojawapo kinabainisha hicho kishazi sharti na tena kinatokea katika nafasi ya kijalizo katika sentensi. Uchanganuzi huu tumeukopa kutoka kwa Chomsky (1981) ambako kuna madai kuwa kuna kanuni ya muundo virai katika Kingereza (na katika kila lugha iliyo na vijalizo) inayokubali aina ya vijalizo kubainishwa katika muundo msingi. Kanuni hii ni kama inavyoonyeshwa hapa chini.

$\overline{S} \rightarrow$ KIJ – S

Alama KIJ inawakilisha kifundo cha muundo msingi (au kibunda cha sifa) ambacho kinatawala kijalizo, Bresnan (1970:300).

Uchanganuzi huu unachukulia kuwa sentensi inajumuisha kiambajengo kijalizo na sehemu pendekezo (wazo kuu) S. Tungependa kutaja hapa kuwa tunaenda kutumia kanuni miundo virai za aina ya nadharia ya x-bar. Aidha tutatumia $\overline{S}$ kama kifundo kinachotawala kishazi sharti cha Ekegusii.

### 3.3.1 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘ONYE’

Tulitaja hapo awali kuwa kitambulishi cha kishazi sharti cha ‘onye’ cha Ekegusii kinaweza kutumiwa katika njeo zote. Mifano ifuatayo itatusaidia kuelewa muundo msingi wa sentensi sharti ikiwa katika njeo ya wakati uliopita na vili vile wakati ujao.

17. EK: Onye onyorete chibesa rirorio Omari nagorete omogondo.

    KS: Kama alipata pesa basi Omari alinunua shamba.

Sentensi (17) iko katika kiwango cha muundo geuzi, katika wakati uliopita. Sentensi hiyo inaweza kuwasilishwa katika kiwango cha muundo msingi kama inavyoonyeshwa katika sentensi inayofuata.

18. $[_{S_1}$ Omari$_{KN}$ $[_{KT}$ nagorete omogondo $]]$ $[_{\overline{S}}$ onye $[_{S_2}$ onyorete chibesa $]]]]$

Katika (18) kuna vishazi viwili ambavyo ni $S_1$ and $S_2$

i. Omari nagorete omogondo ($S_1$)


ii. Omari onyorete chibesa. ($S_2$)

kishazi $S_2$ kimebebwa katika kishazi $S_1$kwa matumizi ya kiunganishi tegemezi 'onye'. Kiunganishi hiki kina jukumu maalum la kutambulisha kishazi sharti. $S_1$ ndicho kishazi kikuu ilhali $S_2$ ndicho kishazi bebwa. Kipashio 'onye' kinabainisha kishazi $S_2$. Kipashio hiki kinatiwa chini ya kijalizo ili kishazi 'onyorete chibesa' kijitokeze kama $\overline{S}$ inavyodhihirishwa katika (19).

19. (c) Onye onyorete chibesa.

Sentensi (18) ambayo ni muundo msingi wa (17) inaweza kuwasilishwa katika kielelezo tungo kinachofuata.

20.





EK: Omari nagorete omogondo onye onyorete chibesa.

KS: Omari alinunua shamba kama alipata pesa.

Kutokana na kielelezo tungo (20), inatubainikia kuwa kama tulivyotaja hapo mbeleni, sentensi sharti ya Ekegusii ina vishazi viwili. Vishazi hivyo ni $S_1$ na $\overline{S}$ katika kielelezo tungo cha hapo juu. Kishazi kikuu ni kile ambacho viambajengo vyake ni KN na KT kinachotawaliwa na $S_1$. Kishazi bebwa nacho ni kile kilicho na viambajengo KIJ. na $S_2$ na ambacho kinatawaliwa na $\overline{S}$. Kishazi $\overline{S}$ kinaweza kusogezwa kutoka mahali kilipo na

kutiwa sehemu iliyo kushoto mwa kishazi kikuu. Baada ya kutua huko, sentensi hiyo itakuwa na muundo ufuatao. Muundo huo ni muundo geuzi wa (20) au uwasilishi wa (17).

21.




EK: Onye Omari onyorete chibesa (rirorio) nagorete omogondo.


KS: Kama Omari alipata (basi) alinunua shamba.

Kielelezo tungo (21) ni muundo geuzi wa (18). Muundo huu umezaliwa kutokana na kanuni ya usogezi ambayo ni husogeza kishazi elezi cha sharti hadi sehemu ya kushoto mwa kishazi shurutiwa. Baada ya usogezi huu kufanywa, kiunganishi tegemezi ‘rirorio’ kinachochewa kutokea na kuchopekwa ambapo kinakitegemeza kishazi sharti kwa

kishazi kikuu. Kiunganishi tegemezi ‘rirorio’ si cha lazima katika muundo huu. Kinajitokeza  na kuchopekwa kwa hiari. Huwa kinachochewa kutokea kutokana na kutangulizwa kwa kishazi elezi cha sharti. Kipashio hiki hujitokeza katika kiwango cha muundo geuzi peke yake wala hakijitokezi katika kiwango kile cha muundo msingi. Kipashio ‘rirorio’ kinajitokeza katika muundo geuzi wakati kishazi sharti kinawekwa kabla ya kishazi kikuu, yaani kishazi shurutishwa kama inavyodhihirishwa katika sentensi inayofuata.

22. [$_{S_1}$ Omari (KN) [nagorete omogondo (KT)] [$_{\bar{S}}$ onye [$_{S_2}$ onyorete chibesa]]]]

Kutokana na usogezi uliofanywa katika (21), inabainika kuwa kiambajengo kilichosogezwa ni kishazi elezi cha sharti kwa ujumla wake. Kishazi hicho kimesogezwa kutoka nafasi iliyo baada ya kishazi shurutiwa hadi nafasi mbele au kabla ya kishazi shurutiwa inavyoonyeshwa katika sentensi inayofuata.

23 


Baada ya usogezi huo kutekelezwa, tunakuwa na muundo kama huu uliopo (24)

24. Onye onyorete chibesa rirorio Omari nagorete omogondo ____

$S_1$ $\bar{S}$ $S_2$

Katika vielezo (23 na 24), tunaona kuwa kishazi sharti kinachotambulishwa na 'onye' kimesogezwa jinsi inavyoonyeshwa na mishale. Hali hii inachochea kuchipuka na kuchopekwa kwa 'rirorio' ambacho ni kiunganishi kiambatanishi kisicho cha lazima. Kisha kipashio hicho 'rirorio' huunganisha kwa kukitegemeza kile kishazi sharti kwa kishazi kikuu. Usogezi huu tunaweza kuuita utangulizaji wa kishazi sharti. Usogezi huu hukihamisha kishazi elezi kutoka sehemu yake ya chini hadi juu katika kielelezo tungo ilivyoshuhudiwa katika (21).

Usogezi huu unaonyesha jinsi vishazi elezi vya sharti vinaweza kuhama hama. Hivyo basi kwa kuwa kishazi sharti cha Ekegusii ni kishazi elezi, kina uhuru kutokea katika sehemu ya kabla ya kishazi kikuu au baada ya kishazi kikuu katika msingi wa mpangilio kimlalo wa viambajengo.

### 3.3.2 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI '-ISE'

Sentensi sharti iliyo na kitambulishi cha kishazi sharti -ise katika Ekegusii hutumiwa katika wakati ujao pekee. Hebu tutazame mfano ufuatao:

25. EK: Aise gosoma rirorio Mokua nanyore emeremo.

KS: Endapo atasoma basi Mokua atapata kazi.

Sentensi ya (25) iko katika kiwango cha muundo geuzi. Sentensi hiyo inaweza kuwasilishwa katika kiwango cha muundo msingi kwa kutumia sentensi ya mabano kama inavyoonyeshwa katika kielelezo kinachofuata.

26.


EK : [ [ Mokua ]$_{KN}$ [ nanyore emeremo [ aise [ gosoma. ]$_{S_2}$ ]$_{\bar{S}}$ ]$_{KT}$ ]$_{S_1}$

KS : Mokua atapata kazi endapo atasoma.

Sentensi (26) ni sawa na sentensi (25) ila tu kuwa kishazi sharti katika (25) kimetangulizwa huku kishazi hicho kikiwa cha pili katika sentensi (26). Tulivyoeleza awali ni kuwa sentensi inayoanza na kishazi kikuu huchukuliwa kuwa ndiyo ya kimsingi kuliko ile inayoanza kwa kishazi sharti. Katika muktadha huu, ‘Mokua nanyore emeremo’ ndicho kishazi kikuu na hivyo kuifanya sentensi (26) kuwa msingi (muundo msingi) wa sentensi ya (25). Tumeeleza kuwa sentensi (25 na 26) zipo katika njeo ya wakati ujao. Hii inamaanisha kuwa kuna matumaini kuwa Mokua atasoma na hivyo kupata kazi. Sentensi yenyewe ni sharti halisi. Kupata kazi kwa Mokua kunategemea kusoma kwake.

Tukirejelea sentensi (26) ambayo ni muundo msingi wa (25) inabainika kuwa sentensi hii ina vishazi viwili. Vishazi hivyo ni $S_1$ na $S_2$. Kishazi $S_2$ kimetegemezwa katika kishazi $S_1$ kwa matumizi ya kiunganishi tegemezi ‘-ise’ kilichoambishwa kwa kuongezewa kisabiki cha nafsi ya kwanza umoja ‘a’. Kiunganishi hiki kina jukumu la kutambulisha kishazi sharti licha ya lile la kuviunganisha vishazi husika. Muundo msingi wa (25) waweza kuwasilishwa katika kielelezo tungo (27)

27.





EK: Mokua nanyore emeremo (Mokua) aise gosoma.

KS: Mokua atapata kazi endapo atasoma.

Kielelezo tungo cha (27) hapo juu kina vishazi viwili ambavyo ni $S_1$ na $\overline{S}$ Kishazi kikuu ni kile kinachotawaliwa na $S_1$ ambacho kina viambajengo KN, na KT. Kishazi bebwa ni kile kinachotawaliwa na $\overline{S}$ ambacho kina viambajengo KIJ. na $S_2$.

Kishazi 'aise gosoma' ambacho ni kielezi cha sharti kinaweza kusogezwa hadi sehemu ya kushoto mwa kishazi shurutiwa. Kutokana na uhamisho huo, muundo ufuatao utajitokeza.

28.




EK: Aise gosoma (rirorio) Mokua nanyore emeremo.

KS: Endapo atasoma (basi) Mokua atapata kazi.

Kielelezo tungo (28) kinawasilisha sentensi iliyo katika kiwango cha muundo geuzi. Kielelezo tungo hicho kinazaliwa kutokana na kanuni inayokitanguliza kishazi elezi cha sharti. Kishazi hicho kimehamishwa hadi sehemu iliyo mbele au kabla ya kishazi kikuu na hapo kuchochea kuchipuka na kuchopekwa kwa ‘rirorio’ ambayo inaunganisha kishazi elezi cha sharti kwa kishazi kikuu.

Kiunganishi ‘rirorio’ kinadhihirika tu katika muundo geuzi wakati kishazi sharti kinawekwa mbele ya kishazi shurutiwa. Wakati kishazi sharti kinatokea baada ya kishazi shurutishwa, basi ‘rirorio’ haihitajiki na kwa hivyo kukosa katika mpangilio wa


viambajengo vya sentensi sharti. Hii ni kwa kuwa '-ise' inafanya kazi ya kuunganisha licha ya kutumiwa kukitambulisha kishazi inavyoonyeshwa katika sentensi inayofuata.

29. EK: [$_{S_1}$ Mokua nanyore emeremo [$_{\bar{S}}$ aise [$_{S_2}$ gosoma. ]]]

KS: Mokua atapata kazi endapo atasoma.


Kutokana na uhamisho uliofanywa katika (28), tunaona kuwa viambajengo vilivyosogezwa ni kishazi elezi cha sharti kizima na virai nomino. Virai nomino hivyo vinajumuisha yambwa na yambwa tendewa. Tutazame mfano (30 na 31).

30.




Baada ya usogezi wa hapo juu kukamilika tunapata muundo kama huu unaofuata.

31.




Kishazi elezi cha sharti kinasogezwa kama jinsi mshale unavyoelekeza na kuchochea kuchipuka na kuchopekwa kwa kipashio 'rirorio' ambacho si cha lazima. Halafu

kiunganishi ‘rirorio’ huunganisha kishazi elezi cha sharti kwa kishazi kikuu (kishazi shurutiwa). Huu ni usogezi ambao unatanguliza kishazi elezi cha sharti kutoka sehemu yake kilimokuwa katika muundo msingi hadi sehemu iliyo mbele ya kishazi shurutiwa kama vile imedhihirishwa katika kielelelezo tungo (31).

Ugeuzi huu unaitwa utangulizaji wa kishazi sharti kwa kuwa kishazi sharti kilichosogezwa hutua mbele ya au kabla ya kishazi kikuu. Kishazi sharti hiki kinachotambulishwa na ‘-ise’ kina uhuru kama kile kinachotambulishwa na ‘onye’, kuhama hama na kujitokeza katika sehemu kabla ya au baada ya kishazi shurutiwa.

### 3.3.3 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘K-’

Mofu ‘k-’ huweza kuunganishwa na vokali a, e, i au o kutegemea ngeli ya nomino husika au nafsi ili kutumiwa kutambulisha sharti katika Ekegusii.

Mifano ifuatayo ni miundo geuzi inayotusaidia kuonyesha jinsi sentensi zilizo na kitambulishi sharti ‘k-’ zinavyoundwa kutegemea ngeli za nomino au nafsi. Mifano ni kama inavyofuata.

32. (a) EK: Kaaranyore chibesa Omari nagore omogondo.

KS: Kama atapata pesa basi Omari atanunua shamba.

(b) EK: Keenyomba eraagachwe rirorio mbang’anye.

KS: Kama nyumba itajengwa basi watahama.

(c) EK: Kibarache rirorio mbamonyore.

EK: Kama watakuja basi watampata.

(d) EK: Koomote oragechwe rirorio chinko nchitoke.

KS: Kama mti utakatwa basi kuni zitapatikana.

Sentensi (32a hadi d) tulivyosema ziko katika kiwango cha muundo geuzi. Mofu ‘k-’ imeunganishwa na vokali mbalimbali kuleta upatanifu sahihi kutegemea ngeli na nafsi. Katika kila sentensi ya hapo juu, kishazi sharti kimetangulia kikifuatwa na kishazi kikuu. Sentensi za hapo juu zinaweza kuwasilishwa katika kiwango cha muundo msingi inavyodhihirishwa katika (33a hadi d).

33.

a) EK: $[_{S_1}$ Omari [nagore omogondo $[_{\bar{S}}$ ka $[_{S_2}$ aranyore chibesa. $]]]]$

KS: Omari atanunua shamba kama atapata pesa.

b) EK: $[_{S_1}$ Mbang’anye $[_{\bar{S}}$ ke $[_{S_2}$ enyomba eraagachwe. $]]]$

KS: Watahama kama nyumba itajengwa.

c) EK: $[_{S_1}$ Mbamonyore $[_{\bar{S}}$ ki $[_{S_2}$ barache. $]]$

KS: Watampata kama watakuja.

d) EK: [Chinko nchitoke [ko [omote oragechwe.]]]
$S_1$ $\bar{S}$ $S_2$

KS: Kuni zitapatikana kama mti utakatwa.


Kwa kutumia sentensi (33d) kama kiwakilishi cha muundo wa sentensi (33a hadi d) tunaweza kuwasilisha muundo msingi wa sentensi sharti ya Ekegusii iliyo na kitambulishi cha sharti 'k-'. Kwanza ufuatao ni muundo msingi wa sentensi hiyo unaowasilishwa kwa matumizi ya sentensi ya mabano (34).

34. EK: [Chinko nchitoke [ko [omote oragechwe]]]
$S_1$ $\bar{S}$ $S_2$

KS: Kuni zitapatikana kama mti utakatwa.

Muundo msingi wa (34) unaweza kuwasilishwa katika kielelezo tungo (35) kifuatacho.

35.





EK: Chinko nchitoke koomote oragechwe.

KS: Kuni zitapatikana kama mti utakatwa.

Kielelezo tungo cha (35) kinadhihirisha viambajengo vya sentensi sharti ya Ekegusii iliyo na kitambulishi sharti 'k-' katika kiwango cha muundo msingi. Kielelezo tungo hicho kina vishazi viwili ambavyo ni $S_1$ na $\overline{S}$. Kishazi kinachotawaliwa na $S_1$ ndicho kishazi kikuu ilhali kishazi kinachotawaliwa na $\overline{S}$ ni kishazi tegemezi. Hiki ndicho kishazi elezi cha sharti. Kifundo cha kijalizo huzalisha kijalizo 'k-' katika muundo msingi. Baadaye kishazi hicho huhamishwa hadi nafasi fulani mahususi katika kikundi tenzi cha kishazi

elezi cha sharti. Nafasi yenyewe kinapohamia ni ile iliyo baada ya kikundi nomino na kabla ya kiambishi kipatanishi cha nafsi. Kifundo $\overline{S}$ ambacho ni kiambajengo cha $S_1$ kinaweza kusogezwa hadi sehemu iliyo kushoto mwa kishazi kikuu. Baada ya usogezi huo, muundo unaofuata huibuka.

36.




EK: Koomote oragechwe (rirorio) chinko nchitoke.

KS: Endapo mti utakatwa (basi) kuni zitapatikana.

Kielelezo tungo cha hapo juu ni muundo geuzi unaotokana na kanuni ya usogezi inayokitanguliza kishazi elezi cha sharti katika sehemu iliyo kabla ya kishazi kikuu. Baadaye kunachochewa kutokea na kuchopekwa kwa ‘rirorio’ (basi) ambacho ni kiunganishi kinachokitegemeza kishazi sharti kwa kishazi kikuu. Hata hivyo, ‘rirorio’ ni kiunganishi ambatani cha ‘k-’ ambacho si cha lazima. Kuchipuka kwake kunachochewa

na kule kutangulizwa kwa kishazi elezi cha sharti. Kipashio hiki 'rirorio' kinatambuliwa tu katika kiwango cha muundo geuzi wakati kishazi sharti kinawekwa kabla ya kishazi kikuu, ambacho ni kishazi shurutishwa kama ilivyoonyeshwa katika kielelezo tungo cha hapo juu. Ikiwa kishazi sharti kitatokea baada ya kishazi shurutishwa, basi kiunganishi 'rirorio' hakitahitajika. Hali hii inathibitishwa na muundo wa sentensi ifuatayo.

37. EK: [ $_{S_1}$ Chinko nchitoke ] [ $_{\bar{S}}$ ko [ $_{S_2}$ omote oragechwe. ] ]

KS: Kuni zitapatikana kama mti utakatwa.

Katika sentensi sharti ya hapo juu, kiunganishi 'rirorio' hakihitajiki na hivyo kinakosa katika mpangilio wa viambajengo vya sentensi hiyo. Hali hii inatokea kutokana na sababu kuwa kipashio 'k-' kinatekeleza jukumu la kuviunganisha vishazi viwili husika, licha ya kutekeleza jukumu muhimu la kutambulisha kishazi sharti.

Tukikirejelea kielelezo tungo (36), tunaona kuwa kuna usogezi fulani uliofanywa. Usogezi huu ni ule wa kukihamisha kishazi kielezi cha sharti kutoka sehemu ya pili ya sentensi kilipokuwa katika muundo msingi hadi sehemu ya kwanza au upande wa kushoto wa kishazi kikuu kilipo sasa katika kiwango cha muundo geuzi. Tukumbuke kuwa kishazi hiki kina kikundi nomino na kikundi tenzi kama viambajengo vyake. Kwa hivyo katika uhamisho huo viambajengo hivyo huweza kuhamishwa vikiwa ni vijenzi vya kishazi sharti. Uhamisho huo ni kama unavyoonyeshwa katika kielelezo tungo (38) kinachofuata.

38. [ ___ Chinko nchitoke [ ko [ omote oragechwe. ]]]
$S_1$ $\bar{S}$ $S_2$

Usogezi na kuchipuka kwa 'rirorio'

Katika kielelezo tungo (38), kishazi elezi cha sharti kinatokea baada ya kishazi kikuu. Baada ya usogezi huo kama unavyoashiriwa na mishale hapo juu kufanyika, tunakuwa na muundo ufuatao wa sentensi.

39.

[ Ko [ omote oragechwe ] (rirorio) chinko [ nchitoke. ___ ]]]

Kishazi elezi cha sharti kinasogezwa kama inavyoonyeshwa na mishale katika vielelezo tungo vya hapo juu. Hali hii inachochea kuchipuliwa kwa 'rirorio' ambacho ni kiunganishi kisicho cha lazima. Kiunganishi hiki huweza kukiunganisha kishazi elezi cha sharti na kishazi kikuu katika sehemu ya kushoto mwa kishazi kikuu. Usogezi huu tunaurejelea kama utangulizaji wa kishazi elezi. Usogezi huu hukitoa kishazi elezi katoka sehemu ya baada kishazi kikuu katika kiwango cha muundo msingi na kukisogeza hadi sehemu ya kabla ya kishazi kikuu katika kiwango cha muundo geuzi. Usogezi huu unatubainishia kuwa kishazi elezi cha sharti kilicho na kitambulishi 'k-' kina uwezo na uhuru wa kuhamahama na kujitokeza ama kabla ya, au baada ya kishazi shurutiwa.

### 3.3.4 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI '-ARE'

Tulikwisha taja kuwa kitambulishi kishazi sharti '-are' cha Ekegusii kinatumiwa katika njeo ya wakati uliopita. Ama kinaweza kutumiwa kutambulisha kishazi sharti katika wakati mrefu uliopita au wakati muda mfupi uliopita. Maendelezo ya sentensi zilizo katika nyakati hizi mbili huwa sawa lakini huweza kutofautishwa kimaana kwa matumizi ya toni. Toni ya kupanda hutiwa katika irabu ya kiambishi kipatanishi cha ngeli au nafsi kilichounganishwa na mzizi wa kitenzi '-are' ili kuelezea tukio la muda mrefu uliopita. Kwa upande mwingine, toni ya kushuka hutiwa katika irabu ya kiambishi kipatanishi cha ngeli au nafsi kilichounganishwa na mzizi wa kitenzi '-are' ili kuelezea tukio la muda mfupi uliopita. Mifano ifuatayo itatudhihirishia hali hizo.

40. EK: Omari áaré konyora chibesa rirorio nkogora áaré omogondo.

    KS: Omari angalipata pesa basi angalinunua shamba.

Sentensi ya (40) imeandikwa katika njeo ya wakati mrefu uliopita. Katika kikundi tenzi áaré, toni ya kupanda imetiwa katika irabu ya kwanza ambayo ni kiambishi kipatanishi cha nafsi ya kwanza katika umoja. Kikundi tenzi áaré kinajitokeza mara mbili katika sentensi hiyo. Kinajitokeza katika kishazi shurutiwa na vile vile katika kishazi elezi cha sharti. Muundo huu wa sentensi ni kama ule wa sentensi sharti ya Kiswahili iliyo na kitambulishi kishazi sharti 'nga' au 'nge' ambavyo pia hujitokeza katika vishazi viwili vya sentensi sharti. Sentensi ya (40) inaweza kugeuzwa na kuwasilishwa katika njeo ya muda mfupi uliopita kama inavyoonyeshwa katika (41).

41. EK: Omari àaré konyora chibesa rirorio nkogora àaré omogondo.
KS: Omari angalipata pesa basi angalinunua shamba.

Sentensi ya (41) imeandikwa katika njeo ya wakati uliopita, muda mfupi uliopita. Maendelezo ni sawa na sentensi (40). Kimuundo sentensi hizi zinafanana. Tofauti inasababishwa na toni kwa kuwa toni ya kushuka imetiwa katika irabu ‘a’ ya kwanza ya kikundi tenzi ‘aare’ hivyo kuashiria tukio kutokea muda mfupi uliopita. Irabu hiyo iliyotiwa toni ni kiambishi kipatanishi cha nafsi ya kwanza, katika hali ya umoja. Kiothografia tunaona kuwa sentensi (40) na (41) zinaendelezwa sawa na muundo wao ni mmoja. Tofauti inasababishwa katika kiwango cha maana kutokana na matumizi ya toni. Matumzi haya ya toni yanazitofautisha sentensi hizi katika kiwango kimoja tu. Kiwango hiki ni kile cha wakati wa tukio. Sentensi ya (40) ina maelezo ya sharti lililotolewa katika wakati muda mrefu uliopita ilhali ya (41) ina sharti lililotolewa katika muda mfupi uliopita. Hata hivyo inabainika kuwa viambajengo na muundo wa sentensi hizi mbili ni sawa. Kutokana na ukweli huu, tungo zinazofuata zinawakilisha miundo ya aina mbili za sentensi tulizozitambua hapo juu.

Sentensi (40) na (41) ni sentensi sharti za Ekegusii zilizowasilishwa katika kiwango cha muundo geuzi. Sentensi hizo zinaweza kuwasilishwa katika kiwango cha muundo msingi kama zinavyodhihirishwa katika sentensi (42) iliyotumia mabano.


42. EK: [Nkogora aare [omogondo [Omari [aare [konyora chibesa.]]]]]
$_{S}$ $_{KT}$ $_{KN}$ $_{KN}$ $_{\overline{S}}$ $_{KT}$

KS: Angalinunua shamba Omari angalipata pesa.

Sentensi (42) ni wasilisho la muundo msingi wa sentensi (40 na 41). Sentensi (42) ina vishazi viwili. Kishazi S ndicho kishazi kikuu. Kishazi $\overline{S}$ kimetegemezwa katika kishazi

kikuu. Kishazi hiki ndicho kishazi elezi cha sharti. Muundo msingi wa sentensi (40 na 41) unaweza kuwasilishwa kwa matumizi ya kielelezo tungo (43) kinachofuata.

43.




EK: Nkogora aare omogondo Omari aare konyora chibesa.


KS: Angalinunua shamba Omari angalipata pesa.

Kielelezo tungo (43) kinatudhihirishia kuwa sentensi sharti ya Ekegusii iliyo na kitambulishi kishazi sharti '-are' ina vishazi viwili ambavyo ni kishazi shurutiwa pamoja na kishazi elezi cha sharti. Katika kielelezo tungo hiki, $S_1$ ndicho kishazi kikuu ilhali $\bar{\mathbf{S}}$

ndicho kishazi elezi cha sharti. Kishazi hiki kielezi cha sharti kimetegemezwa katika kishazi kikuu. Kishazi $\bar{S}$ kina uhuru wa kusogezwa kutoka mahali kilipo na kuhamia sehemu iliyo mbele au kushoto mwa kishazi kikuu.

Baada ya usogezi huo kukamilika, muundo ufuatao ambao upo katika kiwango cha muundo geuzi huweza kuzaalika. Hebu tutazame kielelezo tungo (44) kinachouwasilisha muundo huo.

44.




EK: Omari aare konyora chibesa (ririorio) nkogora aare omogondo.

KS: Omari angalipata pesa (basi) angalinunua shamba.

Kielelzo tungo (44) kinatupatia muundo geuzi wa sentensi (42). Muundo geuzi huu umezaliwa kutokana na kanuni ya usogezi ambayo inakisogeza kishazi elezi cha sharti wakati kipo katika kiwango cha muundo msingi hadi sehemu ya kushoto mwa kishazi

kikuu hivyo kuibuliwa kwa muundo geuzi. Usogezi huu unapofanywa, ugeuzi unaochochea kuchipuka kwa kiunganishi tegemezi ‘rirorio’ hufanyika. Kiunganishi hiki hujitokeza na kuchopekwa baina ya vishazi viwili husika. Kama katika sentensi sharti zingine za Ekegusii, kiunganishi tegemezi ‘rirorio’ kinachopatikana katika sentensi sharti iliyo na kitambulishi cha kishazi sharti ‘-are’, si cha lazima. Kiunganishi tegemezi hiki hutumiwa katika aina hii ya sentensi sharti kwa hiari. Kiunganishi hiki huchochewa kutokea kutokana na kutangulizwa kwa kishazi sharti kama ionyeshwavyo katika (44). Matumizi yake yanatambulika katika muundo geuzi pekee. Ikiwa kishazi elezi cha sharti kitatokea baada ya kishazi kikuu (kishazi shurutishwa), basi kiunganishi tegemezi ‘rirorio’ katika muktadha huu hakihitajiki na hakijitokezi. Hii inadhihirishwa na mfano wa sentensi (45).


45 EK: [ Omari nkogora aare omogondo aare [ [ konyora chibesa. ] ] ]
$S_1$ S $S_2$
KS: Omari angalinunua shamba angalipata pesa.

Katika sentensi (45), kiunganishi ‘rirorio’ hakihitajiki na hivyo kinakosa katika mpangilio huo. Hii ni kwa kuwa kipashio ‘-are’ kinatekeleza jukumu la kuunganisha vishazi viwili husika licha ya kutekeleza wajibu wa kukitambulisha kishazi elezi cha sharti.

Tukikirejelea kielelezo tungo (45), tunaona kuwa usogezi uliofanyika ni ule wa kukihamisha kishazi elezi kizima cha sharti. kishazi hicho kina viambajengo vyake ambavyo ni pamoja na kirai nomino na kirai tenzi. Katika usogezi huo, viliweza navyo kuhamishwa kama viambajengo vya kishazi elezi cha sharti. Katika wasilisho la (46)


lifuatalo, kunadhihirishwa nafasi ambayo kishazi elezi cha sharti kilipohamishwa na vile vile nafasi kilipohamia wakati wa usogezi huo.

46.




Katika (46), mishale inaonyesha mwelekeo wa usogezi wa kishazi elezi cha sharti. Kishazi hicho kinasogezwa kwa kuhamia sehemu iliyo mbele ya kishazi shurutiwa inayotambuliwa kwa alama(-). Baada ya usogezi kufanyika, muundo unaowasilishwa katika (47) huibuka.

47.




Kishazi elezi cha sharti 'Omari are konyora chibesa' kinasogezwa jinsi inavyoonyeshwa na mishale na kuchochea kuchipuka kwa kiunganishi 'rirorio' ambacho kinakiunganisha kishazi elezi cha sharti katika upande wa kushoto wa kishazi kikuu yaani 'Omari nkogora are omogondo'. Usogezi huu tunaweza kuuita utangulizaji wa kishazi sharti.

Usogezi huu unakitoa kishazi elezi cha sharti kutoka sehemu yake kilimokuwa katika kiwango cha muundo msingi hadi sehemu iliyo mbele ya kishazi kikuu na kutupatia kielelezo tungo kama kile cha (47). Usogezi huu unabainisha uwezo wa kishazi elezi cha

Ekegusii kuhama hama. Kishazi sharti hiki kina uhuru wa kutokea katika sehemu kabla ya kishazi shurutiwa au baada ya kishazi shurutiwa.

### 3.3.5 MUUNDO WA SENTENSI YENYE KITAMBULISHI ‘EBE’

Kipashio ‘ebe’ ni kitambulishi sharti cha Ekegusii kilicho na matumizi sawa na kitambulishi sharti ‘onye’ cha Ekegusii. Kitambulishi sharti ‘ebe’ hutumiwa katika njeo ya wakati uliopita, uliopo na wakati ujao ili kutoa masharti katika lugha ya Ekegusii. Tungo ifuatayo ni sentensi sharti iliyo na kitambulishi cha sharti ‘ebe’.

48. EK: Ebe omorwaire ogwenire rirorio naarwe nyagitari.

    KS: Kama mgonjwa amepona basi ametoka hospitalini.

Sentensi ya (48) ina kishazi sharti na kishazi shurutiwa. Kishazi sharti hapa ni ‘Ebe omorwaire ogwenire’, ilhali kishazi shurutiwa ni ‘(omorwaire) naarwe nyagitari.’ Sentensi yenyewe ina maana kuwa ikiwa mgonjwa amepona, atatoka hospitalini. Kutoka kwa mgonjwa hospitalini kunategemea kupona kwa mgonjwa huyo. Hivyo basi ikiwa hajapona, mgonjwa huyo hatatoka hospitalini. Sharti linalohitajika kutimizwa kwanza ni kupona kwa mgonjwa ndipo kitendo cha kuondoka hospitalini kiweze kutekelezwa.

Sentensi (48) imewasilishwa katika kiwango cha muundo geuzi. Sentensi sharti hiyo inaweza kuwasilishwa katika kiwango cha muundo msingi kwa kutumia sentensi ya mabano inavyoonyeshwa katika kielelezo (49).

49. EK: [Omorwaire [naarwe nyagitari [ebe [omorwaire ogwenire.]]]]

KN KT $\overline{S}$ KN KT


$S_1$ $S_2$

KS: Mgonjwa atatoka hospitalini kama Mgonjwa amepona.

Sentensi (49) ina maana sawa na sentensi (48). Tofauti baina sentensi hizi mbili ni kuwa katika (48) kishazi sharti kimetangulizwa na kimetokea kabla ya kishazi shurutiwa. Katika sentensi (49), kishazi sharti kimetokea baada ya kishazi shurutiwa. Sentensi (49) ni muundo msingi wa sentensi (48). Hii ni kwa sababu (49) inaanza kwa kishazi kikuu. Sentensi inayoanza kwa kishazi kikuu (shurutiwa) hutambuliwa kuwa ndiyo ya kimsingi kuliko ile inayoanza kwa kishazi sharti. Katika hali hii, 'omorwaire narwe nyagitari' ndicho kishazi kikuu. Kishazi hiki kimetokea kabla ya kishazi sharti 'ebe omorwaire ogwenire.' Hali hii inaifanya sentensi (49) kuwa msingi (muundo msingi) wa sentensi (48). Sentensi sharti (49) ambayo ni muundo msingi wa (a) ina vishazi viwili. Vishazi hivyo ni $S_1$ na $S_2$. Kishazi $S_1$ ndicho kishazi shurutiwa. Kishazi sharti kimetegemezwa katika kishazi shurutiwa kwa matumizi ya kiunganishi tegemezi 'ebe'. Katika muktadha huu wa sentensi sharti, umbo 'ebe' linatekeleza majukumu mawili. Kwanza ni kuwa umbo hilo linatumika kutambulisha sharti. Pia umbo hili lina jukumu la kukitegemeza kishazi sharti kwa kishazi shurutiwa, ambacho hapa ndicho kishazi kikuu.

Sentensi (49) iliyo katika kiwango cha muundo msingi inaweza kuwasilishwa kwa matumizi ya kielelezo tungo (50).

50.





EK: Omorwaire narwe nyagitari ebe (omorwaire) ogwenire.

KS: Mgonjwa atatoka hospitalini kama (mgonjwa) amepona.

Kielezi tungo (50) hapo juu kina vishazi viwili. Vishazi hivyo ni $S_1$ na $\overline{S}$. Kishazi kikuu ni kile kinachotawaliwa na $S_1$, ambacho kina viambajengo KN na KT. Kishazi tegemezi ni kile kinachotawaliwa na $\overline{S}$ ambacho kina viambajengo KIJ na $S_2$. Hiki ndicho kishazi sharti.

Kishazi sharti ‘ebe omorwaire ogwenire’ kina uhuru wa kusogezwa hadi sehemu kushoto mwa kishazi kikuu. Kusogezwa huko kunapelekea kishazi sharti kutokea kabla ya kishazi shurutiwa. Baada ya kukamilika kwa uhamisho huo, matokeo yake ni muundo unaofuata.

51.




EK: Ebe omorwaire ogwenire rirorio naarwe nyagitari.

KS: Kama mgonjwa amepona basi ataondoka hospitalini.

Kielelezo tungo (51) ni uwasilisho wa sentensi sharti iliyo katika kiwango cha muundo geuzi. Kielelezo tungo hicho kimezaliwa kutokana na kanuni ya ugeuzi inayokisogeza na kukitanguliza kishazi elezi cha sharti. Kishazi hicho kimehamishwa na kutokea katika sehemu kushoto mwa, na kabla ya kishazi shurutiwa. Wakati wa uhamisho huo, kiunganishi tegemezi 'rirorio' kinachochewa kuchipuka na hatimaye kuchopekwa baina ya vishazi hivi viwili. Kiunganishi hiki kinakitegemeza kishazi sharti kwa kishazi kikuu. Katika muktadha wa sentensi sharti ya Ekegusii, kiunganishi 'rirorio' kinadhihirika tu katika muundo geuzi wakati kishazi sharti kinatangulizwa na kutokea kabla ya kishazi shurutiwa.


Ikiwa kishazi sharti kitatokea baada ya kishazi shurutiwa, basi kiunganishi ‘rirorio’ hakitahitajika na kwa hivyo kinakosa katika mpangilio wa viambajengo vya sentensi sharti. Hali hii ni kwa sababu umbo ‘ebe’ linafanya kazi ya kuviunganisha vishazi viwili husika na vile vile kutekeleza lile jukumu la kukitambulisha kishazi sharti. Wazo hili linathibitishwa kwa matumizi ya sentensi ya mabano inayofuata.

52. EK: [$_{S_1}$ Omorwaire naarwe nyagitari [$_{\bar{S}}$ ebe [$_{S_2}$ ogwenire. ]]]

KS: Mgonjwa atatoka hospitalini kama amepona.

Sentensi (52) inaonyesha kuwa kiunganishi kitegemezi ‘rirorio’ hakihitajiki ikiwa kishazi sharti kinatokea baada ya kishazi shurutiwa. Hali hii inaturejesha kwenye kielelezo tungo (51). Katika kielelezo tungo hiki, tunaona kuwa uhamisho wa viambajengo uliofanywa, ulihusisha kusogezwa kwa kishazi elezi cha sharti kizima. Hivyo inamaana kuwa hakuna kiambajengo cha kishazi elezi cha sharti kilichoachwa nyuma. Vielelezo vifuatavyo vinatudhihirishia mchakato wote wa ugeuzaji kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo geuzi.

53.




Usogezi na kuchipuka kwa ‘rirorio’

Kielezo cha hapo juu kinatubainishia kiambajengo cha kusogezwa na sehemu wazi ambapo kitahamia. Kiambajengo hiki kinachohamishwa ni kishazi sharti. Hivyo baada ya usogezi huo kufanywa na kukamilika, muundo ufuatao ambao upo katika kiwango cha muundo geuzi hupatikana.

54. [ _Ebe_ [ _ogwenire_ ] rirorio [ omorwaire naarwe nyagitari ___ ] ] ] ]

Mishale katika kielezo cha hapo juu inaelekeza mkondo wa usogezi unaofanywa na kishazi sharti. Wakati wa uhamisho huo, kiunganishi tegemezi ‘rirorio’ kinachochewa kuchipuka. Hatimaye kiunganishi hicho kinachopekwa baina ya kishazi sharti na kishazi shurutiwa. Kiunganishi hiki si cha lazima. Kina jukumu la kukitegemeza kishazi sharti kwa kishazi shurutiwa.

Kutokana na ufafanuzi huu, tunaona kuwa sentensi sharti ya Ekegusii ikiwa katika kiwango cha muundo msingi, kishazi sharti hutokea baada ya kishazi shurutiwa. Ugeuzi unapofanywa ili kuiwasilisha sentensi hiyo katika kiwango cha muundo geuzi, kanuni za ugeuzi huo hukitanguliza kishazi sharti na kuishia kutokea kabla ya kishazi shurutiwa. Usogezi huu ni utangulizaji wa kishazi sharti. Kwa ujumla, kishazi sharti kilicho na kitambulishi ‘ebe’ kina uhuru wa kuhamahama na kutokea ama kabla au baada ya kishazi shurutiwa.

### 3.4.0 HITIMISHO

Katika sura hii ya tatu tumetoa fasili ya sentensi sharti ya Ekegusii. Tumeeleza umbo la sentensi sharti ya Ekegusii kwa mujibu wa mpangilio wa viambajengo vikuu vinavyotumika kuiumba aina hii ya sentensi. Tumevitambua viambajengo vikuu vya sentensi sharti ya Ekegusii ambavyo ni pamoja na kishazi shurutiwa, kishazi elezi cha sharti, kitambulishi cha kishazi sharti na kiunganishi kiambatishi cha kitambulishi cha kishazi sharti katika lugha ya Ekegusii. Tumefafanua jinsi ya kukitambua kishazi sharti kutegemea na aina ya kitambulishi sharti kilichotumiwa katika sentensi husika.

Matumizi ya sentensi sharti ya Ekegusii yameelezewa katika sura hii. Vitambulishi sharti katika lugha ya Ekegusii vimetambuliwa na matumizi yao kuelezewa. Vitambulishi sharti hivyo ni pamoja na ‘onye, -ise, -are, k- na ebe’. Tumeona kuwa kitambulishi sharti ‘-are’ hutumiwa kutolea masharti katika njeo ya wakati uliopita peke yake. Aidha kitambulishi hiki hutokea katika kishazi sharti na vile vile katika kishazi shurutiwa. Kitambulishi sharti ‘-ise’ hutumiwa kutolea masharti katika njeo ya wakati ujao pekee. Hivyo vingine ambavyo ni ‘onye, k- na ebe’, hutumiwa katika njeo zote za nyakati kutolea masharti katika Ekegusii.

Tumefafanua muundo wa sentensi sharti ya Ekegusii na mageuzi yanayotekelezwa wakati wa kuigeuza sentensi sharti kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo geuzi. Muundo msingi wa sentensi sharti ya Ekegusii huanza kwa kishazi shurutiwa kikifuatwa na kishazi sharti. Hii ni kinyume na muundo geuzi ambapo kishazi shurutiwa hukifuata kishazi sharti kwa mujibu wa mpangilio wa viambajengo vya sentensi sharti.

Muundo geuzi hutokea wakati kishazi sharti kinasogezwa na kutiwa sehemu kabla ya kishazi shurutiwa.

Tumeonyesha jinsi kishazi sharti cha Ekegusii kilivyo na uhuru na uwezo wa kuhama hama hivyo kutokea kabla au baada ya kishazi kikuu. Tumeonyesha jinsi vitambulishi vya vishazi elezi vya sharti vinavyotekeleza jukumu la kutambulisha vishazi sharti na vilevile kuunganisha vishazi husika vya sentensi sharti. Aidha tumeonyesha jinsi kiunganishi kiambatishi 'rirorio' katika Ekegusii kinavyochochewa kuchipuka na kuchopekwa katika muundo geuzi wa sentensi sharti ya Ekegusii. Kiunganishi kiambatishi hiki hujitokeza tu katika kiwango cha muundo geuzi kutokana na utangulizaji wa kishazi elezi cha sharti. Mwisho tumeonyesha jinsi vitambulishi vya vishazi sharti katika Ekegusii vinavyojitokeza katika sehemu ya kijalizo kwa mujibu wa mpangilio wa viambajengo vya sentensi sharti ya Ekegusii.

# SURA YA NNE

## 4.0.0 ULINGANISHI WA SENTENSI SHARTI YA KISWAHILI NA EKEGUSII

### Utangulizi

Katika sura ya pili na ya tatu tumeshughulikia sintaksia ya sentensi sharti ya Kiswahili sanifu na Ekegusii mtawalia. Katika sura hii tunalinganisha sintaksia ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii. Ulinganishi huu unatekelezwa kwa kuzingatia vipashio vya masharti, miundo ya sentensi na ugeuzi katika lugha ya Kiswahili na ya Ekegusii. Ulinganishi huu ndio unabainisha ni vipengele vipi vinavyolingana na ni vipi vinavyotofautiana baina ya lugha hizi mbili katika muktadha wa sentensi sharti, na kwa mujibu wa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi tunayoitumia.

## 4.1.0 KAIDA YA NADHARIA YA UPANUZI WA SARUFI SAWAZISHI

Nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi inadai kuwa kiwango cha muundo ndani na kile cha muundo nje vyote huchangia kuwasilisha maana katika sentensi. Tunapochunguza lugha ya Kiswahili na Ekegusii, sentensi sharti inaweza kuwasilisha maana ama ikiwa katika kiwango cha muundo msingi au katika kiwango cha muundo geuzi. Mageuzi yanayotokea wakati wa kukitanguliza kishazi sharti na ambayo yanajitokeza katika muundo nje, hayapotoshi maana bali huwakilisha maana sawa na ile ya muundo msingi. Katika kiwango cha muundo msingi, kishazi shurutiwa hutangulia mwanzoni mwa sentensi, kikifuatwa na kishazi sharti. Kitambulishi sharti hukitegemeza

kishazi sharti kwa kishazi kikuu. Kitambulishi sharti hiki hutokea baina ya vishazi hivi viwili. Madai haya yanawasilishwa kwa matumizi ya sentensi zifuatazo.

1. Mjomba ataacha biashara kama atapata hasara.

Sentensi ya hapo juu inawasilishwa katika kiwango cha muundo msingi na ina maana kamilifu. Sentensi hiyo inaweza kugeuzwa hadi muundo geuzi na maana yake ikasalia kuwa ile ile. Ugeuzi huo unatekelezwa kwa mujibu wa sheria za ugeuza maumbo.

2. Kama mjomba atapata hasara (basi) ataacha biashara.

Sentensi (2) ina maana sawa na sentensi (1) ingawa zimewasilishwa katika viwango tofauti. Sharti linalotolewa katika sentensi (1) ndilo linalotolewa katika sentensi (2) na yanafanana. Hali hii katika Kiswahili inalingana na hali ya sentensi sharti ya Ekegusii. Tutazame mfano ufuatao.

3. EK: Tokomonyora onye gokonyorwa.
   KS: Hutampata kama utachelewa.

Sentensi (3) imewasilishwa katika kiwango cha muundo msingi na ina maana kamilifu. Sentensi hiyo yaweza kuwasilishwa katika kiwango cha muundo geuzi na maana ikasalia kuwa ile ile.

4 EK: Onye gokonyorwa (rirorio) tokomonyora.
  KS: Kama utachelewa (basi) hutampata.

Sentensi (4) imewasilishwa katika kiwango cha muundo geuzi, maana yake ni sawa na ile ya (3) iliyo katika kiwango cha muundo msingi. Kutokana na ufafanuzi huu, tunaona kuwa lugha ya Kiswahili na ya Ekegusii zinafanana katika kuitikia madai ya nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi. Madai haya ni kuwa kiwango cha muundo ndani na kile cha muundo nje, vyote huchangia kuwasilisha maana katika tungo. Mageuzi ambayo tumeyajadili yametekelezwa katika muundo nje na yanazua maana kamilifu.

Katika mifano ya hapo juu, kiunganishi kitegemezi 'basi' cha Kiswahili na 'rirorio' cha Ekegusii havipatikani katika muundo msingi kama tulivyofafanua katika sura ya pili na ya tatu mtawalia. Hata hivyo vinajitokeza katika kiwango cha muundo geuzi, ingawa kujitokeza kwao ni kwa hiari. Si vya lazima. Hata hivyo vinapojitokeza katika muundo geuzi, vinatekeleza jukumu la kukitegemeza kishazi sharti kwa kishazi shurutiwa. Huu ni mchango wa muundo nje kuwasilisha maana katika tungo katika lugha hizi mbili. Lugha hizi zinafanana kwa kauli hii kulingana na ufafanuzi ambao tumeutoa.

## 4.2.0 UAINISHAJI WA SENTENSI SHARTI YA KISWAHILI NA EKEGUSII

Sentensi sharti ya Kiswahili na ile ya Ekegusii zote ni sentensi changamano. TUKI (1990) inaeleza kuwa sentensi changamano ni aina ya sentensi yenye kishazi tegemezi kimoja au zaidi. Sentensi sharti ya Kiswahili na ile ya Ekegusii huundwa kwa vishazi viwili au zaidi. Vishazi vya lazima ni kishazi shurutiwa na kishazi sharti. Kishazi shurutiwa ndicho kishazi kikuu ilhali kishazi sharti ndicho kishazi tegemezi. Vishazi hivi kwa pamoja huunda sentensi sharti katika Kiswahili na Ekegusii ambazo zina muundo wa sentensi changamano. Sentensi sharti ya lugha hizi mbili ina muundo ambapo kishazi

sharti hakiwezi kujitokeza peke yake na kikawa na maana kamilifu. Lazima kishazi hicho kitegemezwe kwa kishazi shurutiwa ndipo maana kamilifu ipatikane katika tungo. Utegemezi huo hupelekea kujitokeza kwa sentensi iliyo na muundo wa sentensi changamano. Mfano ni katika tungo zinazofuata.

5 Mkitaka kuenda ughaibuni lazima mpate vyeti vya usafiri.

Sentensi (5) ya hapo juu ni sentensi sharti ya Kiswahili. Sentensi hii ina vishazi viwili ambavyo ni kishazi kikuu na kishazi sharti. ‘Lazima mpate vyeti vya usafiri’ ni kishazi kikuu. Hiki ni kishazi shurutiwa. ‘Mkitaka kuenda ughaibuni’ ni kishazi tegemezi. Hiki ndicho kishazi sharti. Muungano wa vishazi hivi viwili unaibua muundo wa sentensi changamano. Hali hii inashuhudiwa katika sentensi sharti ya Ekegusii inayoonyeshwa katika tungo inayofuata.

6 EK: Onye rigori ri’endagera rigokina, obogima oborakong’e.

KS: Kama bei ya chakula itapanda, maisha yatakuwa magumu.

Katika sentensi ya hapo juu, ‘obogima oborakong’e’ ni kishazi shurutiwa. Hiki ndicho kishazi kikuu. Kishazi sharti ni ‘onye rigori ri’endagera rigokina.’ Hiki ndicho kishazi tegemezi. Vishazi hivi kwa pamoja vinaunda sentensi sharti iliyo na muundo wa sentensi changamano. Kutokana na ufafanuzi huu, inadhihirika kuwa miuundo ya sentensi sharti ya Kiswahili na ya Ekegusii inafanana. Sentensi zote zina muundo wa sentensi changamano.

### 4.3.0 ULINGANISHI WA KISHAZI SHARTI CHA KISWAHILI NA EKEGUSII

Kishazi sharti cha Kiswahili na Ekegusii vinafanana. Vishazi hivi vinapatikana katika kategoria ya kielezi katika sentensi. Kishazi sharti cha Kiswahili na Ekegusii vina uamilifu wa kielezi katika muundo wa sentensi. Vinatumika kama vipashio vielezi vinavyovifafanua vishazi shurutiwa. Vinatekeleza jukumu hilo kwa kutaja sharti linalotawala tukio linaloelezewa na kishazi shurutiwa. Vishazi hivi hutoa maelezo ya hali au matendo ambayo lazima yatimizwe kwanza ndipo hali au matendo yanayotajwa na vishazi shurutiwa yaweze kutekelezwa.

Kishazi sharti cha Kiswahili na cha Ekegusii ni vishazi tegemezi. Haviwezi kujitokeza kivyao katika tungo bila kutegemezwa kwa kishazi kikuu. Vishazi hivi hutegemezwa kwa vishazi vikuu kwa mujibu wa vitambulishi vya masharti. Mfano wa kitambulishi sharti katika Kiswahili ni ‘kama, iwapo, endapo, ikiwa, ki, nga, ngali, nge na ngeli’. Katika Ekegusii ni ‘onye, ebe, -are, -ise, na k-.’ Vitambulishi hivi vya masharti hutekeleza jukumu la kuvitegemeza vishazi sharti kwa vishazi shurutiwa, licha ya kutekeleza jukumu la kimsingi la kukitambulisha kishazi sharti.

Kishazi elezi cha sharti cha Kiswahili na cha Ekegusii, vyote vinaweza kutokea katika upande wa kulia au kushoto mwa kishazi shurutiwa kwa mujibu wa mfuatano wa viambajengo katika sentensi sharti. Kwa hivyo kinaweza kukitangulia au kukifuata kishazi shurutiwa katika tungo. Kishazi elezi cha sharti cha Kiswahili na Ekegusii kinapotiwa kulia mwa kishazi shurutiwa au kukitangulia kishazi shurutiwa katika tungo, vitangulizi (vitambulishi) vya masharti hutumiwa kuviunganisha vishazi hivi. Mifano inayofuata inaonyesha kufanana huko.

7 Mfanyikazi hatalipwa kama ataendelea kugoma.

Sentensi sharti ya Kiswahili hapo juu ina vishazi viwili, ‘Mfanyikazi hatalipwa’ ni kishazi shurutiwa kilichotokea mwanzoni mwa tungo. Kishazi sharti ‘kama ataendelea kugoma kimetokea kulia mwa kishazi shurutiwa. kitambulishi sharti ‘kama’ kimetumiwa kuviunganisha vishazi hivi kwa kukitegemeza kishazi sharti kwa kishazi shurutiwa. Hali kama hii inashuhudiwa katika sentensi sharti ya Ekegusii inayofuata.

8. EK: Omwana takorara onye ng’ina taiyo.

KS: Mtoto hatalala ikiwa mama yake hayuko.

Katika sentensi ya hapo juu, ‘Omwana takorara’ ni kishazi shurutiwa na kimetokea mwanzoni mwa sentensi. ‘onye ng’ina taiyo’ ni kishazi elezi cha sharti kilichotokea kulia mwa kishazi shurutiwa. Vishazi hivi vimeunganishwa pamoja kwa matumizi ya kitambulishi hiki kinachoviunganisha vishazi hivi kwa kukitegemeza kishazi sharti ‘ngina taiyo’ kwa kishazi shurutiwa. Hivyo kinatekeleza jukumu la kuunganisha licha ya lile la kimsingi la kukitambulisha kishazi sharti.

Kishazi sharti cha Kiswahili na cha Ekegusii vina kufanana wakati kishazi sharti kinapotiwa upande wa kushoto mwa kishazi shurutiwa. Hali hii inapojitokeza huwa kishazi sharti kimetangulia katika tungo kikifuatwa na kishazi shurutiwa. Hali hii inapotokea, viunganishi vitegemezi ambavyo si vya lazima hutumiwa kuviunganisha vishazi viwili husika katika sentensi sharti ya lugha hizi mbili.

Katika sentensi sharti ya Kiswahili, kiunganishi kitegemezi (kiambatishi) hicho ni ‘basi’ ilhali katika sentensi sharti ya Ekegusii ni ‘rirorio’. Viunganishi vitegemezi hivi hutumiwa kihiari. Vinaweza kuwepo au visiwepo katika muundo geuzi wa sentensi sharti za lugha hizi mbili. Ikiwa kiunganishi ‘basi’ na ‘rirorio’ havitumiwi katika sentensi sharti ya lugha husika, alama ya uakifishi ya koma (,) hupachikwa baina ya kishazi sharti na kishazi shurutiwa. Alama hiyo huwakilisha mpumuo katika maongezi. Mifano ifuatayo inatuonyesha jinsi kishazi sharti cha Kiswahili na Ekegusii kinavyowasilishwa kikiwa kimetangulizwa au kimetiwa kushoto mwa kishazi shurutiwa.

9. Kama mfanyikazi ataendelea kugoma (basi) hatalipwa.

‘Kama mfanyikazi ataendelea kugoma’ ni kishazi kilicho upande wa kushoto mwa kishazi shurutiwa, ‘(mfanyikazi) hatalipwa.’ Vishazi hivi viwili vimeunganishwa kwa matumizi ya kiunganishi kitegemezi ‘basi’ ambacho si cha lazima. Kiunganishi hiki hutumiwa kihiari na hutokea tu wakati kishazi sharti kimetangulizwa. Kikiwa hakipo kama kiambajengo cha sentensi sharti ya hapo juu, alama ya uakifishaji (,) hutumiwa na kutupatia umbo la tungo lifuatalo.

10. Kama mfanyikazi ataendelea kugoma, hatalipwa.

Uwasilishi wa sentensi sharti ya Kiswahili wa hapo juu unafanana na wa sentensi sharti ya Ekegusii kama inavyofuata ambapo kiunganishi ‘rirorio’ kinatumiwa kama kiunganishi ‘basi’ cha Kiswahili.

11. EK: Onye ng'ina omwana taiyo (rirorio) omwana takorara.

KS: Ikiwa mama ya mtoto hayuko (basi) mtoto hatalala.

Kishazi sharti 'onye ng'ina omwana taiyo' kimetokea kushoto mwa kishazi shurutiwa, 'omwana takorara.' Vishazi hivi vimeunganishwa na kiunganishi kitegemezi 'rirorio' ambacho si cha lazima. Ikiwa kiunganishi hicho hakipo kama kiambajengo cha sentensi hiyo, alama (,) inatumiwa kama vile katika Kiswahili. Hivyo sentensi sharti ya Ekegusii inawasilishwa ifuatavyo bila kiunganishi 'rirorio'.

12. Onye ng'ina omwana taiyo, omwana takorara.

Kutokana na maelezo haya, inabainika kuwa kishazi sharti cha Kiswahili na cha Ekegusii vinafanana. Vishazi hivi vinatoa maelezo ambayo ni masharti yanayotolewa dhidi ya matendo au hali inayotajwa na vishazi shurutiwa. Katika lugha hizi mbili, kishazi sharti cha Kiswahili sawa na kile cha Ekegusii, vinaweza kutokea upande wa kushoto au kulia mwa kishazi shurutiwa. Hivyo vinaweza kuvitangulia au kuvifuata vishazi shurutiwa katika tungo. Vishazi sharti vinapovifuata vishazi shurutiwa katika lugha hizi zote, vitambulishi sharti hutekeleza jukumu la kuvitegemeza vishazi sharti kwa vishazi shurutiwa, licha ya kutekeleza jukumu la kuvitambulisha vishazi sharti.

Vishazi sharti vinapovitangulia vishazi shurutiwa au kutokea kushoto mwa vishazi shurutiwa kiunganishi kiambatishi 'basi' katika Kiswahili au 'rirorio' katika Ekegusii ambavyo si vya lazima, hutumiwa kuvitegemeza vishazi sharti kwa vishazi shurutiwa.

Ikiwa viunganishi vitegemezi hivyo havitumiwi, alama ya koma (,) hutumiwa baina ya vishazi hivyo viwili ambayo inawakilisha mpumuo katika mazungumzo.

## 4.4.0 ULINGANISHI WA VITAMBULISHI SHARTI VYA KISWAHILI NA EKEGUSII

Lugha ya Kiswahili na Ekegusii zina vipashio kadhaa ambavyo hutumiwa kutambulisha masharti katika sentensi na hivyo kuvibainisha vishazi vielezi vya masharti katika sentensi. Lugha ya Kiswahili ina jumla ya takribani vitambulishi sharti tisa ambavyo hutumiwa kutolea masharti katika lugha hii. Vipashio hivyo vinavyotambulisha masharti katika lugha ya Kiswahili ni kama vifuatavyo.

i. kama
ii. ikiwa
iii. endapo
iv. iwapo
v. ki
vi. nga
vii. ngali
viii. nge
ix. ngeli

Katika upande wa lugha ya Ekegusii, lugha hii ina jumla ya takribani vipashio vitano vinavyotumiwa kutolea masharti. Vipashio hivyo ni kama vifuatavyo.

i. onye
ii. k-
iii. -are
iv. -ise
v. ebe

Tunapochunguza idadi ya vitambulishi sharti vya Kiswahili na vya Ekegusii, tunagundua kuwa vile vya lugha ya Kiswahili ni vingi kuliko vya lugha ya Ekegusii. Lugha ya Kiswahili ina vitambulishi sharti tisa ilhali lugha ya Ekegusii ina vitambulishi sharti vitano. Kiulinganishi tunaafikia uamuzi kuwa kuna tofauti kuhusiana na kipengele cha idadi ya vitambulishi sharti baina ya sentensi sharti ya Kiswahili na ya Ekegusii. Vya Kiswahili ni vingi kuliko vya Ekegusii.

Lugha ya Kiswahili na Ekegusii zinafanana pia katika misingi ya mazingira ya matumizi ya vipashio vitambulishi masharti. Lugha hizi zina vitambulishi sharti vinavyotumiwa katika njeo ya wakati uliopita peke yake, wakati ujao peke yake na vingine vinavyotumiwa katika njeo zote za nyakati.

Katika lugha ya Kiswahili, maumbo ‘nga, ngali, nge na ngeli’ hutumiwa katika njeo ya wakati uliopita pekee kutolea masharti katika sentensi. Maumbo haya hutumika kimpishano huru hivi kwamba, umbo moja huweza kutumiwa badala ya umbo lingine bila kubadilisha maana. Kwa ujumla, maumbo haya manne yamekitwa katika kutolea masharti katika njeo ya wakati uliopita peke yake. Hayatumiki kutolea masharti katika njeo zingine kama vile wakati uliopo na ujao.

Kwa upande wa lugha ya Ekegusii, ni umbo moja tu lililokitwa katika kutoa masharti katika njeo ya wakati uliopita pekee. Umbo hili ni '-are'. Umbo hili halitumiwi kutolea masharti katika njeo ya wakati uliopo wala ujao. Kuhusiana na kipengee hiki, tofauti iliopo baina ya lugha hizi mbili ni kuwa, wakati lugha ya Kiswahili ina vitambulishi sharti vinne vilivyokitwa kutolea masharti katika njeo ya wakati uliopita pekee, lugha ya Ekegusii ina kitambulishi sharti kimoja tu kinachotumiwa katika hali hiyo.

Pili, inadhihirika kuwa mofu '-are' inatumiwa pamoja na sifa ya toni ambayo inabainisha masharti yaliyotolewa katika njeo ya wakati uliopita muda mrefu, na pia katika njeo ya wakati uliopita muda mfupi kama ilivyofafanuliwa katika sura ya tatu. Hali kama hii haipatikani katika lugha ya Kiswahili. Vipashio vya masharti 'nga, ngali, nge na ngeli' vinatumiwa katika njeo ya wakati uliopita iwe ni muda mrefu au mfupi uliopita na bila matumizi ya sifa ya toni.

Kuhusu vipashio vya masharti vilivyo na uamilifu wa kutoa masharti katika njeo ya wakati ujao pekee, lugha ya Kiswahili ina kitambulishi sharti 'ki' peke yake. Kitambulishi hiki hakitumiwi katika njeo ya wakati uliopita wala uliopo isipokuwa wakati ujao. Lugha ya Ekegusii nayo ina mofu '-ise' inayotumiwa kutolea masharti katika njeo ya wakati ujao peke yake. Kuhusiana na kipengele hiki, lugha ya Kiswahili inafanana na Ekegusii. Hii ni kwa kuwa lugha zote zina maumbo yanayotumiwa kutolea masharti kwa kujikita katika njeo ya wakati ujao peke yake. Pili, lugha ya Kiswahili ina umbo moja tu, sawa na lugha ya Ekegusii iliyo na umbo moja tu linalotumiwa kutolea masharti kwa kujikita tu katika njeo ya wakati ujao peke yake.

Katika lugha hizi mbili, kuna vipashio vya masharti vinavyotumiwa kutolea masharti katika njeo zote za nyakati. Hali hii inatunapatia kufanana kwa lugha ya Kiswahili na ile ya Ekegusii. Lugha ya Kiswahili ina vitambulishi sharti 'kama, ikiwa, endapo na iwapo' ambavyo hutumiwa kutolea masharti katika njeo zote. Hali hii ni sawa na ilivyo katika lugha ya Ekegusii iliyo na vitambulishi sharti 'onye, k- na ebe' vinavyotumiwa kutolea masharti katika njeo zote. Tofauti hapa ni kuwa lugha ya Kiswahili ina jumla ya vipashio vinne vya aina hii ilhali ya Ekegusii ina jumla ya vipashio vitatu vya aina hii.

### 4.4.1 MAUMBO YA VITAMBULISHI SHARTI

Kimaumbo, vitambulishi sharti vya Kiswahili na Ekegusii vinaweza kuainishwa katika makundi mawili. Makundi haya ni:-

(i) Vitambulishi sharti huru.
(ii) Vitambulishi sharti funge (tegemezi).

Lugha ya Kiswahili na Ekegusii zinafanana kwa kuwa zote zina vishazi sharti vinavyopatikana katika makundi haya mawili.

### 4.4.2 VITAMBULISHI SHARTI HURU

Vitambulishi sharti huru ni vile vitambulishi vilivyo na umbo lililokamilifu kama neno, na linalojitegemea kuwasilisha sharti bila kutaka kuongezewa mofu yoyote. Kwa hivyo,

kitambulishi sharti huru kina umbo la mofu huru. Mofu huru ni mofu iliyo na uwezo wa kukaa peke yake na kuleta maana. Mgullu (1999) anaeleza kuwa mofu huru ni mofu zilizo na uwezo wa kukaa peke yao na zikawa maneno kamili yenye maana inayoweza kueleweka bila kusaidiwa na mofu nyingine. Lugha ya Kiswahili na Ekegusii zina vitambulishi sharti vilivyo na umbo la mofu huru. Vitambulishi sharti hivi vina uwezo wa kukaa peke yao katika tungo na kuwasilisha maana bila kuunganishwa na mofu nyingine. Vitambulishi sharti hivi katika lugha ya Kiswahili ni pamoja na:- 'kama, endapo, ikiwa na iwapo'.

Vitambulishi sharti vya hapo juu havitegemei kuunganishwa na mofu yoyote ili kutokea na kuwasilisha maana kamilifu. Mifano ni kama ifuatavyo.

13. (a) Mtachelewa mkutanoni kama mtatembea pole pole.

(b) Yohana atamuoa Amina ikiwa anampenda.

(c) Idi ataajiriwa endapo atahitimu mahojiano.

(d) Wafanyikazi walirejea kazini iwapo walilipwa mishahara yao.

Katika lugha ya Ekegusii vitambulishi sharti vilivyo na umbo la mofu huru ni viwili. Navyo ni 'onye' na 'ebe'. Mifano ifuatayo inaonyesha jinsi vitambulishi sharti hivi vinavyojitokeza bila kusaidiwa na mofu nyingine katika kuwasilisha maana. Vinajitegemea inavyodhihirika hapa katika tungo zifuatazo.

14. (a) EK: Barangerie baragere onye endagera yarugirwe.
KS: Waite wale kama chakula kimepikwa.

(b) EK: Obogima bwaye mbobe obuya ebe otigire amarwa.
KS: Maisha yake yatakuwa mazuri endapo ameacha pombe.

Mifano ya hapo juu inaonyesha kufanana kwa maumbo ya vitambulishi sharti vya Kiswahili na Ekegusii vinavyojitokeza kama mofu huru. Kiidadi kuna kutofautiana kwa kuwa vile vya Kiswahili ni vingi kuliko vya Ekegusii. Vya Kiswahili ni vinne ilhali vya Ekegusii ni viwili.

### 4.4.3 VITAMBULISHI SHARTI FUNGE

Vitambulishi sharti funge (tegemezi) ni vitambulishi vilivyo na maumbo ambayo hayawezi kutokea pekee katika kuwasilisha masharti. Vitambulishi hivi huhitaji kuunganishwa na mofu zingine ili viweze kutumiwa kutoa masharti. Vitambulishi hivi vina umbo la mofu funge. Tuki (1990) wanaeleza kuwa mofu funge ni mofu ambayo haiwezi kukaa peke yake ikawa neno kamili. Mgullu (1999) anaeleza kuwa mofu funge ni lazima iwekwe pamoja na angalau mofu nyingine moja ndipo tupate neno kamili. Maana za mofu funge huwa zimefungwa kwenye muktadha maalum. Mofu funge inapoondolewa kwenye muktadha wake hukosa maana na ni vigumu kujua maana yake bila kuiweka katika muktadha wa neno.

Lugha ya Kiswahili na ya Ekegusii zina vitambulishi sharti ambavyo vina sifa za mofu funge. Vitambulishi sharti hivi huwa lazima viwekwe pamoja na mofu nyingine ili viweze kutumika kutambulisha sharti. Maana zao za kutambulisha sharti hueleweka zikiwa zimeambatanishwa na mofu nyingine katika muktadha wa sentensi sharti.

Katika muktadha wa sentensi sharti ya Kiswahili, vitambulishi hivi ni pamoja na ‘nga, ngali, nge, ngeli, na ki.’ Vitambulishi sharti hivi hujitokeza katika kikundi tenzi vikiwa

vimeambatanishwa na mofu za nafsi, viambishi vipatanishi vya ngeli na mizizi ya vitenzi. Mifano ni kama inavyoonyeshwa katika tungo zifuatazo.

15. (a) Tungatoka mjini mapema tungaepuka kunyeshewa mvua.

(b) Wangalijikaza kulima, wangalimaliza shamba lote.

(c) Mwanariadha angejiandaa vizuri, angenyakua nishani ya dhahabu.

(d) Nauli ingelipanda, abiria wangeliahirisha safari.

(e) Mwanafinzi akitaka kufaulu, sharti atie jitihada masomoni.

Mifano ya hapo juu inaonyesha kuwa vitambulishi sharti vilivyotumiwa katika sentensi sharti hizo haviwezi kukaa peke yao bila kuambatanishwa na mofu nyingine. Vinapatiwa maana kwa kuambatanishwa na mofu nyingine na kutumika katika muktadha wa sentensi sharti.

Katika lugha ya Ekegusii vitambulishi sharti vilivyo na umbo la mofu funge ni pamoja na '-are', -ise, na k-.' Vitambulishi sharti hivi vinajitokeza kama mofu funge ambazo haziwezi kujitokeza kama neno kamili pasipo na kuambatanishwa na mofu nyingine. Vitambulishi sharti hivi hutokea katika kikundi tenzi vikiwa vimeambatanishwa na viwakilishi nafsi, vipatanishi vya ngeli na mizizi ya vitenzi. Sentensi sharti zifuatazo zinaonyesha jinsi vitambulishi sharti hivyo vinavyotokea kwa kuambatanishwa na aina mbalimbali za mofu.

16 (a) EK: Abaremi baare gosimeka omotieni oeta nabo baare kunyora rigesa rigiya.

KS: Wakulima wangalipanda mwezi uliopita wangalipata mavuno mema.

(b) EK: Abanyagitari baise kogoma, abarwaire abange abarakwe.

KS: Endapo wauguzi watagoma, wagonjwa wengi watakufa.

(c) EK: Omonene oito kaarache ankio, ningotebie oche komorora.

KS: Mkubwa wetu akija kesho, nitakuambia uje kumwona.

Mifano ya maumbo ya vitambulishi sharti vya Ekegusii vya hapo juu inadhihirisha kuwa vitambulishi hivyo haviwezi kutokea peke yao katika tungo bila kuambatishwa na mofu nyingine. Hali hii ni sawa na ile ya vitambulishi 'nga, ngali, nge na ngeli' vya Kiswahili ambavyo lazima viambatishwe na mofu nyingine ndipo maana zao ziweze kueleweka katika muktadha wa sentensi sharti.

Tofauti inayojitokeza baina ya vitambulishi sharti funge vya Kiswahili na Ekegusii inajitokeza katika muundo wa vitambulishi sharti hivyo baada ya kuunganishwa na mofu zingine ili kuunda kikundi tenzi. Katika lugha ya Kiswahili, mofu za kitambulishi sharti funge zinajitokeza baina ya kiambishi kipatanishi cha ngeli au nafsi na mzizi wa kitenzi. Katika lugha ya Ekegusii, kitambulishi 'k-' kinatokea mwanzoni mwa kikundi tenzi kinachosetiri sharti. Kitambulishi sharti hicho hutokea mwanzoni kikifuatwa na kipatanishi cha ngeli au nafsi na kisha mzizi wa kitenzi. Kitambulishi '-ise' na '-are' hutokea baada ya kipatanishi cha ngeli au nafsi na kuunda umbo lililo kitenzi kisaidizi. Kitenzi hutokea kando kama umbo binafsi.

Tofauti nyingine inayoibuka katika kundi hili la vitambulishi sharti vyenye umbo la mofu funge ni kuwa idadi ya vitambulishi sharti vya aina hii katika Kiswahili ni vingi kuliko vya lugha ya Ekegusii. Katika Kiswahili ni vitano ilhali vya Ekegusii ni vitatu.

Kufikia hapa tumeona kuwa vitambulishi sharti vya Kiswahili na vya Ekegusii vinafanana na vile vile vinatofautiana kimaumbo, na vinajitokeza katika makundi mawili. Kuna vile vinavyotokea kama mofu huru na vile vilivyo na umbo la mofu tegemezi. Katika kila kundi la vitambulishi hivi, Kiswahili kina vitambulishi vingi kuliko Ekegusii.

## 4.5.0 ULINGANISHI WA MUUNDO WA SENTENSI SHARTI YA KISWAHILI NA EKEGUSII

Kutokana na ufafanuzi tulioufanya hapo awali kuhusu muundo msingi wa sentensi sharti ya Kiswahili na ile ya Ekegusii, inabainika kuwa sentensi hizi zina muundo msingi unaofanana kwa kiwango kikubwa. Sentensi sharti ya Kiswahili na ya Ekegusii zina muundo msingi ulio na kishazi shurutiwa kikiwa kimekitangulia kishazi sharti. Kishazi sharti hutokea baada ya kishazi shurutiwa au upande wa kulia mwa kishazi shurutiwa. Baada ya geuzi la utangulizaji wa kishazi sharti kutekelezwa, sentensi sharti za lugha hizi hutokea na muundo geuzi ulio na kishazi sharti kilichotokeza mwanzoni mwa tungo kikifuatwa na kishazi shurutiwa. Kutokana na geuzi hilo, vitambulishi huru katika lugha hizi hujitokeza mwanzoni kabisa mwa tungo geuzi. Katika muundo msingi, vitambulishi sharti huru hivyo hujitokeza baina ya vishazi husika viwili katika lugha hizi mbili.

### 4.5.1 SENTENSI ZENYE KITAMBULISHI KATIKA KISHAZI SHARTI NA SHURUTIWA

Tumekwisha tambua kuwa lugha ya Kiswahili ina maumbo ‘nga, ngali, nge na ngeli’ yanayotumiwa katika njeo ya wakati uliopita peke yake. Katika lugha ya Ekegusii kuna umbo moja tu lililokitwa kutolea masharti katika kutolea masharti katika njeo ya wakati uliopita peke yake. Umbo hilo ni ‘-are.’ Maumbo haya tuliyoyatambua hutokea katika kishazi sharti na vile vile katika kishazi shurutiwa katika tungo moja. Hii ni sifa inayopelekea sentensi ya Kiswahili na Ekegusii kufanana kimuundo.

Sentensi sharti ya Kiswahili iliyowasilishwa katika kiwango cha muundo msingi kwa kutumia umbo ‘nga, ngali, nge au ngeli, ina mpangalio wa vishazi ulio sawa na ule wa sentensi sharti ya Ekegusii yenye kitambulishi ‘-are.’ Miundo ya sentensi sharti katika lugha hizi zote zina kishazi sharti kinachotokea baada ya kishazi shurutiwa. Kwa hivyo, kishazi shurutiwa kinatangulia katika tungo kikifuatwa na kishazi sharti katika lugha hizi mbili.

Kufanana kwingine ni kuwa vitambulishi sharti hivi katika lugha hizi zote hujitokeza mara mbili katika sentensi sharti. Kitambulishi sharti kinatokea katika kishazi sharti na vile vile katika kishazi shurutiwa iwe ni katika Kiswahili au katika Ekegusii. Mifano ifuatayo inatusaidia kuelewa wazo hili. Tuanze na mfano katika lugha ya Kiswahili.

16. Wageni wangalijipikia kama mpishi angalichelewa kufika.

Katika sentensi hii, ‘Mpishi angalichelewa kufika’ ni kishazi sharti. Katika kishazi hiki, kitambulishi sharti ‘ngali’ kimetokea katika kikundi tenzi ‘angalichelewa.’ ‘Wageni wangalijipikia’ ni kishazi shurutiwa. Katika kishazi hiki, kipashio cha sharti ‘ngali’

kimetokea katika kikundi tenzi ‘wangalijipikia.’ Hebu tutazame mfano ufuatao wa sentensi sharti ya Ekegusii.

17. EK: Nkoeta ba<u>are</u> amatemu onye ngosoma ba<u>are</u> n’omokia.

KS: Wangalipita mitihani kama wangalisoma kwa bidii.

Katika sentensi hii ya Ekegusii, ‘Nkoeta baare amatemu’ ni kishazi shurutiwa. Mofu -are ambayo ni kitambulishi sharti imetokea katika kikundi tenzi ‘baare.’ ‘Ngosoma baare n’omokia’ ni kishazi sharti na ambapo kitambulishi sharti ‘-are’ kimejitokeza kwa mara ya pili. Hali hii ni sawa na ile katika Kiswahili ambapo umbo ‘ngali’ linajitokeza katika kishazi sharti na vile vile katika kishazi shurutiwa. Kitambulishi sharti ‘-are’ cha Ekegusii kinajitokeza katika kikundi tenzi ingawa kama kitenzi kisaidizi. Hii ni sawa na kitambulishi sharti ‘ngali’ kinachojitokeza katika kikundi tenzi.

Matumizi ya toni husababisha tofauti kubwa katika matumizi ya vitambulishi sharti hivi vya Kiswahili na Ekegusii. Lugha ya Kiswahili haina toni katika kutumiwa kwake. Lugha ya Ekegusii ina matumizi ya toni. Katika muktadha wa sentensi sharti, toni inaweza kutumiwa kubainisha sharti linalotolewa katika muda mrefu wa njeo ya wakati uliopita. Toni ya kupanda inatiwa katika irabu ya kiambishi kipatanishi cha ngeli au nafsi kilichounganishwa na mzizi wa kitenzi ‘-are’ ili kuelezea tukio la muda mrefu uliopita. Toni ya kushuka nayo hutiwa katika irabu ya kiambishi kipatanishi cha ngeli au nafsi kilichounganishwa na mzizi wa kitenzi ‘-are’ ili kuelezea tukio la muda mfupi uliopita. Mfano:

18. EK: Omoibi nigo áaré gotama kwáaré gokuura.

KS: Mwizi angalitoroka ungalipiga mayowe.

Sentensi ya hapo juu imeandikwa katika njeo ya wakati uliopita, muda mrefu. Hii ni kutokana na kutiwa toni ya kupanda katika irabu ‘a’ ya kikundi tenzi ‘áaré’ cha kishazi shurutiwa na kikundi tenzi ‘kwáaré’ cha kishazi sharti.

Toni ya kushuka ikitiwa katika irabu zilizotambuliwa katika vikundi tenzi vya hapo juu, sentensi itakuwa na maana ya vitenzi kutendeka katika njeo ya wakati uliopita lakini muda mfupi. Muda usio mrefu. Mfano ni kama ufuatavyo.


19. Omoibi nigo àaré gotama kwàaré gokuura.

Kutokana na ufafanuzi huu, ni dhahiri kuwa sentensi sharti ya Ekegusii huweza kutumia toni kutolea masharti katika njeo ya wakati mrefu uliopita na ile ya wakati mfupi uliopita. Toni hutiwa katika irabu za viambishi vipatanishi vya ngeli au nafsi vilivyounganishwa na mzizi ‘-are’ ili kuunda kikundi tenzi kisaidizi kinachosetiri sharti. Tumeshaeleza kuwa lugha ya Kiswahili haina sifa ya toni. Hata hivyo lugha hii huwa na mkazo kwenye silabi ya pili kutoka mwisho wa kila neno.

Kufanana kwingine kunakoshuhudiwa kuhusu sentensi sharti iliyo na vitambulishi sharti vinavyojitokeza mara mbili, ni kuwa vitambulishi sharti hivyo ‘nga, ngali, nge na ngeli’ vya Kiswahili na ‘-are’ cha Ekegusii, vyote vinazaliwa chini ya kifundo cha kijalizo katika kishazi sharti katika kiwango cha muundo msingi. Vitambulishi sharti hivi vya Kiswahili ambavyo ni vijalizo huweza kuhamishwa kutokana na kanuni ya usogezi kutoka kifundo hicho cha kijalizo hadi sehemu ya kikundi tenzi katika kishazi sharti. Kile cha Ekegusii ‘-are’, nacho huhamishwa kutokana na kanuni ya usogezi hadi chini ya


kifundo cha kikundi tenzi cha kishazi sharti ambapo kinatua chini ya kifundo cha kitenzi kisaidizi. Vielelezo tungo vinavyofuata vinatusaidia kuelewa mawazo hayo ili kubainisha kufanana huku.

20. Kiswahili.




Wageni wangalijipikia (kama) mpishi angalichelewa.

21. Ekegusii.




EK: Ching’iti echiáaré gosira amanani áaré gosarigwa.

KS: Wanyama wangetoweka misitu ingaliharibiwa.

### 4.5.2 MUUNDO WA SENTENSI ZENYE VITAMBULISHI KATIKA VISHAZI SHARTI PEKEE

Lugha ya Kiswahili na Ekegusii zina sentensi sharti zenye vitambulishi sharti vinavyotokea katika kishazi sharti pekee bila kutokea katika kishazi shurutiwa. Katika lugha ya Kiswahili vitambulishi sharti vinavyojitokeza katika kishazi sharti pekee ni 'kama, endapo, ikiwa, iwapo na ki'. Katika lugha ya Ekegusii, vitambulishi sharti vya aina hiyo ni 'onye, -ise, k- na ebe.' Maumbo haya ambayo tumeyatambua, hutokea mara moja tu katika sentensi. Hutokea katika kishazi sharti pekee iwe ni ya Kiswahili au ya Ekegusii.

Muundo msingi wa sentensi zenye vipashio vya masharti vinavyotokea katika kishazi sharti pekee katika lugha ya Kiswahili na Ekegusii, ina mpangilio ambao unavitanguliza vishazi shurutiwa, vikifuatwa na vishazi sharti. Vijalizo hivyo vyote vinavyotumiwa kutambua masharti katika tungo huzalishwa chini ya kifundo cha kijalizo katika kishazi sharti.

Sentensi sharti ya Kiswahili na Ekegusii ikiwa katika kiwango cha muundo msingi, vipashio hivyo vya masharti hutokea baina ya kishazi sharti na kishazi shurutiwa. Vipashio hivyo hutekeleza jukumu la kukitambulisha kishazi sharti na vile vile kuviunganisha vishazi viwili husika. Vinatekeleza jukumu hili la kuunganisha kwa kukitegemeza kishazi sharti kwa kishazi shurutiwa. Kwa hivyo, vitambulishi sharti hivi vya Kiswahili na vya Ekegusii vinatekeleza majukumu yaliyo sawa. Muundo msingi unaozaliwa huwa na maana kamilifu. Mifano inayofuata inawasilisha sentensi sharti katika kiwango cha muundo msingi na zilizo na maana kamilifu.

22. Kiswahili

a) [ Uchumi utakua [ kama [ teknolojia itaimarishwa. ] ] ]
KN KT KN KT

b) [ Watu watakuheshimu [ endapo [ utajiheshimu mwenyewe. ] ] ]
KN KT KT KN

23. Ekegusii

a) EK: [ Amache natoke [ onye [ embura kegotwa. ] ] ]
KN KT KN KT


KS: Maji yatapatikana kama mvua itanyesha.

b) EK: [ Chimbusuro nchimere [ ebe [ chiasimekirwe buya. ] ] ]
KN KT KT KE

KS: Mbegu zitamea iwapo zimepandwa vizuri.


Miundo ya sentensi sharti ya Kiswahili na ya Ekegusii iliyotolewa hapo juu inafanana. Kwa kutumia sentensi sharti za hapo juu tunaweza kuwasilisha muundo msingi wa sentensi sharti ya Kiswahili na ya Ekegusii katika vielelezo tungo vinavyofuata.

24. Kiswahili




Uchumi utakua kama teknolojia itaimarishwa.

25. Ekegusii




EK: Amache naatoke onye embura kegotwa.

KS: Maji yatapatikana kama mvua inanyesha.


Vielelezo tungo vya hapo juu vinaonyesha kufanana kwa muundo msingi wa sentensi sharti ya Kiswahili na ya Ekegusii. Kila lugha ina kishazi sharti kinachotokea baada ya kishazi shurutiwa. Vishazi hivi viwili vinaunganishwa kwa mujibu wa kukitegemeza kishazi sharti kwa kishazi shurutiwa kwa matumizi ya kiunganishi kitegemezi. Mfano hapa ni umbo ‘kama’ katika Kiswahili na ‘onye’ katika Ekegusii. Maumbo haya ndiyo wakati huo huo yanatekeleza lile jukumu la kutambulisha sharti.

Wakati wa kugeuza sentensi sharti ya Kiswahili kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo geuzi. Mchakato unaohusika unafanana na ule wa kugeuza sentensi sharti ya Ekegusii kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo geuzi. Hali hii inapelekea miundo nje inayozaliwa kufanana.


Wakati wa mchakato wa kugeuza sentensi sharti ya Kiswahili na Ekegusii unapotekelezwa, vishazi sharti katika lugha hizi hutangulizwa au kusogezwa kutoka sehemu iliyo kulia mwa kishazi shurutiwa hadi ile iliyo kushoto mwa kishazi shurutiwa. Vitambulishi sharti vilivyokuwa baina ya vishazi hivi, sasa hujitokeza mwanzoni mwa sentensi. Wakati wa kutanguliza kishazi sharti katika lugha hizi mbili, kunachochewa kuchipuka kwa kiunganishi kitegemezi ambacho si cha lazima katika lugha hizi mbili. Kiunganishi kitegemezi hicho ni ‘basi’ katika Kiswahili na ‘rirorio’ katika Ekegusii. Viunganishi vitegemezi hivi viwili hujitokeza kwa hiari. Huwa havijitokezi katika kiwango cha muundo msingi. Hutokea tu katika kiwango cha muundo geuzi kutokana na mchakato wa kukitanguliza kishazi sharti katika lugha husika ya Kiswahili na ya Ekegusii. Mchakato wa kugeuza sentensi sharti ya Kiswahili na ya Ekegusii kutoka

kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo inaonyeshwa jinsi inavyofanana na kuzaa miundo nje ambayo pia inafanana.

26. Kiswahili





27. Ekegusii





Vielelezo vya hapo juu vinafafanua mahali kishazi elezi cha sharti cha Kiswahili na cha Ekegusii vinapohamishwa na mahali vinapohamia. Vinasogezwa kutoka sehemu iliyo baada ya kishazi shurutiwa hadi ile iliyo kabla ya kishazi shurutiwa. Vielelezo viwili vya hapo juu vinawasilisha sentensi hizo katika kiwango cha muundo msingi. Baada ya usogezi unaoashiriwa na mishale katika vielelezo hivyo kukamilika, miundo ifuatayo huzaliwa. Hii ni miundo geuzi na ambayo inaonyesha kufanana baina ya Kiswahili na Ekegusii.

28. Kiswahili




29. Ekegusii





Mifano ya hapo juu inaonyesha kufanana katika jinsi sentensi sharti ya Kiswahili na ya Ekegusii zinavyogeuzwa kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kiwango cha muundo geuzi. Kishazi elezi cha sharti katika lugha hizi zote kinahamishwa kutoka sehemu iliyo baada ya kishazi shurutiwa sentensi ikiwa kiwango cha muundo msingi, na kusogezwa hadi sehemu iliyo kabla ya kishazi shurutiwa hivyo kuzalisha muundo geuzi. Wakati wa ugeuzi huo, kiunganishi kitegemezi ‘basi’ katika lugha ya Kiswahili na ‘rirorio’ katika lugha ya Ekegusii vinachochewa kuchipuka na hatimaye kuchopekwa baina ya kishazi sharti na kishazi shurutiwa. Kila kimoja cha viunganishi hivi kinakitegemeza kishazi sharti kwa kishazi kikuu. Hata hivyo viunganishi hivi si vya lazima. Vinatokezwa katika muundo geuzi pekee wa sentensi sharti na ni kwa hiari. Vinaweza kutokea au visitokee. Mageuzi haya yanafanana katika lugha hizi mbili.

Kutokana na ugeuzaji huu wa kukitanguliza kishazi sharti katika lugha hizi, inabainika kuwa vishazi sharti katika Kiswahili na Ekegusii vina uhuru wa kuhama na kutokea

sehemu kabla au baada ya kishazi shurutiwa. Vishazi sharti katika lugha hizi zote, vikiwa katika kiwango cha muundo msingi hutokea baada ya kishazi shurutiwa. Vikiwa katika kiwango cha muundo geuzi, vishazi sharti hutokea kabla ya kishazi shurutiwa. Kutokana na ufafanuzi huu ni dhahiri kuwa sentensi sharti ya Kiswahili inafanana na ya Ekegusii katika kiwango cha muundo msingi, ugeuzi na muundo geuzi.


Matokeo ya ugeuzi ambao tumeufafanua hapa yanaweza kuwasilishwa kwa matumizi ya vielelezo tungo ambavyo navyo vinadhihirisha kufanana kwa muundo wa sentensi sharti ya Kiswahili na ya Ekegusii.

30. Kiswahili.




Kama teknolojia itaimarishwa (basi) uchumi utakua.

31. Ekegusii.




EK: Onye embura kegotwa (rirorio) amache naatoke.

KS: Kama mvua inanyesha (basi) maji yatapatikana.

Vielelezo tungo viwili vya hapo juu vinawasilisha muundo geuzi wa sentensi sharti ya Kiswahili na ya Ekegusii. Miundo hii miwili inafanana. Miundo hii imezalishwa kutokana na kanuni ya usogezi inayokihamisha kishazi elezi cha sharti. Katika vielelezo tungo hivi viwili kishazi sharti kimehamishwa na kutangulizwa kikifuatiwa na kishazi shurutiwa.

# SURA YA TANO

## 5.0.0 HITIMISHO

Utafiti wetu umeweza kulinganisha sintaksia ya sentensi sharti ya Kiswahili Sanifu na ya Ekegusii kwa msingi wa nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi. Katika utafiti huu, imedhihirika kuwa sintaksia ya sentensi sharti ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii zinafanana kwa kiwango kikubwa sana.

Tulidhamiria kuchunguza miundo ya sentensi sharti ya Kiswahili Sanifu na ya Ekegusii ambapo tuliwasilisha nadharia tete kuwa miundo mingi ya sentensi zenye vishazi sharti katika lugha hizi mbili inafanana. Uchunguzi umepata kuwa miundo ya sentensi sharti katika lugha ya Kiswahili Sanifu na ya Ekegusii inafanana. Lugha hizi mbili zina sentensi sharti zilizo na miundo ya sentensi changamano. Hivi ni kusema kuwa sentensi sharti ya Kiswahili na ya Ekegusii zinaundwa kwa kishazi kikuu na kishazi tegemezi. Kishazi shurutiwa ndicho kishazi kikuu na kishazi sharti ndicho kishazi tegemezi katika lugha hizi mbili.

Sentensi sharti ya Kiswahili Sanifu na ya Ekegusii zikiwa katika kiwango cha muundo msingi zinafanana hivi kwamba vishazi shurutiwa vinatangulia vikifuatwa na vishazi sharti kwa mujibu wa mpangilio wa vishazi kama viambajengo vya sentensi sharti.

Uchunguzi umeonyesha kuwa sentensi hizi zinapogeuzwa kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo geuzi, mageuzi yanayotokea yanafanana katika lugha hizi mbili. Mageuzi haya yanaafikiana na lengo na nadharia tete iliyokuwa na wazo kuwa kanuni nyingi za ugeuzi zinazosababisha mageuzi katika sentensi sharti katika Kiswahili na Ekegusii zinafanana. Kwa mfano sentensi sharti katika lugha hizi zinapogeuzwa

kutoka kiwango cha muundo msingi hadi kile cha muundo geuzi, kishazi sharti kinatangulizwa kikifuatwa na kishazi shurutiwa. Yaani kishazi sharti kinatokea kabla ya kishazi shurutiwa sentensi ikiwa katika kiwango cha muundo zalishwa. Ugeuzi mwingine ni kuchipuka kwa kiambatishi kitegemezi katika Kiswahili na vile vile katika Ekegusii. Viambatishi vitegemezi hivi si vya lazima na hujitokeza tu katika muundo geuzi katika lugha zote mbili. Havitokei katika muundo msingi bali katika muundo geuzi pekee. Viambatishi vitegemezi hivyo ni ‘basi’ katika Kiswahili na ‘rirorio’ katika Ekegusii.

Uchunguzi huu umeonyesha kuwa kiwango cha muundo msingi na kile cha muundo geuzi vyote vinachangia kuwasilisha maana kwa matumizi ya sentensi sharti ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii hivyo kuafikiana na kaida ya nadharia ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi inayotambua mchango wa muundo ndani na muundo nje katika kuwasilisha maana. Sentensi sharti ya Kiswahili na ya Ekegusii huwasilisha maana kamilifu zikiwa katika kiwango cha muundo msingi na vile vile kiwango cha muundo geuzi.

Uchunguzi huu umeshughulikia vipashio vya masharti vitumiwavyo kama vitambulishi sharti katika lugha hizi mbili kufuatana na malengo na nadharia tete za uchunguzi huu. Imegunduliwa kuwa vipashio vinavyotumiwa kutambulisha masharti katika Kiswahili ni vingi kuliko vile vya Ekegusii. Matokeo ya kipengele hiki yanaafikiana na nadharia tete yetu iliyo na wazo kuwa vipashio vya masharti katika lugha ya Kiswahili ni vingi kuliko vya lugha ya Ekegusii. Uchunguzi umetambua jumla ya vipashio tisa vya masharti katika lugha ya Kiswahili ambavyo ni ‘kama, ikiwa, iwapo, endapo, ki, nga, ngali, nge, na ngeli’. Kwa upande wa lugha ya Ekegusii, vipashio vitano vimetambuliwa ambavyo ni pamoja na ‘onye, -ise, k-, ebe na –are’. Aidha tumetambua kuwa kuna vitambulishi sharti

huru na vitambulishi sharti funge katika lugha zote mbili. Vitambulishi sharti huru huweza kutokea kama maneno kamili yaliyo na maana iliyokamilifu. Vitambulishi hivi katika Kiswahili ni ‘kama, ikiwa, iwapo na endapo’. Katika Ekegusii, vitambulishi huru ni viwili ambavyo ni ‘onye na ebe’. Vitambulishi sharti funge huhitaji kuongezwa mofu nyingine ndio viweze kuwa na maana kamilifu. Haviwezi kutokea katika tungo bila kuunganishwa na mofu nyingine ili maana zao kuwasilishwa. Katika Kiswahili, vitambulishi vya aina hii ni ‘ki, nga, ngali, nge, na ngeli’. Katika Ekegusii ni ‘-ise, k- na -are’.

Utafiti huu umetambua kuwa katika lugha ya Kiswahili na ya Ekegusii kuna vitambulishi sharti vinavyotokea katika vishazi vyote viwili. Vitambulishi hivyo hutokea katika kishazi sharti na vile vile katika kishazi shurutiwa. Vitambulishi sharti hivyo ni ‘nga, ngali, nge na ngeli’ katika Kiswahili, na ‘-are’ katika Ekegusii. Sentensi zenye vitambulishi sharti vya aina hii zina miundo inayofanana katika Kiswahili na Ekegusii. Imebainika kuwa vitambulishi sharti hivi vyote iwe katika Kiswahili au Ekegusii vinafanana kwa kuwa vyote vina umbo la mofu funge. Haviwezi kujitokeza bila kutegemea kuunganishwa na mofu nyingine ndiposa viweze kuwasilisha maana.

Uchunguzi huu umeonyesha tofauti kubwa kati ya lugha ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii. Lugha ya Ekegusii inatumia toni kuwasilisha maana katika baadhi ya sentensi sharti. Lugha ya Kiswahili haina matumizi ya toni. Lugha ya Kiswahili huwa na sifa ya kutia mkazo katika silabi ya pili kutoka mwisho wa kila neno.

Tungependa kuhitimiza sehemu hii kwa kusema kuwa lugha ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii zinafanana katika sintanksia ya sentensi sharti kwa mujibu wa nadharia ya

Upanuzi wa Sarufi Sawazishi. Hali hii inathibitisha ule unasaba wa lugha hizi mbili kuwa zote ni lugha za Kibantu. Tofauti ndogo inayojitokeza baina ya lugha hizi mbili inaweza kuelezewa kutokana na kutengana kwa lugha hizi ambapo ziliishia katika maeneo tofauti kijiografia yaliyo na umbali wa masafa marefu na mazingira tofauti. Aidha urefu kiwakati baada ya kutengana huku kuliweza kusababisha athari dhidi ya maendeleo ya lugha hizi katika ujumla wake na hivyo kuzua tofauti tulizozijadili.

## 5.1.0 MAPENDEKEZO

Tunapendekeza hapa kuwa utafiti ufanywe kuhusu sentensi sharti ya lugha ya Kiswahili na ya Ekegusii kwa mujibu wa nadharia zilizozuka baada ya Upanuzi wa Sarufi Sawazishi.

Tunawapendekezea wanaisimu washughulikie aina mbalimbali za sentensi zilizo na muundo wa uchangamano katika lugha ya Kiswahili na Ekegusii, na lugha zingine za Kibantu.

## MAREJELEO

Chomsky, N. . (1977a), 'On Wh Movement'. In P. Culicover, T. Wasow, and A. Akimajian. (editors) (1977) *Formal Syntax.* New York:Academic Press, Inc.

_____(1965), *Aspects of the Theory of Syntax*. Cambridge, Massachusets: M.I.T. Press.

——— (1957), *Syntactic Structures*. The Hague: Mounton.

Bresnan J. (1978), A realistic transformational grammar, in M. Halle, J. Bresnan and G.A. Miller (eds), *Linguistic Theory and Psychological Reality*, Cambridge, MA. MIT. Press.

Crystal, D. (1999), *A Dictionary of Linguistic and Phonetics 4th Edition.* United Kingdom: Blackwell Publishers Ltd.

Gesare, H.L. (1992), *A Morphological Typology of Ekegusii in a Structural Framework.* M.A. thesis, University of Nairobi. (Haijachapishwa).

Gicheru, D.K (1999), *Ulinganishi wa Muundo wa Kikundi Nomino Cha Kiswahili Sanifu na Kikuyu Cha Kabete.* Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Guthrie, M. (1948), *The classification of Bantu Languages*. London: Oxford University Press.

Haegeman, L. (1992), *Introduction to Government and Binding Theory*.United Kingdom: Blackwell Publishers.

Hartman, R.K and Storm F.C. (1972), *Dictionary of Language and Linguistics*. London

Jacobsen, B. (1977), *Transformational Generative Grammar*. New York: North-Holland Publishing Company.

Jerono, P. (2003), *Kishazi Huru Arifu cha Kiswahili: Mtazamo wa X-bar.* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kariuki, A.W. (1997), *Sintaksia ya Virai Rejeshi katika Kiswahili Sanifu na Kikikuyu*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Katz and Postal P. (1964), *An Integrated Theory of Linguistic Descriptions*. Cambridge, MA: MIT Press.

Maw, J. (1969), *Sentences in Swahili; A study of their internal relationship*. London: Unwin Brothers Limited.

Mayaka, B.A. (2000), *The Structure of Ekegusii Sentences. A Transformational Generative Approach.* B.A. Thesis, University of Nairobi. (Haijachapishwa).

Mgullu, R.S (1990), *The structure of Swahili Sentensi. A Transformational Approach.* M.A. Thesis, University of Nairobi. (Haijachapishwa)

Mgullu, R.S (1999), *Mtalaa wa Isimu, Fonetiki, Fonolojia, na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers (Kenya) Ltd.

Myachina, E.N. (1973), *The Swahili Language: A descriptive Grammar*. London: Oxford University Press.

Obuchi, S na A. Mukhwana (2010), *Muundo wa Kiswahili, Ngazi na Vipengele.* Nairobi: A~Frame Publishers.

Oichoe M.P. (2005), *Ulinganishi wa Kirai Tenzi cha Kiswahili Sanifu na Ekegusii Kimofosintaksia: Mtazamo wa Uminimalisti*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Omusula, F.B (1998), *Ulinganishi wa Mifanyiko ya Kimofolojia Baina ya Mnyambuliko wa Kitenzi Cha Kiswahili na cha Kikabarasi*. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Platt, J.T. (1971) *Grammatical form and Grammatical meaning: A Tagmemic view of Fillmore's Deep Structure case Concepts*. Amsterdam and London: North Holland

Polome, E. (1967), *Swahili Language Handbook*. Washington: Centre for Applied Linguistics.

Poole, G (2002), *Syntactic Theory*. New York: Palgrave.

Sewangi, S. (1993), *The Syntax of Empty Category in Swahili simple Sentences*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Radford, A. (1981***),*** *Transformational Syntax*. Cambridge: Cambridge University Press.

Tuki (1990), *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salam: TUKI.

Wesana-chomi, E (1986), *Towards the syntax of complex sentences. Kiswahili*. Vol. 43/2.

Williams, E. and Riemsdijk, H.V (1986***).*** *Introduction to the Theory of Grammar*. Cambridge, Massachusets. The M.I.T Press.